ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 13 April, 2012

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mahamoud Muhammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Asaa Othman Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari) Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi) Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 111

Makaazi Duni ya Askari wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua ikiendeleza sera ya makazi bora kwa wananchi wake.

(a) Je, kwanini Askari wa Vyuo vya Mafunzo wanaishi katika nyumba chakavu na zisizotosha kwa kuishi wao na familia na kulazimika kukosa faragha.

(b) Je, Serikali haioni ni ukiukwaji wa haki ya faragha ya kikatiba kwa Askari kuishi katika chumba kimoja pamoja na watoto wenye umri wa utu uzima.

(c) Mhe. Waziri tatizo la ukosefu wa nyumba bora za Askari wa Vyuo vya Mafunzo litachukua muda gani kupatiwa ufumbuzi wake.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 111(a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi sio tu katika Vyuo vya Mafunzo bali hata katika Idara Maalum nyengine zinakabiliwa na tatizo kubwa la Makaazi kwa Maafisa na Wapiganaji wake. Kwa upande wa Vyuo vya Mafunzo juhudi za makusudi zinachukuliwa na Serikali kukabiliana na tatizo hili ambapo kwa mwaka huu wa fedha wa 2011/2012, nyumba ya familia mbili katika kambi ya Kangagani kwa upande wa Pemba inaendelea kujengwa na matengenezo ya nyumba za Maaskari katika kambi za Ubago na Kinumoshi kwa upande wa Unguja vile vile zinaendelea kujengwa.

Serikali inakusudia katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuondoa kabisa tatizo la ukosefu wa nyumba bora za Askari na Maofisa wa Vyuo vya Mafunzo. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Kipya

kinachotarajiwa kujengwa Hanyengwa Mchana nako kutatatua kwa kiasi kikubwa tatizo hili ambapo jumla ya nyumba mpya sita (6) za ghorofa moja za maofisa na nyumba ndogo ndogo 30 kwa ajili ya Askari wa kawaida zinatarajiwa kujengwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Mhe. Waziri unajua kwamba tatizo hili linanyima hata fursa ya faragha kwa kupanga uzazi serikali imefanya tathmini kuondoa tatizo hili kiasi gani cha fedha.

b) Kutokana na umuhimu wa suala la makaazi Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutumia vikosi vyake vya SMZ kwa kujenga nyumba kwa ajili ya makazi yake.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, amezungumzia suala la faragha najua kuna tofauti kidogo wakati zile nyumba zilivyo kuna nyumba za maafisa na kuna nyumba zile za askari wa kawaida. Sasa askari wa kawaida mara nyingi nyumba zao huwa kama bangaloo lakini mna chumba kimoja kimoja kwa wale ambao ndio kwanza wanaanza kazi au wana familia ndogo.

Lakini kama nilivyosema tuna mpango sasa wa kuhakikisha tunawapa nyumba zenye stara, sasa hili suala la faragha kweli nakiri kwamba kidogo halipo sasa tutajitahidi kuona tunawapa stara nzuri nao waishi kama binaadamu.

Kuhusu kujenga kutumia vikosi ni kweli hilo tutalifanya na tunaendelea kulifanya vikosi vyetu vyote vina kitengo cha ujenzi, mbali ya kujenga katika idara zao lakini pia wanachukua *contract* hata nje, kwa hivyo tunakuomba Mhe. Jaku kama una ujenzi huko nao wanaingia tena kwenye tenda sio kama wanapendelewa wanaingia kwenye tenda wanashindana kwa hivyo tusaidiane ili kuutunisha mfuko wao.

Nam. 150

Huduma za Zimamoto na Uokozi Baharini

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Ili kuhakikisha kwamba huduma za uzimaji moto baharini zinapatikana ipasavyo, ni vyema kikosi cha Zimamoto na Uokozi kikapatiwa Boti za Kisasa zenye kuweza kutoa huduma hiyo.

(a) Je, kwa sasa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinamiliki boti ngapi za uokozi.

(b) Je, Kikosi cha Zimamoto kimeweka mipango gani kutoa huduma ya dharura kwa Askari wa Zimamoto na Uokozi anapoumia katika kutoa huduma ya kuzima moto, hasa baharini.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 150 (a), na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe, Mwenyekiti kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mbarouk Mussa Wadi kwa kufuatilia usalama wa wananchi katika maeneo yake au katika jimbo lake, napenda sana maswali yake hasa ya upande wa zimamoto na hii inatupa changamoto sisi kufuatilia kwa makini sana, wiki iliyopita aliuliza swali moja kwamba pale pana *Land Rover* pale Mahonda lakini sio *Land Rover* tu lakini pana gari kamili la kuzimia moto naomba nimpe taarifa ile tu, kwa sababu aliuliza swali lile.

Sasa baada ya utangulizi huo naomba nimjibu swali lake kama ifuatavyo:-

a) Kwa sasa hivi Kikosi cha Zimamoto hakina Boti ya kuzimia moto. Hata hivyo mipango madhubuti inafanywa kuona vyombo hivyo vinapatikana haraka iwezekanavyo ili Kikosi kiweze kuzitumia wakati wa maafa ya baharini yatakapotokezea. Hivi sasa Idara Maalumu ya Zimamoto na Uokozi inategemea boti (Tagi) ya Shirika la Bandari ambayo inauwezo wa kuzima moto baharini.

b) Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinatoa huduma ya dharura ya malipo ya fidia kwa Askari na Maofisa kwa Kikosi wanapoumia wakati wanapotoa huduma kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine wa serikali inapotokezea wanapoumia kazini.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kua nchi yetu ni ya visiwa na kuna usafiri wa meli ambao unatoka hapa usiku hasa kuelekea Dar es Salaam kwa nyakati za usiku, kwa mujibu wa maelezo yako Mhe. Waziri umesema kwamba kikosi hiki hakina boti ambayo inaweza kwenda kuzima moto wakati wowote ule kwa baharini, katika maelezo yako umesema mipango inafanywa kuweza kupata hiyo boti.

a) Mimi nilikua nataka kujua kwanza ni mipango gani hiyo inayofanywa na lini itakamilika.

b) Lakini usafiri unaofanywa usiku unaonekana ni wahatari zaidi kama kutakua hakuna boti ya uokozi kama ambavyo tumeona hivi karibuni katika *MV. Spice Islender* ile ilizama tu haikuwaka moto na uokozi wake ulichukua muda kiasi kile. Sasa je itakapotokezea boti imewaka usiku ni hatua gani mtakazochukua kuhakikisha kwamba watu walikuwemo katika boti ile wanaokolewa maisha yao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kama nilivyosema kwamba serikali imo kwenye mipango na tukisema kwenye mipango basi bila ya shaka tunaingiza kwenye bajeti, hivi sasa ndio tunatayarisha hiyo bajeti tutatizama unajua hivi vitu ni ghali sana, kwa mwaka huu tunaweza kutoa japo nusu kama ununuzi wa kiserikali unavyokwenda. Kwa sababu nakumbuka juzi nilizungumza ununuaji wa gari sasa tunakamilisha ununuaji wa gari ya nchi kavu na hatua hii itafuata. Kwa hivyo siwezi kusema lini lakini serikali inajitahidi nalo hili kuona umuhimu wake.

Pili aliuliza kuhusu hadhari ni kawaida kwa chombo chochote cha baharini kwa hivyo vyombo ambavyo vinatambulika ambavyo vinaorodheshwa kwa kuchukua abiria wana utaratibu wa kuweka vitu vile vya kuzimia moto, wanaweka ndani ya meli na hata ile mipira ya maji utaona kuna njia zao za mipira ya maji wanaita *FIRE hourse* au *water house* kwenye meli utaona mote mle mmezunguuka mapira yale na yale yamewekwa maalum kwa hadhari pindi moto ukitokezea. Sasa cha muhimu labda tukubali kwamba mbali ya wale wafanyakazi waliomo mle ndani wenyewe wanaojua kutumia, lakini hata raia ukitokea moto nao wafundishwe vipi waweze kusaidia.

Hili tutalichukua tutoe elimu kama unavyopanda ndege ukikaa katika mlango wa dharura unafundishwa jinsi ikitokea dharura ufungue vipi na wao watoe elimu kuwasidia watu wetu ikitokezea hali kama hiyo wafanye vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Waziri lakini kwa ruhusa yako naomba niongezee nyongeza kama ifuatavyo. Hivi karibuni Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atafanya ziara kwenda nchini Israil kwa madhumuni makubwa ya mazungumzo kuhusu vifaa vya uokoaji hapa Zanzíbar, kwa hivyo huo ni mmoja katika mpango ambao serikali inakusudia kuufanya kwa nia ya kuweza kupata vifaa, hata hivyo hivi sasa tunatayarisha orodha ya vifaa vya uokoaji ili kuiwasilisha katika serikali ya China kwa ajili ya msaada kama huo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri hivi karibuni meli ya MV. Serengeti iliwaka moto ilikuweko nje ya Serena kule na kwa bahati nzuri watu hawakuwepo. Je, Mhe. Waziri sasa hivi hapa Mhe. Waziri wa Nchi katika Afisi ya Makamo wa Pili amesema kwamba Makamo wa Pili atakwenda katika nchi za huko kwenda kuhangaikia suala hilo.

a) Hatuoni kwamba sasa hivi hili suala serikali haioneshi umuhimu wowote wa kuweza kupatikana chombo hicho.

b) Je, kwa nini tusiweze kutafuta gari moja ambalo katika sehemu zilizokuweko nyingi tukasema tuliuze ili kutafuta usafiri wa baharini ambapo hata boti moja mpaka sasa hivi haijakuwepo na kila leo vyombo vinasafiri na abiria.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Hivi juzi tu kulitokea moto mwengine jina la meli siikumbuki kulikua na meli ndogo iliungua pale na ilipoungua bahati mbaya hii meli ambayo tunaizungumza ya tagi nayo iliharibika, lakini kwa mashirikiano ya Shirika la Bandari na Shirika la Meli na kikosi chetu cha zimamoto na wapiganaji wengine wote tulipata boti pale tukatumia pampu za maji za kawaida ambazo zile zinatumika popote na kutumia maji ya baharini, maana yake lazima ufikirie maji kiasi gani tunaweza kuchukua.
Lakini vijana wetu wamefanya ubunifu kwa pampu ile ya baharini wanachukua kwa pampu na moto ule ukazimwa na mambo yakawa salama.

Kwa hivyo namhakikishia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba serikali iko macho na inalifuatilia suala hili kwa makini na hatutokaa tukaona kwamba maisha ya watu au vyombo vya watu viteketee, tunafanya kila juhudi kila mbinu kuona kwamba hali hii inakwenda vizuri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tulipata matatizo ya MV. Spice Islander kuzama na ikabidi tukapata shida sana kwenye uokozi kwa sababu ilikua hata pale ilipo meli hapajulikani, sasa katika vifaa hivyo vinavyotafutwa vya uokozi Helkopter ni moja ya vifaa vya uokozi ili kuwajua watu inapotokea ile ajali na watu kupata urahisi wa kuokoa.

a) Je, kwa hivi sasa tuna helkopter ngapi za uokozi hapa Zanzíbar.
b) Je, kama hatuna kwa nini serikali haioni kama kuna haja ya kutafuta japo helkopter moja ili inapotokea ajali ikawa ni rahisi kujua ajali imetokea wapi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, panapo uwezo sio tatizo na fikra yake ni nzuri kama serikali tunaichukua na tutaizingatia.

Nam. 52

Wafanyakazi wa Afya

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Kwa nia njema mwaka huu tulionao SMZ chini ya Wizara ya Afya imeajiri wafanyakazi wengi wakiwemo wauguzi, madaktari na kadhalika na kuamua kuwasambaza Zanzibar yote. Wapo wafanyakazi wanaoishi Unguja wamepelekwa Pemba na wale wa Pemba wamepelekwa Unguja.

(a) Je, Wizara iliajiri wafanyakazi wangapi.

(b) Wangapi miongoni mwao walipangaiwa Unguja na wangapi waliopangiwa Pemba.

(c) Zipo taarifa kua karibu wafanyakazi 20 waliopangiwa kwenda Pemba wameondoka au hawakuripoti kabisa. Je, ukweli ukoje.

(d) Iwapo wafanyakazi hao hawakuripoti Pemba, mishahara yao inatoka vipi.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 52 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kukabiliana na upungufu wa wafanyakazi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Afya iliajiri wafanyakazi wa kada mbali mbali na kuwasambaza nchini.

(a) Jumla ya wafanyakazi 267 waliajiriwa ambao waliomaliza masomo yao mwaka 2011 katika chuo cha Sayansi za Afya Mbweni.

(b) Wafanyakazi waliopangiwa Unguja 105 na Pemba 162
(c) Hadi kufikia March 2012 wafanyakazi waliopangiwa kwenda Pemba na kuondoka na wale ambao hawakuripoti kwa sababu tofauti jumla yao walikua 34.

(d) Utaratibu wa Serikali kulipa wafanyakazi wake ni kwa kupitia kwenye akaunti zao. Kila muajiriwa alipeleka namba ya akaunti yake katika mchakato wa kuajiriwa na mishahara yao ilipelekwa kwenye akaunti hizo. Kwa wale waliobainika kutokwenda au kuondoka Pemba majina yao yaliorodheshwa na taarifa zilipelekwa Utumishi na mishahara yao ikazuiliwa na baadae taarifa zikapelekwa Wizara ya Fedha na majina yao yakaondolewa kwenye malipo ya mishahara "*pay roll*" na fedha zinabaki kwenye akaunti ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutoa majibu mazuri hata hivyo naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Kwa kua alikiri kwamba kuna wafanyakazi ambao Pemba hawakuripoti kwa sababu mbali mbali lakini Mhe. Waziri anakubaliana nami kwamba wafanyakazi hawa wamesomeshwa kwa fedha za serikali, hatua ya kuwazuilia mshahara ni hatua moja lakini kinidhamu Wizara imechukua hatua gani ili kuwa fundísho kwa wafanyakazi wengine kwamba pale ambapo wameomba kazi na tayari wamejaza mkataba basi nidhamu ya serikali izingatiwe.

Mhe. Waziri wa Afya: Kwanza naomba kumshukuru kuona kwamba kuna umhimu kwa wafanyakazi wanaoajiriwa kuripoti panapotakiwa na kufuata nidhamu za kiserikali, hatua zinazochukuliwa ni za aina mbili bahati nzuri Waziri wa utumishi wa umma yupo hapa ni kwamba ninavyojua mimi kwamba kuna taarifa au sheria ya serikali katika kudhibiti watu wanaosomeshwa na serikali kwa kutumia fedha za serikali, wakishapata elimu wakajiona ni muhimu zaidi wakaondoka bila ya kuzingatia umuhimu wa taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, hawa ambao majina yao tunayo utaratibu tunaotaka kuchukua ili kudhibiti suala hili kwa wengine ni kuwaita wazee wao na kuwaambia kwamba itabidi wawajibike, kwa kua watoto wao walikua wamesomeshwa na serikali na wao itabidi tuwawajibishe ipasavyo. Ni hatua gani zitachukuliwa ni suala la mashirikiano kati yetu sisi na Wizara ya Utumishi.

Lakini naomba kwa kutumia nafasi hii kueleza na nimeshawahi kueleza hapa kwamba sote sisi hapa tumesomeshwa na serikali na tuna wajibu wa kuitumikia serikali, wenzangu nadhani wachache waliokuwemo humu sisi tulipomaliza *degree* mwaka 1975 tulitakiwa kujenga taifa na tulikua tunalipwa shilingi mia moja na arubaini na nne tu (144) tukiita *cross* kwa mwaka mzima na baada ya hapo tukawa tunalipwa shilingi elfu na mia moja (1,100) kwa mwaka mwengine mzima na baada ya hapo tena ndio tukawa tunazingatiwa kama tuna hadhi ya kupata nyongeza na mshahara unaostahiki.

Yote hayo ilikua kusaidia kulipia angalau kwa kiasi fulani gharama ya ile elimu iliyolipwa na michango ya masikini, sasa hili wazee wanahitaji kulizingatia nakumbuka katika kujibu suala katika kikao kilichopita, inasikitisha kuona kwamba wataalamu tuliokua hatuna nchi hii ni wale wa nusu kaputi tumewachukua watoto kwa miadi na mikataba pamoja na wazee wao tumewapeleka Chuo cha Moshi, wamesoma kwa pesa kamili za serikali walipomaliza wamerudi wawili.

Wawili mpaka leo hawakurudi wanaona wao wakatafute palipokua pazuri wamesahau kabisa kwamba serikali ililipia. Kwa hivyo natoa wito tushirikiane wazee sisi humu ni wazee wa watoto na wale wanaonisikiliza kwamba juhudi za serikali ni kuongeza huduma za afya ziwe nzuri tukiwa hatuna wafanyakazi tunalaumu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu serikali iliongeza wafanyakazi hawa kwa nia ya kutatua matatizo katika hospitali mbali mbali katika nchi yetu na kwa kua wafanyakazi hao walipangiwa sehemu mbali mbali lakini hawakuhudhuria au hawakuitikia wito huo.

a) Je, kwa sasa serikali imeshaajiri watu wengine kwa ajili ya kuziba mapengo yao.

c) Je, kama bado vile vituo ambavyo walikua wamepangiwa je upungufu ule utakua bado unaendelea au utakua umeondoka.

d) Kama ni hivyo ni hospitali gani ambazo zilikua zimepangiwa hawa watu na hawakwenda.

Mhe. Waziri wa Afya: Mule ambamo wamepangiwa na hawamo bado bila ya shaka kutakua na matatizo ya hapa na pale, kazi walizopangiwa zinafanywa kwa dharura na wale waliokuwepo na kwasababu hiyo mwahali mwengine hua wanatoka kituo kimoja kusaidia chengine. Lakini kwa taarifa ya Baraza hili kuna watoto

wengine kiasi mia tatu tena kutoka chuo hicho hicho cha Mbweni wanamaliza na kamati yangu inayosambaza wale wafanyakazi imeshafanya

Nam. 59

Wodi ya Wazazi Wete Pemba

Mhe. Ashura Sharif Ali – Aliuliza:-

Tunashukuru Serikali yetu pamoja na washirika wenzetu wa Maendeleo kwa huduma za kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto. Kwa upande wa Hospitali ya Wete mazingira ya wodi ya wazazi si mazuri na hawana vitanda maalumu kwa ajili ya kujifungulia. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwaondoshea tatizo hilo ili kuwarejeshea mazingira mazuri.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika**,** kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 59 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara kupitia mradi wake wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kinamama wajawazito na watoto unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ADB ina mpango wa kulifanyia matengenezo makubwa jengo hilo. Baada ya kukamilika kwa matengenezo hayo kutakua na wodi za kisasa za wazazi, vitanda, vifaa pamoja na chumba cha upasuaji mkubwa kwa akina mama wajawazito ambao wameshindwa kujifungua kupitia njia ya kawaida.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona mda huu, kwa kuwa anategemea matengenezo haya, anaweza kutwambia lini matengenezo hayo yanaweza kufanyika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, tulitegemea matengenezo hayo yangeanza mwaka huu. Lakini taratibu za taasisi za kimataifa zinataratibu zake. Hivi sasa sisi katika fedha zilizobaki kwenye mradi wetu wa ADB tuliojengewa nyumba na vituo, tumeshaziomba na tumeshakubaliwa, lakini mradi huu upo pamoja na Tanzania Bara. Tunapotaka sisi tupeleke moja kwa moja tunatakiwa ripoti yetu iyende pamoja na Tanzania Bara. Sasa Tanzania Bara wao walikuwa hawajakamilisha, sisi tumeshafikisha, nimejitahidi kulisukuma ili liwahi mapema. Hivi ninavyozungumza barua inatoka Wizara ya Afya Bara inaingia Wizara ya Fedha ya Muungano. Nilitaka kwenda mwenyewe Wizara ya Fedha Muungano kulisukuma lakini taratibu nyengine zinakuwa haziniruhusu.

Ukweli ninachoweza kusema ni kwamba mpaka pale utakaporudi mrorongo huo wa kimangimeza ndipo ujenzi utaanza. Kama utawahi hivi sasa tutaanza hivi sasa kama haitowahi tutahaulisha fedha hizi katika bajeti inayofuata.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa malengo ya melenium ni kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga. Mhe. Waziri katika jibu lake umeelekeza kutatua tatizo la muda mrefu. Je, Wizara yake ina mpango gani wa dharura wa muda mfupi, kutatua tatizo hili ambalo limeulizwa na Mhe. Ashura.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kila nikimuona Mhe. Rashid Seif napata furaha kwamba afya yake inaendelea vizuri. Suala la dharura kwa Hospitali ya Wete, pale tuna daktari mmoja kwa magonjwa ya akina mama ambaye anaitwa dokta Omar Issa Mgongo, yeye ni *specialist* aliyepelekwa katika kusaidia shughuli hizo. Mwanzo kulikuwa hata huyu hayupo. Kwa bahati nzuri yeye katika kumpa moyo huyu anapewa motisha zaidi na hiyo Fund ya ADB ili ile kazi yake aifanye vizuri. Suala la dharura tunafanya. Pale inapohitaji madaktari kupelekwa kwa dharura tunapeleka, lakini kwa sasa hiyo ndiyo hali tuliyonayo. Angalau tuna *specialist* mmoja na huduma za pale kwa ujumla za uzazi zinaendelea vizuri kama inavyotakiwa.

Nam. 90

Matokeo Mabaya ya Mitihani ya Form IV

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:-

Hivi karibuni Baraza la Mitihani Tanzania *NECTA* lilitangaza matokeo ya mitihani ya kidago cha nne (Form IV) ya mwaka 2012. Matokeo hayo yanaonyesha kwamba kwa Zanzibar hali ni mbaya sana, wanafunzi wengi hawakupata vyeti (div -0) na hao waliopata vyeti wamepasi masomo ya dini na kiarabu tu. Mwelekeo ni kwamba Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo walimu kutoka sifa za kutosha za kufundisha, wanafunzi wengi hushindwea kufahamu lugha ya kiingereza ambayo ndio lugha ya kufanya mitihani, na ukosefu wa tathmini sahihi ya viwango vinavyofundishwa. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani endelevu katika kukabiliana na changamoto hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 90 kama hivi ifuatavyo:

Kwanza naomba kutoa maelezo tangulizi. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba hivi karibuni Baraza la Mitihani la Tanzania lilitangaza matokeo ya mtihani wa kidatu cha nne ya mwaka 2011. Matokeo haya yalionesha kuwa jumla ya watahiniwa wa skuli 180,216 sawa na asilimia 53.59 ya watahiniwa wote wamefaulu mitihani yao. Kiwango hicho cha kufaulu kimeongezeka ukilinganisha na asilimia 50.4 ya mwaka 2010.

Kwa upande wa Skuli za Zanzibar watahiniwa 8,081 sawa na asilimia 75.93 ya watahiniwa wote wa skuli za Zanzibar wamefaulu mitihani yao. Kwa upande wa Tanzania Baraza asilimia ya watahiniwa waliofeli ni asilimia 46.41na kwa upande wa Zanzibar ni asilimia 24.1.

Kwa upande wa wanafunzi waliofaulu na kupata vyeti vya daraja la kwanza mpaka la tatu kwa Tanzania nzima ni watahiniwa wa skuli 33,577 sawa na asilimia 9.98 ya watahiniwa wote kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni watahiniwa 939 sawa na asilimia 7.9 watahiniwa wote.

Uhashidi huo unadhihirisha kuwa watahiniwa skuli za Zanzibar hawajafanya vibaya ukilinganisha na watahiniwa wa Skuli za Tanzania Bara kinyume na dhana ya Mheshimiwa Mwakilishi. Pamoja na matokeo haya Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba bado sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo uhaba wa madarasa, maabara, vitabu vya kufundishia, uhaba wa walimu wenye sifa za kufundishia hasa masomo ya sayansi, hisabati na kiingereza.

Pia Wizara ina changamoto ya ufatiliaji wa tathmini ya maendeleo ya wanafunzi wetu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti naomba kujibu swali lililoulizwa na Mhe. Shadiya kama ifuatavyo:-

Wizara yangu hivi sasa imeanza kukamilisha taratibu za uajiri wa walimu 240 wenye shahada na stashahada za ualimu kwa ajili ya skuli za Sekondari Unguja na Pemba . Uajiri wa walimu hawa utasaidia katika kupunguza uhaba wa walimu katika skuli za sekondari, pia skuli mpya 13 za sekondari zinazotarajiwa kufunguliwa hivi karibuni zitapunguza msongamano wa wanafunzi katika baadhi ya skuli zetu za sekondari na kutoa mazingira mazuri ya kusomea. Vile vile vitabu vya masomo yote vya sekondari vimesambazwa katika skuli zetu zote.

Aidha Wizara yangu inaendesha mafunzo mbali mbali ya walimu wa sayansi, hesababi na kiingereza kupitia vituo vya walimu. Mafungo hayo nayo yanachangia sana katika kuimarisha uwezo wa kufundishia kwa walimu wetu. Pia serikali imeunda Baraza la Mitihani ambalo rasimu yake ya sheria imepitishwa na Baraza lako tukufu. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shadiya Muhammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri inaonekana skuli nyingi za mashamba ndizo ambazo hazikufanya vizuri. Je, kuna sababu gani za msingi zilizopelekea maskuli hayo kutokufanya vyema mitihani yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alivyozungumza Mhe. Shadya alivyouliza kuwa skuli zetu za mashamba inaonekana zinafanya vibaya mwaka hadi mwaka. Wizara ya Elimu tumeliona suala hilo na sababu za msingi ambazo zinapelekea wanafunzi wetu wa skuli za mashamba kufanya vibaya ni hizi ambazo nimezieleza. Baada ya matokeo haya tulifanya ziara hususan katika zile skuli ambazo zimefanya vibaya , tukenda tukatizama tatizo hasa ni nini.
Moja ambalo tumeligundua ni kutokuwajibika kwa baadhi ya walimu. Walimu hawamalizi *syllabus* zao. Walimu wanachelewa kufika skuli na kuanza kusomesha watoto. Mbali ya hayo hata walimu wetu wakuu

wengine inaonekana uwezo wao wakusimamia skuli ambazo tumewakabidhi ni mdogo. Kwa hivyo Wizara hili wameliona na watalifanyia kazi.

Lakini mbali ya hayo nimezungumza katika jibu langu la msingi kuwa tunaskuli 13 ambazo tunatarajia kuzifungua hivi karibuni na skuli hizi nyingi zao zipo mashamba. Tunatarajia skuli hizi tukizifungua zitatupunguzia huu msongamano wa watoto kukaa kwa wingi katika darasa. Sababu moja kubwa ni hiyo, wanafunzi wetu wanakuwa ni wengi katika madarasa kiasi ya kuwa mwalimu anayefundisha uwezo wake unakuwa ni mdogo kuwafikia. Skuli hizi tukizifungua na kwa vile zitakuwa ni skuli za kisasa zenye maabara basi matatizo haya ya kufeli watoto wetu yatapungua kwa kiasi kikubwa na baada ya hizi hatua ambazo wizara tutachukua za kuwafatilia hawa walimu wetu ambao hawawajibiki kisawa sawa kufanya kazi zao.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa matokeo mabaya yamesababishwa na uvujishaji wa mitihani na kupelekea kufutiwa matokeo wanafunzi wetu. Je, ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa waliohusika na uvujishaji wa mitihani hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, hatua tunazichukua zile ambazo amezizungumzia Mhe. Waziri wa Elimu ambaye kamaliza muda wake juzi hapa kenda katika Wizara nyengine. Lakini tuna kamati ambayo tumeiyunda ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, baada ya ripoti ambayo watatukabidhi Wizara basi hapo tunaweza tukachukua hatua rasmi. Kwa hivi sasa ni mapema mno na namuomba Mheshimiwa aridhike na hilo ili atuachie wizara tufatilie zaidi kadhia hii.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu lako umesema kwamba kuna baadhi ya walimu wakuu uwezo wao kufuatilia ni mdogo. Pia umetamka kuwa una malengo ya kufungua skuli nyengine 13.

Je, wizara yako imejipanga vipi katika kutafuta walimu wenye uwezo zaidi wakati hawa waliokuwepo baadhi yao hawana uwezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nimesema kwama kuna baadhi ya walimu wakuu uwezo wao ni mdogo wa kusimamia kazi ambazo tumewakabidhi. Hatua ambazo tutachukua ni zile ambazo nimezizungumza kama tutawachukulia hatua. Mimi nadhani hilo watuachie.

Na hizi skuli 13 ambazo nimezisema hapa, walimu ambao watasomesha skuli hizi ni walimu hawa 240 ambao tumewaajiri, tutawapeleka katika skuli za shamba, Pemba na Unguja. Pia tuna walimu 10 kutoka Nigeria ambao pia tunatarajia kuwaajiri hawa kwa masomo ya sayansi na hesabati, hawa watatusaidia sana.

Jambo ambalo Mhe. Mwenyekiti, nataka wajumbe wa Baraza lako tukufu wanisaidie kwa sababu wao ni wawakilishi ambao wanatoka katika majimbo yao. Hawa walimu ambao tunawaajiri wanatoka ndani ya skuli zao. Katika walimu 240 Pemba ni walimu 32 tu ambao wameomba, na tuna tatizo kubwa la walimu Pemba. Katika walimu hao 32 walioomba, walimu 23 ndio waliokuja Wizarani na kuchukua mikataba. Baada ya hapo walimu waliobakia ni 21, wawili wameshachukua mikataba, tumeshawakubalia wameondoka wanakwenda kufanya kazi Bara.

Tatizo hili waheshimiwa tulione, tunawasomesha, wanafunzi watoto wetu lakini hawawasaidii ndugu zao, uzalendo unakuwa ni mdogo kwao. Kwa hivyo licha ya serikali kutoa pesa nyingi kuwasomesha wanafunzi mwaka hadi mwaka lakini vijana wetu uzalendo unakuwa ni mdogo sana. Hili ni jukumu lenu Waheshimiwa Wawakilishi tukishirikiana pamoja tutaweza kuwashawishi watoto wetu, ndugu zetu, kama vile ambavyo wamesomeshwa wao na serikali hii basi na wao wasione tabu kuwasomesha ndugu zao na watoto wetu. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam 114

Ukosefu wa Umeme Katika Kijiji cha Jambiani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua hatua ya kufikisha huduma ya umeme Vijijini.

(a) Mhe. Waziri, kwanini wananchi wa Kijiji cha Jambiani wameendelea kukosa huduma ya umeme licha ya kujitolea kununua nguzo za kufanikisha mradi huo.

(b) Kwa kuwa wananchi tayari walinunua nguzo kuna sababu gani zilizopelekea kutounganishiwa umeme huo na kuwasababishia hasara ya shilingi milioni 1.080.

(c) Je, Wizara inashirikiana vipi na wananchi wanapoamua kuchangia mradi ili kuhakikisha vifaa wanavyonunua vinazingatia viwango vya ubora na mahitaji yake.

(d) Je, serikali ina mpango gani wa dharura wa kuondoa tatizo hilo hasa kwa kuzingatia umeme ndiyo injini ya maendeleo kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 114 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, sehemu kubwa ya wananchi wa Kijiji cha Jambiani wananufaika na huduma ya umeme,ila wananchi tunao wazungumza kutonufaika na huduma hii ni kwamba wao waliamua wenyewe bila ya kufuata ushauri wa kitaalamu na kufuata taratibu zinazohusika waliamua kununua nguzo zilizo chini ya kiwango na kuamua kujenga laini ya umeme bila ya kibali cha Shirika la Umeme.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kutokufuata taratibu za uunganishwaji wa umeme huo na Shirika kuchukua tahadhari za wananchi na usalama wa mali zao ndio sababu iliyopelekea kutokuunganishiwa wananchi hao umeme.

(c) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme linathamini sana michango ya wananchi katika kujiletea maendeleo hayo. Hivyo tunashauri katika suala hilo la kuunganisha umeme mtu yoyote anayetaka kuunganisha umeme afika katika afisi zetu za Shirika la Umeme kwa kupata muongozo na kufata utaratibu wa shirika hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kusikitisha ya rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Je, serikali inachukua hatua gani ya kukamilisha hatua iliyobaki hata kama taratibu hazikufuatwa, ukiangalia jukumu la serikali ni kuwaletea maendeleo wananchi.

(a) Unatoa kauli gani kwa wananchi wa jimbo la Jambiani wakati wametumia gharama karibu shilingi milioni tatu ikiwemo nguzo, waya na vikombe. Wanataka kujua hivi sasa wananchi ni hatua gani wizara yako itachukua.

(b) Kwa kuwa Naibu Waziri mradi huo haukufuata taratibu je, mtoto katika familia kumsaidia mzazi kununua kitoweo ni kosa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nieleze kwamba wananchi hao wamefanya kazi ya kuvuta laini kinyume na utaratibu, kama nilivyoeleza katika jibu mama. Wananchi hawa wa Jambiani/Mfumbwi walijivutia laini wenyewe bila ya kupita Shirika la Umeme na kupata kibali cha shirika, isitoshe kwamba wananchi hao wametumia nguzo ambazo hazikuwa na kiwango.

Nguzo zetu za Shirika la Umeme kwenye line LV zinatakiwa ziwe kutoka mita 9 hadi mita 10, nguzo ambazo wamezitumia wao hasikufikia hata mita 8, ilikuwa zipo katika kiwango cha mita 7 kuja na chini. Isitoshe katika laini za HT inatakiwa isipungue kiwango cha mita 13 hadi 14, wananchi hao wao hawakuzifikia katika kiwango hicho. Isitoshe wananchi hawa baada ya kujiunganishia umeme Shirika langu la umeme limewataka wananchi hawa wafike Shirika la Umeme ili wapewe muongozo.

Katika utaratibu wa shirika letu ni kwamba tunapoikuta laini ambayo imevutwa kinyume na utaratibu basi tunaishusha laini hiyo ikisha tunaitaifisha vifaa vyote ambavyo vimetumika katika laini hiyo. Lakini kwa busara na kwa hikma wananchi hao hatukutaka kuwataifishia vifaa isipokuwa tumewaita, tuwape muungozo, baadaye tuvitumie vifaa hivyo hivyo waya, *T.Off, tension*, pamoja na vikombe katika kuwavutia line, isipokuwa tu tunachotaka tubadilishe nguzo hizo na wao tuwapitishe katika utaratibu wa kisheria unaofaa. Serikali ya

Mapinduzi Zanzibar kupitia Shirika la Umeme lina nia nzuri ya kuwaunganishia wananchi huduma hiyo ya umeme.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilichotaka kujua mimi nguvu za wananchi serikali inazithamini au hawazithamini kwa kuwa wamefanya jitihada kubwa sana, wananchi wale. Wao wanataka kujua lini watafanyiwa jitihada ya umeme ikiwa ni moja ya jukumu la wizara yake kuwapelekea maendeleo wananchi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kuongezea jibu la Naibu Waziri na kumfahamisha zaidi swahibu yangu Mhe. Jaku, kwamba kiutaratibu kama hukufuata sheria vifaa ulivyovitumia vinataifishwa na Shirika. Kwa bahati nzuri na kwa upende wa Serikali kwa wananchi wake vifaa vya watu wa Jambiani Mfumbwe havikutaifishwa, wanatakiwa wende wakaelekezwe kupata nguzo sahihi, wakenda kesho, basi vifaa vyao vipo, waya upo na kila kitu kipo, nguzo tu tutakubaliana iweje na watawekewa umeme, hatukuwadharau.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahasante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa swali la nyongeza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kuna wananchi wamenunua nguzo zao lakini Shirika wamezikataa.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kukataliwa.

(b) Hivi karibuni mmeitisha tenda za watu wenyeuwezo wa kuweza waje pale kuweza kukubali na shirika kwa kuleta nguzo. Ni lini kazi hiyo itaweza kufanyika ili wananchi waondokane na usumbufu wa kutafuta nguzo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe hili swali la mwanzo linahusiana na hili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ndio, swali la nguzo limo humo Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa sababu niliona amekwisha kulijibu Mhe. Waziri, lakini haya kwa faida ya wote tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme iko tayari kushirikiana na mwananchi yoyote ambaye kafuata utaratibu wa kisheria. Kama kuna mwananchi kanunua nguzo ambazo zenye kiwango basi sisi kwa hilo hatuna tatizo tutashirikiana naye na tutahakikisha tutampelekea umeme katika sehemu yake inayohusika.
Kuhusu kazi ambayo inataka ifanywe katika sehemu hiyo. Mheshimiwa nakuomba uje ofini kwangu tutashirikiana, tutakwenda kuangalia vifaa vyake ikisha tutampangia kazi kwa utaratibu unaofaa, hatuna pingamizi na hilo.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Mwenyekiti, huduma ya umeme ni muhimu kwa matumizi ya binadamu kwa nini wizara yako inawakatia umeme wananchi wa hali ya chini kwa kiwango cha shilingi 30,000 ikaacha kukata kwenye hoteli na mashirika ambao wanadaiwa si chini ya milioni tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme haibagui mteja gani wa kumkatia umeme, inakata umeme kwa taratibu za kisheria yule mtu yeyote ambaye halipi kodi hiyo ya umeme, basi sisi tunamkatia ikiwa ni mwenye hoteli, ikiwa ni mtu wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, cha msingi ni kwamba awe analipia deni lake la matumizi ya umeme kwa kila mwezi unapofika basi afike pale Shirika la Umeme alipie malipo yake. Lakini mtu yeyote ambaye hatolipa umeme ikiwa mwakilishi, akiwa waziri, ikiwa mwekezaji, ikiwa mwananchi wa chini basi tutamkatia umeme kwa taratibu za kisheria.

Nam. 100

Mnara wa Matumbini

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Minara na maboya ni vifaa muhimu kwa huduma za usafiri wa baharini hususan kwa nchi za visiwa kama Zanzibar. Meli, maboti, majahazi na vyombo vyengine vya baharini vinaweza kusababisha ajali na hasara iwapo havifanyi kazi.

a) Ni kwa nini hadi leo hii mnara wa Matumbini umeshindwa kufanyiwa matengenezo.

b) Minara katika visiwa vyetu huchangia sana mapato, ni kwa nini mapato yanayopatikana kutokana na minara hiyo hayatumiki kufanyia minara hiyo matengenezo.

c) Mnara wa Matumbini uliwahi kutengenezwa na baadhi ya wananchi kupatiwa ajira kwa kazi ya ulinzi. Je, wananchi wale bado wanaendelea na kazi yao na wanalipwa mishahara.

d) Ni minara mingapi katika visiwa vyetu inafanyakazi na mingapi haifanyikazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna minara na maboya ambayo ni vifaa muhimu sana kwa usalama wa safari za baharini, kwa sababu hiyo wizara yangu kupitisha Shirika la Bandari imeweka mpango maalum wa uimarishaji wa alama hizo ili kuweza kuongoza vyombo katika bahari za Unguja na Pemba

a) Mhe. Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kua Shirika la Bandari limeufanyia matengenezo makubwa mnara wa Matumbini katika mwaka 2002 na hali ya jengo la mnara huo liko vizuri na linaridhisha. Tatizo kubwa la mnara huo hivi sasa ni taa yake ambayo inatumia nguvu za jua ambayo imeharibika, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imejipanga kuzibadilisha taa zote za minara na maboya na kuweka taa mpya zote zitakazotumia nguvu za jua ndani ya mwaka huu 2012, ambapo tayari taratibu za zabuni na ununuzi wa vifaa hivyo zimeshakamilika.

b) Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi kua minara katika visiwa vyetu huchangia mapato ya shirika, kutokana na mapato hayo ndio Shirika la Bandari huifanyia matengenezo minara yake kila inapohitajika. Kwa mara ya mwisho Shirika la Bandari limeufanyia matengenezo makubwa mnara wa Mwana wa mwana ulioko Tumbatu katika mwaka 2011.

c) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kua baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa mnara wa Matumbini wizara yangu kupitia Shirika la Bandari iliwaajiri wafanyakazi wawili kwa kazi za ulinzi ambapo wanaishi katika eneo la Matumbini. Wafanyakazi hao bado wanaendelea na kazi zao na wanalipwa stahiki zote kwa mujibu wa sheria.

d) Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Bandari lina jumla ya minara mikubwa 9 ambayo 8 ndio inayofanya kazi usiku na mchana na mmoja huo wa Matumbini kwa nyakati za usiku taa yake imeungua.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize maswali ya nyongeza yenye (a) na (b) kama ifuatavyo;

a) Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba katika jitihada za kuweka ulinzi eneo la Matumbini amewaajiri wananchi wawili na nikiri kwamba ni wananchi wa Jimbo la Kiwani kupitia Mwambe. Lakini kwa wananchi wale wako wengi na kwa kua wanaendelea na familia zao na wanaendelea kuzaa, wizara imeona kuna umuhimu wa kuwajengea shule katika kisiwa kile kwa kushirikiana na mwakilishi na mbunge wa Jimbo la Kiwani, na wizara itakua tayari kusaidia katika hatua za uezekaji wa jengo lile pamoja na huduma nyengine.
Je, ahadi ile ya wizara ya kuwajengea shule kwa kusaidiana na uongozi wa Jimbo la Kiwani imefikia wapi.

b) Mhe. Naibu Waziri hivyo kuuwachia mnara wa Matumbini kutokufanya kazi huku wavuvi na wasafiri wa baharini wakaendelea kupata usumbufu, si kuchangia kusababisha madhara ya baharini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala la kwamba wizara yetu ilitoa ahadi ya kujenga shule hatujaiona ahadi hiyo na kama ipo ahadi tutafanya mawasiliano na wenzetu ili waweze kutupatia suala hilo, lakini pia kama kuna kumbukumbu hiyo tunaamini kwamba watendaji wetu wataweza kutupatia hilo. Lakini nadhani suala la kujenga shule ni utaratibu ambao unaratibiwa na Wizara ya Elimu na mipango yao wanajua maeneo gani ambayo yanastahiki kujengwa shule, idadi gani ambayo inapaswa kujengwa na taratibu nyengine. Mhe. Mwenyekiti, imani yangu kama kuna ahadi ilioko katika Wizara ya Miundombini basi tutashirikiana na Wizara ya Elimu ili kujua taratibu na ikiwezekana kuratibu kuona jambo hilo litaweza kufanikiwa kwa kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Shirika la Bandari katika mwaka huu wa 2012 kabla ya kufika Disemba matengenezo ya minara yote na maboya yatakua yameshafanikiwa, kwani tumeeleza kwamba utaratibu wa zabuni na mkandarasi wa kufanya matengenezo hayo ameshapatikana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida mtu akiumwa na nyoka basi akiona unyasi tu hukimbia, na kwa kua boya iliopo Mkoani pale mara nyingi tangu zamani na hadi sasa haifanyi kazi, na kwa vile juzi MV. Maendeleo iliingia kwenye matope pale na kusababisha taharuki kubwa. Je, pamoja na mpango wako wa muda mrefu kufanya matengenezo ya hii minara na maboya je, ni hatua gani za dharura ambazo ofisi yako imechukua ili kufanya matengenezo ya dharura pale kwenye ile boya ya pale Mkoani.

b) Mhe. Mwenyekiti, kuendelea kuiacha boya hiyo kuwa haiwaki hadi leo hii si kuhatarisha maisha ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tumeeleza kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari tunamiliki minara 9 mikubwa na minara 8 midogo pamoja na maboya yaliomo katika maeneo ya bandari zetu ya Malindi pamoja na bandari ya Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wetu wa dharura ni kuhakisha kwamba tunaondoa mfumo uliopo, taa za minara zilizopo sasa hivi ni mfumo ule wa zamani wa taa zinazotumia gesi. Ni kwamba mapendekezo yetu na mipango ya shirika ni kuondoa mfumo ule wa taa za gesi na kuweka mfumo wa taa zinazotumia jua. Hatua hizo za dharura zinazochukuliwa sasa hivi ni imani yetu kwamba katika kipindi cha mwaka huu jambo hili litakua limekamilika kama tulivyoeleza kwamba tayari taratibu za zabuni zimeshafanikiwa na kampuni ambayo itafanya mabadiliko hayo tumeshaipata. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra jambo hili likamilike.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili linahusiana na hilo hilo suala la minara ni kwamba utaratibu uliopo ni kua minara ile tutakapoweza kuiondoa katika mfumo wa gesi kwa sababu vifaa vinavyotumia katika uwashaji wa gesi na zile huduma nyengine ni vifaa ambavyo vimepitwa na wakati hivyo inapotekea matatizo ili kuweza kupata kifaa cha kufanyia ukarabati inachukua muda kwa sababu katika soko ni vifaa ambavyo vimeshaondoka.

Mategemeo yetu kwamba mabadiliko haya ya kuingiza *system* ya *solar* yanaweza kukidhi hayo mahitaji na kutoa huduma zetu vizuri kwa wasafiri wa baharini.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba umuhimu wa maboya na minara kuwaka usiku tunajua, tuseme kwa bahati mbaya ikatoke meli ya kigeni ikafikwa na ajali kwa sababu ya kutokuwepo mnara unaowaka au maboya nani atawajibika kulipa ni serikali kwa uzembe wake au ni *captain* aliyekosea safari.

Mhe. Mwenyekiti, mnara huu wa Matumbini umeacha kuwaka kwa muda mrefu sana na tuliambiwa kua serikali inaita wataalamu kutoka Afrika ya Kusini kuja kufanya matengenezo, hii leo tunaambiwa kuna zabuni zimetolewa ile ahadi ya mwanzo ya wataalamu kutoka Afrika ya Kusini iliondoka tena na kwa sababu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, alama za minara inayoongoza vyombo vya usafiri baharini ni alama za kimataifa, na kila mnara una alama yake na uwakaji wake katika maeneo husika. Minara hii utaratibu wake ni kwamba inawaongoza ma-*captain* wanaondesha vyombo na

ikitokezea mnara ule ikiwa haufanyi kazi vizuri basi mamlaka inayohusika ndio inayobeba jukumu la kusababisha janga ambalo litatokezea.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulikuja na wataalamu kutoka Afrika ya Kusini kwa ajili ya kufanya matengenezo mnara wetu wa Matumbini, lakini tunachokieleza kwamba dunia inakwenda mbele hairudi nyuma mnara wa Matumbini ulikua ni miongoni mwa minara ambayo inatumia mfumo wa gesi, mfumo wa gesi sasa hivi vifaa vyake na vipuri vinaondoka katika soko.

Ndio maana serikali kwa kupitia Shrika la Bandari tukafanya maamuzi yakuondoa teknolojia ile na kuja na teknolojia mpya ya mfumo wa kutumia nguvu za jua (*solar*), ili sasa tukiweka hiyo *solar* ikiweza kufanya kazi pale ikiwa hatuna tatizo tunaamini kwamba upatikanaji wa vipuri na vifaa vitakavyoweza kurejesha huduma ile pale itakapotokezea matatizo itaweza kupatikana kwani ndivyo vifaa ambavyo viko katika soko kwa muda huu.

Nam. 113

Matengenezo Barabara ya Malindi hadi Mlandege

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imekua ikichukua hatua mbali mbali za kujenga barabara, ikiwemo barabara ya Malindi – Mlandege.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea matengenezo ya barabara hiyo kuchukua muda mrefu na kusababisha kufungwa kwa zaidi ya siku kumi bila ya kufanyika kazi ya aina yoyote ya ujenzi na kusababisha usumbufu kwa wananchi na magari yanayotumia barabara hiyo.

(b) Je, ni kwanini Wizara inaamua kuchimbua barabara kabla haijakua tayari kuifanyia matengenezo na kusababisha usumbufu na msongamano wa magari kwa wananchi wake.

(c) Kwa kua mambo mengi sasa yanafanyika kwa kuzingatia mipango. Je, kwanini Serikali isiwe na utaratibu kuanza ujenzi baada ya kukamilika mipango ili kuondosha usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 113 kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua ikichukua hatua mbali mbali za kujenga na kuzitunza barabara nchini ikiwemo barabara ya Malindi – Kinazini.

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Malindi – Kinazini yenye urefu wa kilomita 1 na upana usiopungu mita 8, ni miongoni mwa barabara zilizopangwa kufanyiwa matengenezo ya muda maalum (*Periodic Maintenance*) kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara. Ujenzi wa barabara hii ulianza mwezi Januari 2012 na ulipangwa kukamilika miezi miwili baadae.

(a) Mhe. Mwenyekiti, sababu zilizopelekea matengenezo ya barabra hiyo kuchukua muda mrefu na kusababisha kufungwa mara kwa mara ni kutokana na uchakavu wa zana za kufanyia kazi ambazo husababisha kuharibika mara kwa mara, kukatika kwa umeme katika sehemu yetu ya uzalishaji wa lami katika mtambo wetu uliko Kibele, mtambo ambao umeme umeunganishwa katika *grid* yetu ya taifa pamoja na kuadimika kwa huduma ya *diesel* hapa nchini kwetu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika jibu (a) ya kwamba ujenzi huu ulifanyika baada ya kukamilika kwa matayarisho yote ikiwemo suala la vifaa. Hivyo serikali inapoamua kutekeleza mradi ni dhahiri kwamba hujiandaa na kukamilisha vifaa na kinachofuata ni utekelezaji, hivyo sio sahihi kusema kwamba serikali haikua tayari kujiandaa na ilifanya maamuzi hayo pasi na kuzingatia muda na vifaa vinavyohitajika.

(c) Serikali imejiwekea taratibu kwa kila kazi inazozifanya zikiwemo kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara kukamilisha taratibu za utekelezaji wake kabla ya mradi huo kuanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili la barabara kuchimbuliwa na kuchelewa kutengenezwa limekua ni la muda mrefu na husababisha uharibu wa mali za watu na hata bidhaa. Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia mambo hayo zikiwemo bidhaa za nguo na vyakula hua vinaingia vumbi na kuharibika.

a) Je, serikali haitoi utaratibu wa kumwaga maji inapojenga barabara ili kuweza kupunguza lile vumbi.

b) Kwa kua wizara yako imekua ikisumbua watu kwani hivi juzi barabara hiyo ya Mchangani imechukua karibu siku 15 imekaa bila ya kuguswa tena bila ya sababu yoyote na mavumbi huingia majumbani mwa watu na kusababisha hata baadhi ya familia kuishi kwa shida na hata misikiti ilikua imejaa mavumbi, na wizara yako haijachukua hatua yoyote hata kuwapa pole wananchi wa Shehia ya Mchangani.

c) Mhe. Mwenyekiti, kuna sababu gani ya kuivunja barabara ile wakati barabara ile ilikua ni nzima na kuwatia hasara wananchi wanapotaka kwenda kupanda boti kuelekea Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mategemeo yangu ni kwamba Mhe. Mwakilishi angechukua nafasi hii kutupongeza Wizara ya Miundombinu chini ya utendaji kazi wa kikosi chetu cha UUB kwa kukamilisha mradi ule ambao utaleta maslahi na ufanisi wa shughuli za usafiri katika Mji wetu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kuonekana kwamba Mhe. Mwakilishi hafurahii uimarishaji wa miundombinu hasa ya barabara katika Mji wetu kama malengo ya serikali walivyoahidi na yanavyotekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi atambue kwamba utaratibu wa utengenezaji wa barabara ni miongoni mwa changamoto za mabadiliko ya miundombinu, tunapozungumzia suala la mabadiliko ya miundombinu bila shaka maendeleo yanakuja na faida na hasara. Suala analolizungumzia Mhe. Mwakilishi ni kuona kwamba maeneo ambayo tunatengeneza barabara yakiwa yanaleta vumbi tutengeneze utaratibu wa kumwaga maji kila siku kuzuia vumbi. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu ni mzuri, lakini Mhe. Mwenyekiti, tukijiuliza kwamba je, utaratibu huu utakua kwa maeneo ya Mjini au maeneo ya nchi nzima. Kwa sababu utengenezaji wa barabara unaendelea sehemu mbali mbali ikiwa Mjini pamoja na Vijijini, kwa hiyo tunapokuja na utaratibu huu kwa watu wa Mjini itakua tunatengeneza matabaka ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoeleza awali kwamba wakati tunatengeneza barabara hii tulikua tunatumia mitambo na mitambo ile ni vifaa ambavyo vimetengenzwa na kama tunavyotambua kwamba mtambo unawezekana muda wowote ukapata hitilafu ambazo hitilazu zile ndizo zilizopelekea kukaa siku 15 wakati mtambo huu unafanyiwa marekebisho tukashindwa kuendelea na kazi. Lakini pia kama tunavyokumbuka kipindi hicho ndicho kipindi ambacho tulikua na matatizo ya mafuta nchini mwetu. Baada ya kukamilisha changamoto hizo idara yetu ya UUB inaendelea na kazi, na kazi ile imekamilika. Mhe. Mwenyekiti, lakini bado barabara ile haijakamilika kinyume na matarajio yetu kwamba kuna maeneo ambayo yakuweka *parking*, tunamatarajio ya kufanya bajeti mpya ili kuweza kuyafidia pamoja na maeneo ya kupita watu wanaotembea kwa miguu.

Mhe. Mwenyekiti, sababu kubwa ya kuijenga barabara ile ni kuona kwamba kwa vile barabara ile ilikua imeshazidiwa kutokana na gari kubwa zenye uzito mkubwa zinazopita katika maeneo yale, barabara ilikua imeshadidimia na ndio maana ikinyesha mvua maji yalikua yanatuwama katika barabara. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, mpango wa serikali ni kuziimarisha barabara zote zinazoingia katika mji wa Zanzibar na tayari wenzetu wa *World Bank* wanatusaidia kufanya *study* na ripoti tumeshaipata umuhimu wa kuimarisha miundombinu hasa barabara zinazoingia Mjini zinaondosha usumbufu hasa wa usafiri kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kua hii barabara ya Mlandege/Malindi ni miongoni mwa barabara zinazotoa taswira ya nchi yetu. Na kwa kua uzoefu wa nchi nyengine unaonesha kwamba barabara muhimu kama zile hata nchi zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara, barabara muhimu kama zile hufanyiwa matengenezo kwa usiku mmoja tu, siku ya pili ikapatikana.

Je, ni sababu gani za msingi ambazo hupelekea sisi Wazanzibari kushindwa kuzifanyia ukarabati kwa kipindi kifupi na hatimae kupelekea Mabalozi kuwatia mavumbi katika kipindi kirefu. Je, kwa kufanya hivyo si kuidhalilisha serikali yetu hii ambayo wananchi pamoja na sisi wawakilishi wao tulioko huku viti vya nyuma inatuuma sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na dhana ya Mhe. Mwakilishi kwamba ipo haja ya kufanya matengenezo kwa muda mfupi kadri hali itakavyoweza kuruhusu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, changamoto yetu kubwa kwa baadhi ya nyakati inakua ni upatikanaji wa fedha, ukusanyaji wa vifaa lakini pia vitendea kazi vyetu kwa maana ya mitambo, pale ambapo mitambo yetu iko vizuri fedha zitapatikana mapema na ukusanyaji wa vifaa utafanyika mapema, basi imani yangu kwamba utengenezaji na ukarabati wa maeneo husika utafanyika kwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo mengi ambayo tunayafanyia ukarabati katika barabara zetu tusione eneo hili tu moja ambalo tunalilalamikia, ni kwamba kuna maeneo mengi ambayo katika kipindi hiki hiki wakati ujenzi huku unaendelea na maeneo mengine yalikua yakiendelea na harakati za kufanyia ukarabati, na ndio maana sasa hivi ukiona barabara zetu zote za Mji wa Unguja ni kama mgongo wa ngisi.

HOJA ZA SERIKALI

Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu ili kukamilisha shughuli zetu kama zilivyopangwa. Aidha, Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii ya kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kuwasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2011. Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria kwa namna ambavyo waliweza kuzijadili kanuni zetu hizi katika hatua ya awali na wakaweza kutoa mapendekezo mazuri ambayo yalituwezesha jana katika semina yetu kufikia mjadala mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu walioshiriki katika semina ile ya jana walipata nafasi nzuri ya kutupa maoni ambayo kwa kiasi kikubwa ndio yaliotuwezesha leo tuweze kuwasilisha hoja hii ya kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya kanuni. Naamini kitabu kile ambacho kila mmoja wetu amekipata kinatokana na maoni ambayo jana tuliyapata. Hivyo, naamini sana kwamba shughuli yetu ya leo itakua nyepesi mno kutokana na kwamba mengi ya yale tayari tumeshakubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe ni ukweli kwamba kanuni zetu zilifanyiwa marekebisho mwaka 2011 ili kukidhi haja ya marekebisho ya Katiba ya Zanzibar yaliyofanywa mwaka 2010. Ofisi yangu imeona ipo haja ya kuleta tena mapendekezo ya marekebisho ya kanuni zetu ili kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi zaidi, kama ilivyo kwa sheria mbali mbali kanuni huhitaji kufanyiwa marekebisho kila haja ya kufanya hivyo inavyojitokeza hasa pale ambapo tunagundua mapungufu wakati wa utekelezaji wa kanuni hizo.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe mambo makuu ya msingi yaliyopendekezwa katika kanuni hizi yanahusiana, kwanza ni kufanya utaratibu wa kusomwa na kupitishwa miswada yetu. Hivyo kanuni ya 82 inakusudia kurekebishwa ili kukidhi haja iliyopo sasa marekebisho ya kanuni hii yanadhamiria kubadilisha utaratibu uliopo sasa wa miswada kusomwa mara mbili, na badala yake kuwezesha miswada hiyo kusomwa kwa mara tatu. Ambapo mswada utasomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano mmoja na hautosomwa kwa mara ya pili, na pia hautajadiliwa katika Baraza hadi hapo katika mkutano unaofuata wa Baraza. Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu unakusudia kutoa fursa kwa Wajumbe wa Baraza kuipitia kwa umakini zaidi miswada hiyo na pia kupata muda wa kushauriana na wananchi ili kutafuta maoni ya wananchi ambao wanawawakilisha. Hata hivyo, utaratibu huu hautohusu miswada ya dharura.

Mhe. Mwenyekiti, pia marekebisho ya kanuni hiyo ya 82 yanakusudia kutoa fursa kwa kamati inaposhughulikia miswada uwezo wa kumualika mtu au taasisi yoyote kwa ajili ya kutoa maoni yake mbele ya kamati hiyo. Marekebisho ya kanuni hii yanakusudia kuweka utaratibu ulio wazi zaidi wa kamati kuwaalika watu au taasisi mbali mbali ili kutoa maoni yao yatakayosaidia kuingia kwa misaada katika hali iliyo bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe mapendekezo mengine ya Marakebisho ya Kanuni ni kanuni ya 90A yanayotoa fursa kwa Baraza kujadili mwelekeo wa Mpango wa Taifa ili kuwezesha Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupitia na kutoa maoni yao juu ya mwelekeo wa Mpango wa Taifa ambao utajumuisha tathmini ya hali ya uchumi kwa mwaka wa fedha unaoendelea, matarajio kwa mwaka wa fedha unaofuata, malengo katika ukusanyaji wa kodi kwa mwaka wa fedha unaofuata pamoja na taarifa nyengine zinazolingana na hizo.

Pamoja na mambo hayo ya jumla, pia kuna marekebisho yanayohusu makosa ya lugha, makosa ya uchapishaji na marekebisho mengine mbali mbali yaliyojitokeza katika kanuni zetu. Aidha, tunapendekeza kutekebishwa na kuwekwa ukomo kwa maswali ya nyongeza pamoja na kufanya marekebisho katika kanuni zinazohusiana na muundo wa Tume ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Vile vile kufanya marekebisho katika muundo wa Kamati Teule zinazoundwa na Baraza letu tukufu.

Pia Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe tunafanya marekebisho ili kumuwezesha kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza apate nafasi zaidi ya kutekeleza majukumu yake katika Baraza. Vile vile tunaweka utaratibu mzuri wa upigaji kura ndani ya Baraza ili kuondoa malalamiko pale ambapo yanaweza yakajitokeza.

Hata hivyo, tunaweka utaatibu wa namna ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kamati mbali mbali za Baraza lako tukufu yanayotolewa katika ripoti za kamati ya mwaka uliotangulia ili ziweze kuwasilishwa hapa Barazani na kutoa nafasi kwa Wajumbe kuona utekelezaji uliofanyika katika serikali.
Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe walipata fursa nzuri jana ya kuijadili kwa kina haya marekebisho ya mapendekezo ya kanuni zetu. Na kwa kuwa ni kutokana na majadiliano yale ndio maana tukaleta hiki kitabu ambacho kila mmoja amepewa cha marekebisho hayo. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, naona kwa kuwa kazi kubwa ilifanyika jana leo ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hili waipitie na kuijadili lakini baadae waipitishe ili sasa tuwe na kanuni zetu zilizo bora zaidi zitakazotuelekeza kufanya shughuli zetu kwa ufanisi na uzuri zaidi.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ahsante sana.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana katika Baraza lako hili tukufu asubuhi ya leo kujadili mambo yetu. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru wewe ambaye umenipatia fursa hii niweze kusoma hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzíbar Januari, 2012.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana tena asubuhi hii ya leo katika ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, katika kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Rasimu muhimu ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Vile vile nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Raisi kwa kutuwasilishia Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la Mwaka 2012 kwa kuhakikisha kuwa marekebisho haya ya Kanuni ni mazuri na pia yanaendana na wakati pamoja na mahitaji ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wake kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia muda wote tulipokua tunajadili na kuchambua Rasimu hii muhimu ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano makubwa wanayonipa pamoja na michango yao madhubuti waliyoitoa ili kuleta tija zaidi katika rasimu hii. Mhe. Mwenyekiti, ili kuzipa nguvu shukurani zangu hizo napenda kuwatambua Wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
8.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu

9. Ndg. Abubakar Mahmuod Iddi - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, malengo ya Rasimu ya Mapendekezo ya Mrekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, ni kuifanya kanuni hii iweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi na pia iendane na Katiba ya Zanzibar ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2010.

Baada ya kazi ya kuupitia mswada huo, Kamati yetu imependekeza na kuyakubali marekebisho kadhaa yenye lengo la kusaidia kuboresha mswada huo yakiwemo ya kilugha. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niainishe baadhi ya marekebisho ambayo kamati iliyapendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeyakubali mapendekezo ya Kanuni ya 40 ambayo inapendekeza kurekebishwa kwa kuandika upya Kanuni ya 40(2) kwa madhumuni ya kuweka wazi ukomo wa maswali ya nyongeza kwa kila swali la msingi ambapo inapendekezwa kuwa maswali matatu tu ya nyongeza ndiyo yaulizwe.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu wa ukomo wa maswali matatu ya nyongeza kwa kila swali la msingi ndio unaotumika kwa sasa ingawa umekuwa ukitekelezwa kwa utamaduni tu bila ya kuwa na Kanuni inayoeleza wazi kuhusu ukomo huo.

Aidha, kamati imeyaridhia marekebisho ya Kanuni ya 40(3) inayokusudia kufafanua zaidi maswali ya nyongeza ambayo Mjumbe mmoja anaweza kuuliza katika kila swali la msingi na inapendekezwa kuwa ni swali moja tu linaloweza kuwekwa katika sehemu zisizozidi mbili. Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 43 inakusudiwa kurekebishwa ili kumruhusu Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza kwani Kanuni iliyopo sasa inamruhusu Waziri pekee kutoa kauli juu ya jambo ambalo Ssrikali inawajibika. Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa kiongozi kama ilivyokuwa hapo awali ambaye ni Makamo wa Pili wa Rais hivyo kanuni hiyo ilikuwa haitoi fursa kwa kiongozi huyo kutoa kauli ya serikali kwa mujibu wa Kanuni hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia imependekeza kuandikwa kwa kanuni mpya itakayojulikana kama Kanuni ya 150 ambayo inaelezea jinsi utaratibu wa mjumbe kupeperusha bendera ya Baraza. Pia kamati imependekeza kuandikwa kwa kifungu kipya cha 151 ambacho kitaelezea utaratibu baada ya kifo cha mjumbe jinsi gani Baraza litasitisha shughuli zake kwa siku hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi huu ndio mukhtasari wa Kamati kuhusiana na Rasimu ya Mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na marekebisho mengine yameainishwa katika warka wa marekebisho uliogaiwa. Nawaomba wajumbe wote wa Baraza hili nao waichangie vizuri Rasim hii kwa madhumuni ya kuiimarisha na kuleta tija zaidi katika rasimu hii lakini hatimae kuikubali na kuipitisha bila ya pingamizi yoyote.

Baada ya kutamka hayo Mhe. mwenyekiti, natamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naunga mkono Rasimu hii ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa asilimia zote mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya Mhe. Waziri kwisha kuwasilisha hoja na Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kutoa maelekezo ya kamati, jana kwa bahati nzuri tulifanikiwa kufanya semina juu ya hoja yetu hii ambayo leo tunataka tuijadili hapa, na kwa namna fulani nahisi kwamba tumefikia pahala pazuri. Sasa niwaombeni Waheshimiwa Wajumbe kama bado tunahisi tuendelee na kuchangia zaidi katika hilo na tuendelee. *Inshaallah*.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuweza kuchangia kanuni iliyofanyiwa marekebisho. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na kamati nao kwa kukiona kitu hichi ambacho kitaweza kutusaidia katika kutuongoza kwenye Baraza hili.

Lakini vile vile katika haya marekebisho mimi niseme kitu kidogo tu sina kubwa, ugomvi wangu uko padogo tu Mhe. Mwenyekiti, hii kitu neon ‘aya’. Hiki ndio kitu kinachonipigisha kelele basi, mimi sina tatizo nimesimama hapa kusema kwamba hili neon ‘aya’ jamani hebu tujaribuni kuliondoa, tusipende kulitumia sana katika Marekebisho ya Kanuni ya 19 ukurasa wa pili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ukaidi wangu uko hapo tu basi, kwa sababu aya ni kitu ambacho tukikitafsiri kwa upana ni jambo kubwa sana. Aya kwenye Qurani ni jambo lililokamilika na ni kweli Qurani tukufu ya

Mwenyezi Mungu inakuwa inakamilika lakini sisi kila siku hapa kwetu tunafanya marekebisho kwa sababu hiki kitu hakikamiliki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwa kuwa wananchi wangu wa Jimbo la Kitope ni wasomi sana wa Qur-ani tena sana na ndio maana wananambia hili neno nisikubaliane nalo, kitu 'aya' tu Mhe. Waziri nakuomba sana tusipende kuitumia katika karatasi, katiak vitu ambavyo havikamiliki na ndio maana kila siku tunafanya marekebisho, lakini aya huwezi kuifanyia marekebisho. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alione suala hili kuwa aya aiondoe kabisa.

Kwa hvyo machache nakubaliana na Mheshimiwa kwa asilimia mia moja na ndio mana nikasimama hapa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuletea hoja hii ya marekebisho ya kanuni ambayo ndio nyezo kamili ya matumizi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, bila ya kuwepo kwa kanuni ambazo zinasaidia utekelezaji wa sheria basi Baraza hili litakuwa halina nguvu za utekelezaji. Kwa msingi huo Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuona haja ya kurekebisha kanuni hizi ili ziende na wakati.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke kwamba zamani kulikuwa na Serikali na kuna Kambi ya Upinzani. Kutokana na marekebisho ya katiba sasa hatuna Kambi ya Upinzani na kwa hivyo tuna mnadhimu wa serikali na wanadhimu wa vyama. Nadhani haikai vizuri katika hali tulinayo sasa kuwa na wanadhimu wa vyama, kwa sababu mawaziri wote wanawajibika kwa pamoja bila ya kuangalia chama na Wawakilishi kwa maana ya *backbenchers* wanawajibika kwa pamoja bila ya kuangalia chama. Kwa hivyo, tungezingatia kuwepo kwa mnadhimu wa *backbenchers* ambaye na yeye angesaidiana na wale wanadhimu wa vyama kwa ajili ya kuweka mambo sawa pale inapotokezea hoja za pande zote. Kwa hivyo, nadhani tuzingatie katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na utata wa fedha lakini nimuombe afanye bidii kwamba kanuni hizi zipatikane haraka sana kabla ya Kikao cha Bajeti kijacho ili uchapishaji wa kanuni hizi uende sambamba na matakwa ya wajumbe ili tuzitumie kabla ya Kikao cha Bajeti kijacho ili tuweze kusaidia ufanisi wa Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo sasa na mimi naunga mkono hoja hii na Mhe. Waziri aangalie busara ya kuwepo na mnadhimu wa *backbenchers* ili washauriane na mnadhimu wa vyama vyote viwili kuweka mambo sawa. Mambo haya ya serikali ya umoja wa kitaifa yanahitaji *negotiation.* Tumeona kuna busara sana kwamba iwapo serikali imeshika hoja A na *backbenchers* wanashika hoja B kuhitaji mazungumzo, lakini wakiachiwa wanadhimu wa vyama na vyama vikishika nafasi ya kutushawishi nadhani si busara katika mfumo huu wa serikali.

Kwa hivyo, mimi niona kuna haja ya mashauriano baina ya serikali na *backbenchers* kupitia mnadhimu wao ama mnadhimu wa CCM na mnadhimu wa *CUF* wawe sehemu ya wanadhimu kwa pamoja katika kujenga hoja pale ambapo serikali inahitaji mashauriano baina ya jambo ambalo lingeleta mgogoro si jambo la kupelekwa kwenye chama. Nadhani kwa msingi huo sasa chama hakina nafasi ndani ya Baraza hili kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Haji Faki Shaali): Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza naunga mkono hoja hii sina matatizo nayo hata kidogo kwa sababu nimeshiriki katika semina na kimsingi ninakubaliana nayo, lakini nina ombi.

Ombi la kwanza, kama itawezekana au kama hakutakuwa na ugumu katika utekelezaji kuna toleo moja la kanuni kwa bahati nzuri lilichapishwa pamoja na Haki, Kinga na Fursa za Wawakilishi, kwa hivyo lilikuwa linaturahisishia *reference* kuwa kuwa una vitabu viwili. Kwa hivyo, naomba toleo litakalochapishwa kama itawezekana basi turejee ule utaratibu wa nyuma tuwe na kitabu kimoja ambacho sehemu moja kuna kanuni na sehemu nyengine kuna haki, kinga, na fursa za Mwakilishi kama toleo moja ambalo Baraza walituchapishia. Hilo lilikuwa ndio ombi langu la kwanza.

Ombi la pili, hili ni lile alilolizungumza Mhe. Hija Hassan Hija mwakilishi mwenzangu kwamba kusiwe na wanadhimu wa vyama lakini kuwe na mnadhimu wa *backbencher* na mnadhimu wa serikali. Mimi nadhani wazo zuri, lakini mimi nafikiri kwanza tusilifanyie haraka, kwanza naomba tupitishe kanuni zetu kama zilivyo. Kwa sababu gani nikasema tusifanye haraka? Kwa sababu tuna *caucus* bado pamoja na kwamba tuna mfumo

huu, lakini wawakilishi wa kila chama wanakutana, wanazungumza na kuweka misimamo juu ya mambo mbali mbali.

Sasa tukiwa wanadhimu moja kwa moja tutakuwa tunauwa na *caucus*, sasa nafikiri tutakapouwa *caucus* itakuwa si kitu kizuri. Sasa mimi nasema kwamba wazo lake mimi sioni kwamba lina ubaya lakini nadhani kwanza hebu tungevuta muda kidogo tukenda na utaratibu huu huu mpaka baadae tukafanya utafiti vizuri tukaona faida na hasara zake kwa sababu ya ile hofu niliyoizungumza kwamba tukiwa wanadhimu ina maana na *caucus* tutaziuwa. Sasa je, tujiulize *caucus* hazisaidii?

Mimi Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa fikra zangu ni hizo na naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Majadiliano yanaendelea, sasa basi ikiwa tumeridhika na hili basi tumuombe Mhe. Waziri aje atoe chochote kama anacho. Vile vile wale wajumbe ambao wako nje tunawaomba waingie ndani ili tuweze kumaliza kazi inayotukabili mbele.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kwa mara nyengine nawashukuru kwa kunipa fursa hii ya kusimama tena mbele ya Baraza lako hili tukufu. Aidha niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza hili kwa namna ambavyo walivyoonesha nia njema kuzipitisha kanuni zetu hizi na ziwe kanuni rasmi na iwe ndio dira yetu ya utekelezaji wa majukumu yetu.

Hili Mhe. Mwenyekiti, lazima niwashukuru sana Wajumbe. Kwa sababu hii ni hatua nzuri sana ambayo itazidi kujenga Baraza letu vizuri. Lakini pia naomba Mhe. Mwenyekiti, uniruhusu niwatambue Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia hoja hii.

1. Mhe. Panya Ali Abdalla- Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hija Hassan Hija
4. Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Haji Faki Shaali)

Mhe. Mwenyekiti, hawa nao tuwashukuru sana kwa maoni yao. Mhe. Mwenyekiti, mimi niishukuru kamati kama nilivyosema mwanzo kwamba tokea awali ilishirikiana na sisi na watendaji wa Baraza la Wawakilishi katika kurekebisha vizuri sana kanuni zetu hizi ili kupata kanuni zenye sifa na zilizo bora kwa ajili ya utekelezaji shughuli zetu. Kwa hivyo, naishukuru sana kamati kwa kazi hiyo nzuri ambayo wametusaidia.

Lakini pia niwashukuru wajumbe hawa ambao wametoa michango yao hivi sasa, nia ilikuwa ni kuboresha zaidi na kuweka taswira nzuri zaidi ya kanuni zetu. Ukweli kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija hapa kwamba upo umuhimu wa kuwa na uwezekano wa kuwana na mnadhimu wa *backbencher*. Nataka niunge mkono sana maneno ya Mhe. Haji Faki Shaali, kwamba bado katika utaratibu wetu huu basi vyama vyetu vina nafasi Fulani katika utekelezaji wa shughuli zetu. Kwa hivyo ni vizuri tuchukue nafasi ya kulifikiria jambo hili zaidi, tushauriane zaidi, ili tupate uamuzi ulio sahihi zaidi.

Hata hivyo, bado serikali upo umuhimu wa kushauriana na wanadhimu hawa waliopo sasa wa vyama katika kufanya mambo mengi, na mimi nimeona mfano mzuri sana juzi ambapo tulishauriana na wenzetu katika mambo mbali mbali tukafikia muwafaka mzuri wa kuendesha shughuli zetu za Baraza. Kwa hivyo nataka niwaahidi tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba hio ndio *spirit* yetu ya serikali na kwa sasa ushauri huo tunaupokea na tutaufanyia kazi ili twende vizuri katika kufikia maamuzi yetu.

Mwisho niombe kutoa hoja ili sasa Baraza lako rukufu hili lipitishe rasmi kanuni hizi na ziwe kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi. Ahsante sana Mhe. mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tukiangalia ndani tuna uhaba kidodo wa wajumbe ambao wako nje kwa shughuli mbali mbali, lakini kwa mujibu wa katiba kifungu cha 83(1) naomba ninukuu:

“Isispokuwa kama imeelezwa vyenginevyo katika katiba hii suala lolote la uamuzi katika Baraza la Wawakilishi litaamuliwa kutokana na idadi kubwa ya Wajumbe waliohudhuria kwenye kikao na kupiga kura”.

Lakini kanuni ibara ya 71(1) inasema:

“Kiwango cha vikao vyote vya Baraza kitakuwa ni nusu ya Wajumbe wote”.

Sasa basi, kwa kutumia kifungu cha katiba cha 83(1) nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe tuamue kuhusu hoja ambayo iko mbele yetu. Naomba tuamue hoja, wale ambao wanakubaliana na hoja wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuchukua fursa hii kuwatangazia rasmi kwamba hoja ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar imepitishwa rasmi. *(Makofi)*

RIPOTI ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari

Mhe. Assaa Othman Hamad (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ni kushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuja kusoma Muhtasari wa Taarifa ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya baadhi ya wizara Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii muhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na Mwenye kurehemu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kujadili mambo mbali mbali yenye maslahi mema na ustawi mzuri kwa nchi yetu na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kwa niaba ya Kamati yangu kuwapa pole Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Bububu kwa kuondokewa na kipenzi chetu Marehemu Salum Amour Mtondoo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwa kuchaguliwa kwake kushika wadhifa wa kuliwakilisha Jimbo la Uzini. Tunaamini kuchaguliwa kwake kumetokana na ukomavu wake kisiasa pamoja na uwezo mkubwa wa kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Uzini. Tunamuomba Mola ampe nguvu, uwezo na afya njema ili aweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu haya makubwa ya Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu mukhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104(h) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi - Zanzibar, Toleo la mwaka 2011. Majukumu na kazi za Kamati hii yameainishwa katika kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambapo, pamoja na mambo mengine, Kamati ina majukumu ya msingi yafuatayo:

(a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.

(d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

(f) Kushughulikia miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

(g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

(h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imepewa jukumu la kusimamia Wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ifuatavyo:

i. Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.
ii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi.
iii. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imekua ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa kazi nzuri waliyoifanya na kupelekea kumaliza misimu mitatu ya Kamati kwa umakini na umahiri mkubwa. Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Mohammed Said Mohammed - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Assaa Othman Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
5. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Abdi Mosi Kombo - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
9. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
10. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha wa 2011/2012, Kamati ilifanya kazi kwa wiki sita kama ifuatavyo:

Kwanza kabisa, Kamati ilianza kutekeleza shughuli zake Unguja kuanzia tarehe 19/09/2011 hadi tarehe 30/09/2011.

Katika mzunguko wa pili, Kamati iliendelea na shughuli zake Pemba, kuanzia Tarehe 12/12/2011 hadi tarehe 23/12/2011.
Aidha, Kamati iliendelea na utekelezaji wa kazi zake Unguja kwa awamu ya pili kuanzia tarehe 20/02/2012 hadi tarehe 02/03/2012.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu kimsingi imeridhika na utendaji wa Wizara zote tatu inayozisimamia. Kamati inawapongeza kwa dhati watendaji wa Wizara zote kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao, licha ya mazingira magumu na bajeti finyu wanayokabiliana nayo. Baada ya shukurani za jumla za Kamati kwa Wizara zote sasa nichambue utekelezaji wa Wizara moja baada ya moja kama ifuatavyo:

Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 18 cha Katiba ya Zanzibar kinaeleza kua kila Mzanzibari anayo haki ya kupewa taarifa kuhusu matukio mbali mbali ya ndani na nje ya nchi au kutoa habari na dhana alizonazo, kupitia chombo chochote cha habari na bila ya mawasiliano yake kuingiliwa kati. Kwa mantiki hiyo basi, sekta ya habari ni pana mno inayohitaji uangalifu mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuweza kuwapatia kwa mara nyengine tena wananchi wa Pemba huduma ya televisheni ambayo ilikosekana si chini ya miaka mitatu. Hizi ni hatua za makusudi ambazo hazina budi kupongezwa kwani kama tunavyojua kua Zanzibar ni visiwa viwili na hivyo huduma zote zinazotelewa hutolewa kwa uwiano baina ya pande mbili hizi. Ni matumaini yetu kua wananchi wa Pemba wataitumia vyema fursa hii na kuweza kufaidika na vipindi vinavyorushwa na *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imesikitishwa sana na hali mbaya ya uchafu wa mji wetu wa Zanzibar hususan maeneo ya mjini ambapo mara kwa mara hujitokeza mrundikano wa taka na kupelekea harufu mbaya sana. Hali hii inaitia dosari nchi yetu kwa wageni wanaotutembelea kwani mbali ya kuchukiza harufu hiyo lakini pia inahatarisha afya zao. Kwa mantiki hiyo basi, upo uwezekano mkubwa wa kupungua kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini iwapo jitihada za makusudi za kurekebisha hali hiyo hazitochukuliwa.
Tunawaomba Wazanzibari kujenga utamaduni wa usafi ili kuyafanya mazingira yetu kua ya kuvutia. Aidha, tunatoa wito maalum kwa Baraza la Manispaa kulivalia njuga suala hili ili Zanzibar iweze kufaidika vyema na Sekta ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, miundombinu ni nyenzo muhimu katika safari ya kuelekea kwenye maendeleo. Kamati imeshangazwa na kitendo cha kutotengenezwa njia iliyopita katika msitu wa Ngezi kwa kutiwa angalau fusi kwa madai ya kwamba wanyama watapotea. Kwa kweli uamuzi huo unapaswa kufikiriwa mara mbili ili kujulikana faida na hasara za kutumia njia katika hali iliyoshuhudiwa na Kamati yetu. Ingawa hoteli za kitalii zinazowajibika kutumia njia hiyo zimo katika mashaka makubwa lakini pia wananchi wanaotumia njia hiyo hutaabika sana hususan wanapopata wagonjwa wanaohitaji kuwapeleka hospitali haraka.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu inakabiliwa na changamoto nyingi katika safari yake ya kuelekea kwenye maendeleo endelevu. Miongoni mwa changamoto hizo ni kua na urasimu mkubwa kwa wawekezaji wa ndani na nje pale wanapojitokeza kutaka kuwekeza kwenye sekta mbali mbali. Tunaishauri Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi *(ZIPA)* kujipanga upya ili kuiondoa kasoro hiyo kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kua michezo huleta furaha na afya kwa wanamichezo, Kamati yetu ina majonzi makubwa kwa hali ya hivi sasa ya michezo ya Zanzibar hasa kwenye medani za Kimataifa. Tunaishauri Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuyatafutia ufumbuzi mambo yanayokwamisha juhudi za wanamichezo wa Zanzibar yakiwemo kukosekana ushirikiano (Kimataifa) baina ya taasisi na vyama vya michezo vya Tanzania Bara na hapa Zanzibar, kukosekana ruzuku kwa vyama vya michezo kwa wakati inapohitajika, uvamizi wa viwanaja vya michezo na kuwakosesha vijana nafasi za mazoezi, kukosekana utaratibu mzuri wa Wizara kuendeleza sekta ya michezo kwa kutoelekeza vyema matumizi ya rasilimali watu, ambapo mafunzo ya michezo hupewa watendaji wasiohusika na michezo, kutopatikana kwa vivutio vya kimichezo na kukosekana kwa jengo maalum la afisi za wanamichezo kwa vyama vyote vilivyosajiliwa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kua Shirika la Utalii la Zanzibar liko mahututi kutokana na kukosa mwendelezo kwa muda mrefu sasa. Aidha, baadhi ya rasilimali zake zimeharibika vibaya baada ya kukosa matunzo yanayostahiki. Kamati inashauri kwamba Shirika lirejeshewe vitega uchumi vyake ili kuweza kufufuliwa upya kwa maendeleo ya Sekta ya Utalii nchini. Hivyo, hoteli za Serikali za Wete na Mkoani zirejeshwe mikononi mwa Shirika ili kuzifanyia marekebisho au kuzikodisha kwa mtu au taasisi nyengine itakayotupatia faida kubwa. Aidha, Kamati imearifiwa kwamba hoteli ya Serikali ya Chake Chake imekodishwa kwa kampuni ya *National Marketing* na baadae kampuni hiyo kuikodisha benki ya *Barclays.* Kwa mantiki hiyo basi, ni vyema Wizara ikaipitia upya mikataba ya ukodishwaji kwa umakini ili kufahamu uhalali wa mkodishwaji *(National Marketing)* kuikodisha tena hoteli hiyo. Kadhalika nyumba za wageni za Bwejuu na Makunduchi zirejeshwe kwa Shirika lenyewe kwa ajili ya kuzipangia matumizi mbadala.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mhe. Mwenyekiti, harakati za ufugaji na uvuvi ni ajira ya asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar kwa vile nchi yetu imezungukwa na bahari. Ni ukweli usiopingika kua kuimarika kwa sekta hizi ni kuimarika kwa jamii

nzima kwa ujumla. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuyachunguza kwa kina na hatimae kuyatafutia ufumbuzi matatizo ya Kamati za Uvuvi za Unguja na Pemba, kwani tumebaini kua migogoro na kutoelewana baina ya viongozi na wavuvi kunawasababishia wavuvi wetu kutopata mafanikio kama Kamati ilivyo yashuhudia hayo kwa wavuvi wa Matemwe na Chwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Kamati yetu imepokea taarifa kwamba wafugaji wetu wazalendo wanaoinukia wamepata pigo kubwa la kushuka soko la kuku kutokana na kuingizwa kuku kutoka nje ya nchi. Kwa kweli hali za wafugaji wetu ambao Kamati imewatembelea ni mbaya mno kiasi cha kuvunjika moyo na kazi wanayoifanya. Wananchi wengi hukimbilia kuku wanaotoka nje ya nchi kutokana na kwamba, kuku wanaoingizwa huwa ni rahisi ukilinganisha na wanaozalishwa nchini kutokana na gharama za uzalishaji baina ya nchi masikini na tajiri. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kuangalia upya sera ya biashara huria kwani bila ya kuwatupia jicho la huruma na msaada wa uhakika, wafugaji wetu wataendelea kula hasara.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uvuvi endelevu ni changamoto kubwa kwa Serikali yetu, kwani wengi kati ya wavuvi wetu wanavua katika njia za asili ambazo hazitoi tija kubwa. Pamoja na uanzishwaji wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu ambayo makao makuu yake yako Fumba, Kamati inashauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuifanyia uchunguzi wa kitaalamu Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla ya kuletwa mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuridhiwa. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi iitazame mikataba na makubaliano yote yanayofikiwa kwa mtazamo wa mbele zaidi ili kuiepusha Zanzibar na maafa yanayoweza kuepukika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanzisha miradi mbali mbali ya ufugaji na uvuvi kwa wananchi wa mijini na vijijini. Kamati imejionea yenyewe jinsi wananchi wanavyotaabika kufuga ng'ombe wa maziwa ambao hawatoi hata robo ya kile kilichotarajiwa. La kustaajabisha zaidi ni kwamba ng'ombe hao wamenunuliwa kutoka nje ya Zanzibar kwa madai kwamba ni mbegu bora na inayotoa maziwa mengi. Matokeo yake ni vifo vya ng'ombe hao kwa wingi na kutokubali kukamwa maziwa na kuhatarisha maisha ya wafugaji. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri Wizara kuunda timu ya wataalamu itakayokua ni dira ya kuelekeza miradi bora yenye maslahi kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Pemba kwa kutekeleza kwa vitendo ahadi zao na maagizo ya Kamati yetu katika msimu uliopita. Tunatoa wito kwa Wizara nyengine kuiga mfano huu ili kujenga jamii endelevu.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu kua Wizara hii imebeba jukumu zito la kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuwajengea mustakbali mwema wa maisha yao ya baadae. Kwa mantiki hiyo basi, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuwapatia fedha zote zinazopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kwa wakati kwani wakati Kamati ilipotembelea Wizara hii imebaini upungufu mkubwa wa fedha za kibajeti na hivyo kuifanya Wizara kutekeleza majukumu yake katika hali ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imepata fursa ya kuvitembelea vikundi mbali mbali vya Ushirika pamoja na *SACCOS* na kushuhudia jinsi wananchi wanyonge wanavyojituma katika harakati za kujikomboa kutokana na janga la umasikini. Aidha, juhudi zao hizo zinaongezwa nguvu na Wizara kwa kuwapatia mafunzo na mikopo kwa kadri hali inavyoruhusu. Zaidi ya yote hayo, Kamati inaishauri Wizara kuwapa mafunzo wanavikundi hao kabla ya kuwapatia mikopo pamoja na kufanya ziara za mara kwa mara ili kujua maendeleo na changamoto za vikundi vyao.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la utoaji na ufuatiliaji wa mikopo nchini, Kamati inaishauri Wizara kua na kitengo imara cha kuelimisha watendaji wa Serikali na wananchi wengine ili waelewe jinsi ya kupata mikopo na njia sahihi za matumizi ya mikopo hiyo kwa nia ya kuwawezesha kulipa mikopo hiyo kwa wakati na kuwapa fursa wananchi wengine kupata mikopo. Aidha, Kamati inashauri kutolewa mafunzo maalumu kwa wanavikundi wadogo wadogo ya kumalizia vizuri bidhaa wanazozalisha ili waweze kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inakabiliwa na changamoto kubwa ya kuondoa tatizo la upungufu wa ajira nchini. Vile vile ujuzi mdogo pamoja na kukosekana kwa utamaduni wa ujasiriamali miongoni mwa vijana ni hali inayoathiri uwezo wao wa kuajirika kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kutafuta namna ya kuiimarisha sekta binafsi na sekta isiyo rasmi ili ziweze kuzalisha nafasi zaidi za ajira kwa vijana waliokosa sifa za kuajiriwa katika sekta rasmi. Aidha, Wizara iwashughulikie vijana wenye sifa

zinazohitajika kwa ajira zilizo rasmi, ili kupunguza wimbi la wahitimu wa vyuo wasio na ajira, jambo ambalo litapelekea vijana hao kukosa imani na Serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, Kamati inatoa shukurani za dhati kwako wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu na usikivu wenu mzuri. Tunamuomba Mola mtukufu awape nguvu na uwezo wa kutekeleza vyema majukumu yenu ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati yangu na wananchi wa Jimbo langu la Wete naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema yake ya uhai na uzima sisi waja wake tukaweza kukutana hapa tukiendelea na kazi ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Pili, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kua mchangiaji wa mwanzo katika mjadala huu wa ripoti za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi tukianza na kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu hasa naomba nieleze masikitiko yangu kwa Afisi ya Baraza kwamba tunajadili kitu muhimu sana hapa, hichi tunachokifanya sasa ni moja katika kazi za msingi za Baraza ambazo zimetajwa ndani ya katiba. Ibara ya 88 inataja kazi za Baraza la Wawakilishi na katika ibara hizo kifungu 88 (d) kinazungumzia "kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya serikali katika njia ile ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa."

Shughuli hii hua tunaifanya kwa kamati kutembelea sekta mbali mbali ambazo ziko chini ya wizara tofauti na baadae kutayarisha ripoti ambayo kila mwaka hua inawasilishwa mara hii moja katika Baraza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hichi ndio kipindi chetu cha Baraza hili kwa niaba ya wananchi kuisimamia serikali kupitia ripoti za kamati. Lakini sijui katika kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi ikiwa ripoti za kamati kwenye kitabu kikubwa kama hichi tunagaiwa hapa asubuhi unapoingia halafu tunategemewa tuje tuijadili hapa kwa muhtasari ambao Mwenyekiti au Mwakilishi wa Kamati anauwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, hii haitutendei haki sisi na haiwatendei haki wananchi ambao tunawawakilisha hapa. Tuoneshe *seriousness* katika kazi zetu. Mwenzangu mmoja alikua akinitania hapa ananambia hili ulipaswa ukalisome nyumbani, nikamchokoza nikamwambia ingekua mmetupa kabla. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili tulitazame sana kwa sababu kama nilivyosema linatufanya tupimwe na wananchi wetu umakini wa shughuli zetu.

Lakini jengine vile vile Mhe. Mwenyekiti, niseme katika hilo hilo la umakini. Mhe. Mwenyekiti, tunapojadili hapa ripoti hizi tunategemea baadae kupewa ufafanuzi na Mawaziri wa Wizara zinazohusika katika kila kamati. Sasa ukiutazama upande wa serikali sasa hivi tunajadili ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, nashukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi yupo hapa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo yupo, lakini Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika simuoni hapa. Sasa najiuliza tutakapotoa hizi hoja zetu zinazohusu masuala ya wizara hii anazipokea nani anatujibu nani.

Mimi nadhani niiombe serikali katika hii ile sehemu ya uratibu inayohusika katika serikali isimamie vizuri shughuli hizi. Leo ilikua inajulikana kama kunajadiliwa ripoti za kamati hapa kwa hivyo wale mawaziri wanaohusika na kamati zinazowasilisha ripoti zake leo walipaswa wote tuwaone hapa. Kwa bahati mbaya kwa wizara hii Mhe. Mwenyekiti, hata Naibu Waziri haina kwa hivyo tunategemea waziri mwenyewe ndio awepo hapa asimamie masuala haya. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hili limejitokeza hapa mwanzo tunaomba kwa huko tunakokwenda kamati zinazofuata lisijitokeze, tuchukuliwe *serious* tunapokuja hapa kuwakilisha maoni ya wananchi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nimesema tumepewa hapa hapa asubuhi utaniwia radhi ikiwa katika kutoa michango yangu nitakua sina mtiririko mzuri. Kwa sababu kama nilivyosema napitia hapa hapa wakati mjumbe kwa niaba ya mwenyekiti wake anawasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na wizara ambayo imeanzwa mwanzo katika ripoti hii ambayo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambayo iko kuanzia ukurasa wa 121 hadi ukurasa wa 130. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme naomba nimpongeze sana Mhe. Said Ali Mbarouk kwa kuteuliwa kuiongoza wizara hii katika mabadiliko yaliyofanyika hivi karibuni. Niseme tuna matarajio makubwa sana kwake na tunaamini kwamba yale mafanikio ambayo yameonekana kipindi kifupi alipokabidhiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi sasa tutayaona katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, muda hauruhusu kusema kwa urefu katika masuala haya kwa hivyo naomba niende moja kwa moja katika yale ambayo nimeyakusudia kuyachangia.

La kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa jumla Sekta ya Habari ambayo iko katika wizara hii. Niwashukuru kamati wamekwenda kwa kina kabisa na niwapongeze sana kwa hili, katika kuangalia matatizo ambayo yako katika sekta hii.

Moja ambalo nataka nilizungumze Mhe. Mwenyekiti linahusu, hili ambalo wameliona Waheshimiwa Wajumbe wa kamati la kwamba tunatakiwa hivi sasa tujiandae kuingia katika mfumo wa *digital* kutoka katika mfumo wa *analogue*. Lakini kamati imebaini kwamba uwezo wetu katika sekta hii ya habari, katika maeneo yote redio na televisheni bado ni mdogo mno kitaalamu kuweza kulikabili suala hili. Mwisho mwaka huu tunaambiwa dunia imeweka ndio mwisho wa matumizi ya mfumo wa *analogue.*

Sasa sisi tumenunua mitambo hapa, lakini je, kwenye *man power* kwenye rasilimali watu tumejiandaa vipi.Nilikuwa naomba hii serikali ilipe uzito unaostahiki. Kwa sababu tunaweza tukafanya gharama kubwa sana ya kununua mitambo, lakini mitambo hiyo ikaharibika kwa muda mfupi kwa sababu haina wataalamu wa kuisimamia na kuihudumia. Au itabidi tufanye kazi kubwa sana ya kuagiza kutoka nje na kuwalipa gharama kubwa sana ya kuweza kutumika hapa Zanzibar. Kwa hivyo, nilikuwa nataka suala hilo tulitizame kwa upana sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, humu sikuliona, naomba niliseme vile vile katika hii sekta ya habari na nimuombe Mhe. Waziri alitizame kwa umakini sana. Sisi kama wawakilishi wa wananchi moja kati ya kazi zetu ni kufuatilia yanayofanyika katika wizara mbali mbali na idara za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kunaripotiwa kuwepo kwa mgongano mkubwa sana wa utendaji katika Shirika la Utangazaji la Zanzibar. Tumeliunda chini ya mfumo mpya ambao Mhe. Rais kaja nao, na mimi naupongeza kabisa kwamba tumeunganisha chini ya shirika. Lakini inaonekana huyu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika kama vile anataka kuchukua madaraka yote sasa, na wale wakurugenzi ambao wamewekwa katika televisheni na katika redio wamekuwa hawapati nafasi ya kufanya kazi zao ipasavyo. Suala hili nimuombe Mhe. Waziri alitazame kwa ukaribu sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili sio siri. Hivi karibuni Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais alifanya ziara katika wizara hii na katika mkutano uliomalizikia tulipata bahati ya kuona sisi wengine katika vyombo vya habari walioneshwa kwa ukamilifu. Wafanyakazi hawakutafuna maneno, wachilia mbali hawa wakurugenzi wa sehemu mbili, lakini hata wafanyakazi wa kawaida, hawakutafuna maneno katika suala zima la jinsi Mkurugenzi Mkuu anavyowaingilia katika majukumu yao na anavyofanya mambo ambayo hayakubaliki. Wamemtuhumu hata kuhaulisha hata baadhi ya vifungu vya matumizi pale na kupelekwa katika mambo mengine ambayo siyo yaliyoidhinishwa na Baraza hili na kuombewa hapa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili alitazame kwa makini.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile wanasema wahenga, ‘sadaka huanzia nyumbani’. Mhe. Mwenyekiti, vikao vyetu hivi vimepata changamoto kubwa na vinafuatiliwa sana na wananchi kwa sababu vinatangazwa moja kwa moja katika televisheni Zanzibar na katika redio Zanzibar. Kwa hivyo, wafanyakazi wanaokuja hapa, muda mrefu tumekuwa tukilipigia kelele, hawatunzwi ipasavyo na tukifuatilia anayetajwa ni huyu huyu Mkurugenzi Mkuu wa ZBC. Mambo haya ni ya kitaalamu huwezi ukaweka *ceiling* ukasema shirika litahudumia wafanyakazi kadhaa, halafu wanaohitajika ile shughuli yote ikamilike ni zaidi ya idadi ile.Sasa unapowaambia mwisho idadi hii hiyo shughuli itafanyika vipi.

Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri hili alitazame sana. Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa sekta hii wana malalamiko mengi sana, hawa wanaokuja hapa pamoja na mafundi wao na watangazaji wao, wana orodha ndefu wenyewe, wanadai malimbikizo tangu kikao cha bajeti kilichopita mpaka tunaingia kikao cha bajeti chengine kinachokuja kesho kutwa hapa, hawajalipwa posho zao. Nimuombe Mhe. Waziri alitazame. Isiwe wakubwa tu waliokuwa katika sekta hii ndio wanaonufaika, na hawa wafanyakazi ambao ndio wenye kazi, sio kazi ndogo Mhe. Mwenyekiti kusimama hapa ukafanya kazi ya kuturikodi ili wananchi wakafaidika huko na ndio tunajenga demokrasia, wananchi wanapata kufuatilia mijadala ya wawakilishi wao kujua wanavyowatetea. Kuna mambo yao mengi kabisa nilikuwa nataka wayatazame sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia wana malalamiko yao hawa kwamba kuna masomo ya Uholanzi walipelekwa mwaka 1998, wakatakiwa kuna baadhi ya huduma wajilipie wakaambiwa baadae watalipwa mpaka leo hawakulipwa. Tunaomba hili litizamwe kwa karibu sana.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, waliahidiwa posho la maziwa, wanafanya kazi ambazo zinatoa mionzi mikali ambayo inaathiri afya zao, lakini kujaribu kulifidia hilo wengi wakashauriwa wawe wanatumia maziwa, hawapewi posho la maziwa, wanatumika muda wa zaidi ya saa za kazi lakini hawalipwi muda huo. Kuna utaratibu wa likizo, likizo zao zimesahauliwa, hata usafiri Mhe. Mwenyekiti. Leo Baraza la Wawakilishi liko huku Chukwani, hii ni kwa upande mmoja tu. Lakini wanafuatilia shughuli nyengine katika maeneo mengine, pengine wanaweza kufika mpaka Nungwi wanatakiwa kufuatilia mambo mbali mbali.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano huu wa Baraza la Wawakilishi, ofisi zao ziko Karume House. Leo matokeo yake wanadhalilika kuwangoja Waheshimiwa Wawakilishi watoke ndani ili wawaombe lifti, sio utaratibu mzuri Mhe. Waziri. Kwa hivyo, isiwe wakubwa wanafanya ugomvi wanagombania gari, lakini wafanyakazi ambao wanatoa huduma hasa wanasahaulika wakati wao ndio wanategemewa wafanye kazi sana. Nakuomba Mhe. Mwenyekiti, suala hii tulitizame sana.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya ya utangazaji yana mambo yake, ili utangaze unatakiwa upendeze pale ukitoka katika *screen* ya TV. Kuna mambo muhimu yanatakiwa yawepo pale, mavazi yao, akina mama vipodozi vyao na mambo mengi tu. Mhe. Mwenyekiti, mara moja nilipokuwepo Uingereza niliwahi kualikwa katika studio fulani kwenda kuhojiwa. Ukifika wewe uliyealikwa unapelekwa katika chumba kwanza kwenda kutengenezwa ili utakapotoka kwenye *screen* upendeze vizuri. Seuze hawa wafanyakazi ambao ni kazi yao ya kila siku. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili alitazame kwa ukaribu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na sekta ya habari kwa kulizungumzia gazeti la Zanzibar Leo. Gazeti la Zanzibar Leo linafanya vizuri na mimi nataka nilipongeze tena kama nilivyolipongeza mwaka jana. Kila siku zinavyokwenda tunaliona kwamba linaongeza ufanisi hata *standard* yake inaongezeka, lakini tuseme bado lina changamoto. Niliwaambia mwaka jana tulipokuwa hapa, kwamba isije ikageuka hadithi ya mgema kwamba akisifiwa tembo akalitia maji, bado wanahitajika kufanya kazi kubwa sana ili wazidi kuliimarisha.

Moja katika hilo Mhe. Mwenyekiti, wana malalamiko yao hawa. Gazeti hili ni la serikali lakini linaendeshwa chini ya shirika linaendeshwa kibiashara. Sasa kama tumeamua lijiendeshe kibiashara maana yake wizara zinapotoa matangazo katika gazeti hili, ili lijiendeshe kibiashara lilipie matangazo haya. Utakuta kunakuwa na madeni makubwa sana katika gazeti hili, matokeo yake linakwama kujiendesha.

Nashukuru katika ripoti nimeona humu, wamefika pahala wamelipa madeni ya kampuni zilizokuwa zikichapisha gazeti hili ni hatua kubwa, lakini tukilipa kila wizara itakapotoa tangazo ikalipa, basi tutalifanya lipate ufanisi vizuri zaidi na liweze kujipanga kitaalamu zaidi. Naomba kwa sababu ya muda Mhe. Mwenyekiti, hilo niliachie hapo. Lakini nasema nawapongeza na niwaombe na wao waimarishe utendaji wao.

Mhe. Waziri pia na yeye akae nao kwa karibu, pengine na wao wana matatizo kama haya ambayo yako katika Idara ya Redio na Televisheni, aone haja ya kuyatengeneza. Kama nilivyosema namuamini kabisa Mhe. Waziri, naamini katika hili atawasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niondoke katika sekta ya habari, kama nilivyosema kwa sababu ya muda hautoshi kuingia kwa undani. Nije katika Kamisheni ya Utalii. Suala hili sitaki kulizungumza kwa urefu sana, kwa sababu juzi tu tulipokuwa tukijadili mswada hapa wa marekebisho ya sheria ya utalii na tumezungumza kwa undani mambo mengi, nina hakika Mhe. Waziri atakuwa kayapata tunayozungumza hapa ili yafuatiliwe. Lakini moja hili linawahusu wapiga kura wangu hasa Mhe. Mwenyekiti, naomba niliseme hapa.

Mhe. Mwenyekiti, Mji Mkongwe ndio moja katika maeneo ambayo yana vivutio vikubwa vya utalii. Lakini pia Mji Mkongwe ndio makao makuu ya serikali ya nchi hii, kama tungekuwa tuna hesabu *Cape Town* ya Zanzibar ni *Zanzibar town*, basi roho yake ni Mji Mkongwe na ndio maana bado huduma nyingi za kibiashara, za kiserikali na za kijamii ziko katika Mji Mkongwe. Hata katika hili la utalii, kwa sababu ndio kitovu cha biashara Mhe. Mwenyekiti, maduka mengi ambayo yanahudumia watalii yako katika Mji Mkongwe, yanauza *souvenir* na vitu vyengine.

Lakini sasa Mji Mkongwe unaonekana hii kuwa ndio kituo kikuu cha biashara, ndio makao makuu ya nchi, inakuwa ndio sumu yake. Kila mwenye kutaka kukamua anaingia Mji Mkongwe. Sasa huyu ng'ombe

keshakamuliwa mpaka sasa nafikiri maziwa yanakwisha karibu itatoka damu Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, naiomba serikali ilitazame hili kwa ujumla, lakini na wizara hii iniambie kwa kupitia Kamisheni ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, jana walinifuata wapiga kura wangu ambao wanaendesha shughuli za biashara, wanaendesha maduka ambayo yanatoa huduma kwa watalii. Sasa imekuwa ni pahala pa kupiganiwa, huku Kamisheni ya Utalii inawaambia kwa sababu mnatoa huduma za utalii, wanaambiwa wakate leseni kutoka Kamisheni ya Utalii. Ninazo hapa Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza nitamkabidhi Mhe. Waziri barua ambazo wamepewa wito kwamba hawajakata leseni ya utalii, na ikifika tarehe ya jana waliambiwa mwisho maduka yao yatafungwa. Wanafuatwa mpaka na polisi na bunduki. Lakini wao wanasema huku tumeambiwa tulipe Kamisheni ya Utalii tukate leseni, na huku Baraza la Manispaa linawabana linawaambia wakate leseni kwao.

Mhe. Mwenyekiti, ninazo hapa, kila mfanyabiashara kapewa barua mbili mbili ninazo hapa. Huku na ya Kamisheni ya Utalii anaambiwa alipe leseni dola 50 na huku Baraza la Manispaa linawaambia walipe leseni Shs. 80,000/-. Sasa Mhe. Mwenyekiti, haya hayakubaliki, ikiwa leseni imeamuliwa ya maduka yale ni ya Kamisheni ya Utalii, basi iwe ni ya Kamisheni ya Utalii tu hawana matatizo, na kama ikiwa ni Baraza la Manispaa basi iwe ni Baraza la Manispaa tu. Lakini ikiwa serikali yenyewe haijui haijajipanga kujua kwamba leseni hii atoe nani basi ndio inayowasababishia usumbufu mkubwa wananchi wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nikuombe sana Mhe. Waziri na kama nilivyosema nitamkabidhi hizi *paper*. Kwanza unyanyasaji ausitishe, kwa Kamisheni ya Utalii kuwafuata na bunduki kwa kipindi hiki, mpaka serikali yenyewe itakapofanya maamuzi, kwamba leseni hizi zilipwe na Baraza la Manispaa au zilipwe na Kamisheni ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mengine ya Kamisheni hii ya Utalii tuliyazungumza kwa urefu sana katika kuchangia mswada ule wa utalii, naamini serikali itakuwa imeyachukua na itayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Hoteli ya Bwawani. Mimi nataka niipongeze. Kwanza hii ndio inayoonesha, mara nyengine unapompa kazi mtu ambaye anapaelewa pale pahala basi anachukua hatua nzuri sana ya kuparekebisha. Waliwekwa watu wengi pale wenye digirii na shahada chungu nzima, Bwawani ikawa ni pahala pa watu kwenda kuvuna. Lakini leo pamewekwa uongozi wa muda tu, lakini kwa sababu watu waliokuwepo pale wanajua kuwa riziki yao, kipato chao na mshahara wao unatoka ikiwa Hoteli ya Bwawani itaweza kufanyakazi zake vizuri, basi wanahakikisha hoteli ya Bwawani inakusanya mapato vizuri zaidi na inafanya kazi vizuri zaidi, tunaona tayari kuna mafanikio pale. Kuna huduma nyingi ambazo zilikuwa hazifanyi kazi, lakini ukienda sasa hivi zinafanya kazi kwa kutumia mapato yao wenyewe wanayoyapata pale Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka kuwapongeza sana kwa kazi hiyo na nadhani Mhe. Waziri awe karibu nao, kwa sababu hoteli ina nafasi nzuri sana ya kuweza kutumika ikiwa itasimamiwa vizuri. Kama nilivyosema katika sheria za magazeti na serikali nayo kwa kupitia wizara na idara iache kuifanya hoteli ya Bwawani ni pahala pa kwenda kufanya shughuli zao halafu wakaondoka wakawa hawalipi, au wakubwa wana mambo yao wakaenda kumalizia pale wakaondoka wakawa hawalipi. Mhe. Mwenyekiti, tuyaache haya, kama tumeamua ijiendeshe kibiashara basi tuiache ijiendeshe kibiashara, anayekwenda kutafuta huduma pale alipe ili hoteli iweze kujiendesha vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika Idara ya Makumbusho ya Mambo ya Kale. Mhe. Mwenyekiti, hapa nina mambo mawili nataka kuyazungumza. Kwanza hivi karibuni nilitembelea, namuomba Mhe. Waziri apate nafasi hebu ayatembelee haya maeneo ya kihistoria yote Waziri mpya. Maeneo mengi yameachwa hata hayapitiwi, unayaona hali yake yanaweza yakaporomoka, hata ule urithi uliobakia ukaporomoka.

Hivi karibuni Mhe.Mwenyekiti, nilikwenda kutembelea magofu ya Maruhubi pale, nilikuwa nina wageni nikawapeleka. Ukiingia kule ndani yale yaliyobakia pale ni yale makuba ambayo yanaweza kuanguka saa yoyote, kwa sababu ile dari yake iliyobakia ndani chache imeshaoza na boriti zote ziko taabani, itaporomoka na ikiporomoka maana yake kile kilichobakia cha kuonesha Maruhubi ilikuwa vipi nacho kinamalizika. Sasa haya magofu yanaingiza mapato, haya mapato pia yatumike kuyaenzi na kuyatunza haya magofu huo ndio utamaduni. Ikiwa Zanzibar tunaisifu kuwa ni kituo kikuu cha ustaarabu katika maeneo hayo, hivyo wakija wageni tunawaonesha kule tulikotoka.

Mhe. Mwenyekiti, hata ule usafi wa yale maeneo. Katika miaka ya nyuma Mhe. Mwenyekiti, pengine miaka 10 au 20 iliyopita, ukienda Maruhubi ilikuwa yale mahodhi ukienda pale yanavutia, pamoja na kwamba ni magofu

lakini yako katika hali ya usafi. Sasa hivi ukienda ni uchafu mtupu Mhe.Mwenyekiti. Kwa hivyo, naomba haya yatazamwe kwa ukaribu sana.

Mhe.Mwenyekiti, nilikwenda pia kutazama pale palipokuwa *Palace Ruins*. Lile eneo lililokuwa na Msikiti wa asili pale ubakie na mpaka leo unatumika, liko katika hali mbaya na suala hili la mmong'onyoko wa ardhi kupitia katika bahari, inaweza ikauathiri ule Msikiti saa yoyote ukaporomoka Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji tuutizame kwa karibu na magofu mengine, yako mengi tu kwa Unguja na Pemba kwa jumla yake, sitaki kutaja moja moja, nataka kusema waziri ayatazame kwa ukaribu ili yaweze kutunzwa.

Lakini la pili katika magofu Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la uendeshaji wa magofu yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, yale magofu yana historia zake, na hata utaratibu wa kuyaendesha ni ule utaratibu unaotokana na historia. Kumekuwa na utaratibu sasa wa watu hasa wawekezaji wa kigeni kuvamia wizarani kutaka wapewe wakayageuze mikahawa kila pahali. Ile *heritage* iliyokuwepo pale, historia yake iliyokuwepo pale basi haipewi umuhimu kuliko suala la kuingiza mapato kupitia mikahawa inayofufuliwa kupitia katika kila magofu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, muwekezaji hawezi kuumwa na historia ile kuliko mwananchi. Sasa inapotokezea kumekuja mwananchi ambaye anataka kuwekeza pale, madamu kafikia viwango basi tumpe kipaumbele huyu mwananchi. Mimi Mhe. Mwenyekiti, hili nitalisemea kila pahala hata kama kuna watu wengine hawapendi, kwamba katika hili wala sio aibu Wazanzibari kupigania kwamba kipaumbele apewe Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni palikuwa na mjadala wa Afrika Mashariki, wenzetu ndugu zetu wa damu hawakuwa na tabu kuwasema majirani zetu, hao tunaoambiwa tuna umoja nao, Wakenya, Waganda, Warwanda watakuja kuchukua kazi zao, ajira zao au ardhi zao. Sasa kweli wao kutetea kwao iwe sahihi, sisi tukitetea kwetu iwe ni madhara mpaka kuandikiwa maoni. Lakini sisi wengine hatujali Mhe. Mwenyekti. Mimi sijali lolote. Yatakapokuja maslahi ya Zanzibar na Mzanzibari basi nitasimama kwa nguvu zote kutetea.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri yatakapokuja masuala haya kama kuna Mzanzibari ambaye anaonesha anataka kuwekeza basi tumpe kipaumbele, mradi tu awe ametimiza masharti na vigezo ambavyo vimewekwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niondoke kwenye magofu niende kwenye Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, lakini nataka kuzungumzia suala la sanaa. Hapa ndio kuna suala ambalo linawahusu wapiga kura wangu. Mhe. Mwenyekiti, jengo la Ngome Kongwe lilijengwa kama ni ngome kama inavyosemwa. Sasa hii imekuwa kama ni sehemu ya urithi wetu katika nchi ya kiutamaduni vinatunzwa pale. Lakini vimegeuzwa sasa mule ndani kwamba ni pahala pa kufanyia sanaa za maonesho kuoneshwa pale. Imekuwa ni maudhi makubwa kwa yale maeneo ambayo wananchi wanaokaa pale Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri alitazame upya, najua tumekimbilia pale na ndio tukageuza kwamba ndio ukumbi ule, kwa sababu hatukufanya kazi miaka yote kuwa na ukumbi wa kuonesha sanaa za maonesho katika Zanzibar. Sasa wizara itafute utaratibu wa kujenga hilo. Pale ile ngome iko wazi, lile ni eneo linalokaa watu. Unapopigwa muziki mule ndani. Siku hizi imekuwa ni kila siku, likimalizika hili linakuja hili. Watu hawalali pale Mhe. Mwenyekiti, kunapigwa muziki mpaka alfajiri pale. Kwa hivyo, serikali itafute njia ya kujenga ukumbi ambao au jengo ambalo litaonesha sanaa za maonesho, na haya yanakuwa na utaratibu wake. Hata huko nje tunakotembelea, kunakuwa na utaratibu kwamba hata *sound system* inakuwa ni ya ndani haitoki nje, seuze pale pako wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nimelipigia kelele hili mara nyingi, na nimelifuatilia mwahala mwingi sipati jawabu, nimeona leo nilieleze mbele ya Baraza la Wawakilishi. Nimuombe Mhe. Waziri hili alisimamie kwa karibu sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo tu nigusie suala la uchafu limezungumzwa katika suala la utalii. Nimesema tena hapa kwamba kama utazungumzia uchafu katika mji, hili limetajwa katika ripoti ya kamati kwenye ukurasa wa 127, changamoto juu pale, nambari moja kabisa uchafu uliokithiri.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sitaki kukataa kwamba tumeacha muda mrefu kuwashajihisha wananchi wetu kuwa na utamaduni wa usafi, hilo nakubali. Lakini suala la kukusanya taka kutoka katika maeneo ya makaazi na kwenda kuzitupa katika eneo lililokuwa limewekwa, hili ni jukumu la serikali kupitia Baraza la Manispaa na wananchi wanalipa. Katika eneo la Mji Mkongwe kila duka linalipa baina ya Shs. 9,000/- na wengine Shs.6, 000/- kulipia kuondoshwa taka. Taka zinatolewa nje, lakini haziondolewi. Majumbani wananchi wanalipishwa. Kuna wakati niliwahi kusema mimi, kama Baraza limeshindwa basi lituruhusu sisi vijana wa Mji Mkongwe

tujikusanye na tuchukuwe taka wenyewe, lakini hii ada ambayo inakwenda kule iachwe kusimamia wananchi, ili wahudumiwe wale ambao watakuwa wanashughulikia taka kama limeshindwa, hayakubaliki.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hasa katika Mji Mkongwe ni eneo ambalo watalii wanakuja kwa wingi kutembelea, lakini uchafu uliokithiri kila pahala, taka zinajaa kwenye yale makontena makubwa yaliyokuwepo pale ya kutilia taka, yanajaa na kufurika mpaka taka zinafurika nje gari la manispaa halijapita kuja kuondosha. Mhe. Mwenyekiti, kweli inatia aibu. Halafu tunazungumza tunataka kuleta ushindani wa kiutalii na maeneo kama *Mauritius* na *Seychelles*, ukienda kule kwa wenzetu miji inang'ara. Kwa hivyo, nilikuwa nasema Mhe. Mwenyekiti, hili naliunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba hivi karibuni kupitia kwa mbunge wangu wa Mji Mkongwe katoa fedha ili barabara ziangaliwe. Naishukuru sana Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa sababu sio jukumu lao, barabara zile za ndani ni jukumu la Baraza la Manispaa, lakini kwa sababu wameombwa na mbunge na katoa fedha zake za mfuko wa jimbo, zile zimeanza kushughulikiwa ni matumaini yangu kwamba zitamalizwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema eneo ambalo linazalisha katika nchi basi litizamwe, lisiwe ni kituo cha kuzalishia mapato kwa serikali, lakini baadae linasahauliwa. Kwa hivyo, naishukuru wizara na rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri hapa yuko karibu yangu, najua kafurahi lakini *Inshaallah* hizi pongezi ninazompa azitumie kukamilishia kazi iliyobakia katika kuzitengeneza barabara hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika muda inabidi mambo mengine niruke ili na wenzangu wapate fursa. Naomba wizara hii niiache. Kwa ufupi kabisa katika eneo moja moja tu, nigusie Wizara ya Mifugo na Uvuvi, halafu nimalizie pia kwa suala moja katika Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Kwenye uvuvi Mhe. Mwenyekiti, kwanza nafurahi kama imebaini kitu kimoja, katika ukurasa wa 137 kifungu cha 6 kinazungumzia, kamati ilipokea taarifa kwamba suala la uvuvi wa bahari kuu bado halina sheria hapa nchini na hivyo, linaendeshwa kwa makubaliano tu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Ingawa sheria kama hiyo iko Tanzania Bara, bado haijaridhiwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutumika Zanzibar, kwani imegundulika kuwa inahitaji kufanyiwa marekebisho ili kusibu mazingira ya Zanzibar. Hivyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iutazame mkataba na makubaliano yote yaliyofikiwa kwa mtazamo wa mbele, ili kuepusha Zanzibar na maafa yanaweza kuepukika. Mimi nataka niliunge mkono Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana katika kikao cha bajeti nilizungumza, kwamba wenzetu katika hili hawako wa kweli hasa katika mapato na nikatoa ushahidi katika kikao cha bajeti kilichopita, kwamba ukitazama ule mgao ambao Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi wakati ule alituambia hapa, kuwa tumepata katika mgawanyo wa nusu mali. Ukitizama majibu ambayo Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Bara alijibu katika bunge mapato yao hayalingani kabisa na hicho tulichopewa sisi ndio asilimia 40 ambayo tulipaswa tuipate. Sasa haya yanaweza kuwa yanakuja kwa sababu ya kuwa tumekubaliana tu kienyeji enyeji, lakini bado sheria Zanzibar. Kwa hivyo, mimi nasema tutazame kama kuna haja ya kui-*adopt* sheria hii ama bado, kwa sababu uvuvi sio suala la Muungano, tuwe na sheria yetu ya uvuvi wa bahari kuu, halafu uendeshaji tu tukakubaliana ipitie mamlaka ile ile, lakini sheria kila mtu akawa ana yake. Hili Mhe. Mwenyekiti, lilikuwa ni suala muhimu sana nilikuwa naomba tulitizame.

Vile vile katika suala hilo la uvuvi Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kumekuwa kuna malalamiko makubwa sana katika utekelezaji wa sheria ya uvuvi hasa kuhusiana na mazingira. Nchi yetu ni visiwa, wananchi wengi sana wanategemea kupata rizki zao kutokana na uvuvi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunapobana sana katika sheria zetu basi hufika pahala tukawafanya badala ya kuwapa ajira tukawanyima ajira wananchi wetu wanalalamika. Hivi karibuni tulipokea ujumbe mkubwa sana, kwa wavuvi kutoka Chwaka Mhe. Mwenyekiti, wana ugomvi mkubwa kati yao na Marumbi kwa sababu ya masuala haya haya ya kusimamia sheria.Kwa hivyo, nilikuwa naomba serikali itazame upya katika hili, tusiwe tu tunaletewa matakwa ya kimataifa yakafika pahala pa kuwaathiri wananchi wetu, mwisho jukumu letu lililobakia pia kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tutafute *the right balance* baina ya kutunza mazingira, lakini pia yasiwaathiri wananchi wetu katika kupata rizki zao kupitia uvuvi.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nimesema nitagusia suala moja tu katika eneo la Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Bahati mbaya kama nilivyosema Mhe. Waziri hapa hayupo. Mhe. Mwenyekiti, kuna malalamiko makubwa sana ya wananchi wa Zanzibar katika suala zima la kuzingatiwa sheria

za kazi na waajiri, na wizara haionekani kwamba inafanya kile ambacho kilipewa jukumu na Mhe. Rais kukifanya, kulinda haki za kazi za wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, serikali haiwezi kuajiri kila mtu, kuna watu wanatafuta ajira kwenye sekta binafsi, lakini hakuna usimamizi mzuri. Hivi karibuni kumejitokeza zoezi la watu kutafuta kazi kupitia kwenye ubaharia, kuna mawakala wengi hapa wanatafuta vijana wanaofanya kazi hii, lakini hakuna utaratibu mzuri wa kusimamia. Sizungumzii wale mawakala ambao hawakuandikishwa, hawa mawakala wameandikishwa na ofisi zao zinajulikana, lakini bado kumekuwa kuna unyanyasaji mkubwa sana wa vijana wetu ambao wanatafuta kazi katika maeneo hayo. Lakini wizara haionekani kusimamia, niombe sana hili.

La pili Mhe. Mwenyekiti, katika hili suala la kazi kuna wafanyakazi wa Kizanzibari wako katika hoteli za kitalii. Kuna tuhuma kwamba baadhi ya viongozi katika wizara ya kazi wamo katika makubaliano fulani na wawekezaji katika sekta ya utalii, kiasi ambacho wanawasaliti wafanyakazi wanaokwenda kulalamika katika wizara ya kazi kwamba haki zao hazilindwi. Kuna watu katika wizara ya kazi wanarudi kuwaambia wale wenye hoteli nani kaja kushitaki, badala ya wale wafanyakazi wanakuja kushtaki kwamba haki zao zinalindwa, basi wao ndio wanakuwa wanaadhibiwa kwa kufukuzwa kazi katika hoteli kwa sababu wanaambiwa wanaripoti katika wizara.

Kwa hivyo, nataka waziri alitazame hili kwa umakini, kama yeye hafuatilii kwa ukaribu, kuna watu huko chini ambao haki zao zinaguswa wanafuatilia Mhe. Mwenyekiti, naomba sana.Isije ikafika kama vile alivyosema Mhe. Mshimba kwamba kuna watu wanajinasibu kuwa serikali wameiweka mkononi au wameiweka mfukoni, hili ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti. Wizara ya kazi ilinde haki za kazi za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema suala hili ni la mwisho.Mwaka jana, nimuombe Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, hayupo, sijui nani atachukua maelekezo hapa au baadae serikali itatujibu.Nilizungumzia suala la wafanyakazi wa Zantel karibu 200 ambao wamepewa zile ajira za mule za *daily pay* kwa miaka zaidi ya nafikiri 10 inakaribia, lakini bado hawakuajiriwa.Nikampa waziri akaniahidi kulifuatilia hapa. Nilimuuliza maswali ya nyongeza mara kadhaa ya suala hili.Kila nikimuuliza, ananiambia karibu tutafikia muafaka, mpaka dakika hii ninayozungumza Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wale wananifuata hakuna chochote kilichotekelezwa na serikali. Sasa mambo kama haya Mhe. Mwenyekiti, yanawavunja watu moyo. Mawaziri wanapotupa majibu hapa, tunapotoa malalamiko ya wananchi wakasema tutayafanyia kazi, basi iwe wanayafanyia kazi kweli, isiwe kutuondosha njiani tu, kwa sababu kama wanadhani sisi wanaweza kutudanganya, kuna wananchi huko ambao ndio hao wanaoathirika, wanaendelea kutufuata sisi na kutuambia kuwa mmeambiwa hili na waziri lakini mpaka leo halijatekelezwa.

Kwa hivyo, nimuombe sana waziri wa kazi, suala la Zantel nililomwambia kuhusu wafanyakazi, basi afuatilie haki zao ili ziweze kupatikana, wametumika kwa muda mrefu hawa, waweze kuajiriwa sasa ili haki zao zipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunivumilia. Lakini kama nilivyosema, haya mambo ni mengi, kamati moja inagusa wizara nyingi na yote ni hapa hapa pa kuyazungumza ili haki za wananchi wa Zanzibar ziweze kulindwa. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, nategemea kupata maelezo ya kina kutoka kwa mawaziri wanaohusika, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile leo ni siku ya Ijumaa na muda wetu tuliobakia nao ni mchache mno. Naomba kuchukua nafasi hii kuakhirisha kikao hiki hadi jioni, saa 11:00 barabara ili tuweze kuendelea na majadiliano. Jioni tutaanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuchangia Kamati ya Utalii, Habari na mambo mengineyo, kwanza nimpongeze sana Waziri mpya aliyeteuliwa katika Wizara hii ya Habari na Utalii. Mhe. Waziri karibu sana, nimpongeze sana katibu wao aliyeisoma taarifa yao au Mwenyekiti, mimi nampongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya mwenyekiti imesheheni mambo mengi sana imechambua sekta hadi sekta na imeeleza yale ambayo wameyaona wao kama wana kamati na hiyo ni kweli hawapotoshi, kwa sababu kamati hiyo ina wataalam wengi sana hata leo huyo mwenyekiti aliyeisoma ni mtaalam mkubwa sana na yeye ana *idea* nyingi katika Wizara hii kwa sababu alikuwemo huko nyuma katika utendaji wake wa kazi mpaka kufikia kuwa Mheshimiwa, nae alikuwemo. Kwa hivyo mimi naamini kuwa kitu kilichofanyika ni kitu cha uhakika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, siku hizi nitakua na kawaida na kutokana na hali halisi ilivyo na baraza lilivyotusomesha jinsi ya kuitumia katiba itakua ni dhambi kabisa kumuonesha kwamba *UNDP* aliyetuletea zile fedha zako haki yako, kumbe wajumbe tumezitumia kihalali kabisa na tumefahamu katiba.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa tatu na kila siku hukaa nasema nilikua zamani simjui nani Mzanzibari nilikua napata shida sana, lakini kwa kua mwalimu wangu mwanasheria yumo humu ndani nashukuru sana huwa mara nyingi hapendi kunikosoa anapenda sana kunielimisha na kunifahamu, sasa hivi ameniambia kijana wangu umekuwa mwanasheria mdogo kutokana na vile nilivyopevuka. Mimi sitaki niseme kuwa kumzidi yeye sipendi kabisa na wala sitofanya kitu hicho.

Lakini nikienda katika kifungu cha ukurasa wa tatu kifungu cha tano kila Mzanzibari kwa misingi ya katiba hii ataweza kufaidika na haki na fursa zote, tumemtia Mzanzibari ndani ya katiba na siku zote tunasema katiba ndio roho ya nchi huwezi kuwa na nchi kama huna katiba hata siku moja ni lazima uwe na katiba, ili katiba ile inaonesha mipaka yake ya utendaji wa kazi na jinsi gani haki ya wenye katiba kuweza kupata katika maeneo kadhaa wa kadha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nalia na utalii serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka wazi kabisa watu wenye fedha zao waje kujenga hoteli za kisasa kwa lengo zuri sana, ili wananchi waweze kupata ajira kwa kujiondolea umasikini hilo suala Mhe. Mwenyekiti, halifichiki inasikitisha sana dhana nzuri sasa imegeuka kuwa dhana mbaya, mimi nikisema jambo Mwenyekiti ujue sisemi kwa kudakasha, kwa utashi, kwa kumchukia mtu mimi wote nawapenda hakuna hata mmoja nisiyempenda hapa wote nawapenda na wote rafiki zangu. Lakini ninapofika pale nikasema huyu nampenda na nitamsema kutokana na sifa zake wapo humu nawapenda sana ndani ya roho mawaziri wazuri tu wapo rohoni mwangu.

Lakini uovu sipendi kuficha Mheshimiwa hata bahari haikubali kuweka uchafu italeta juu tu, leo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema hata viongozi wanashiriki nina simu yangu nimepewa majina ya viongozi aibu ni viongozi wakubwa tu, nimeshangaa nilipoletewa *message* ile unaona tumbo langu limezidi kuwa kubwa lakini nilipuuka alaa kumbe ndio mwenendo wenyewe tukubaliane hivyo. Nikisema Mawaziri wakubwa au watendaji kitendo hichi wanashiriki baadhi yao Mawaziri hatari.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye hoteli moja inaitwa *Blue Bay* Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanalia, watanzania wanalia wanavyonyanyaswa na ndugu zetu wa Kenya wanasema nyinyi semeni mukisha. Alisema Mhe. Ismail Jussa Ladhu sijui kwa nini asiweke wazi leo simlaumu lakini alikusudia kuwa atanitupia pasi sasa mimi nimeidaka ile pasi, na mimi nitatoa pasi kwa mwenzangu.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanavyodhalilishwa ukenda kupeleka ripoti kule basi wakifika kule kupeleka ripoti wakiondoka tu inapigwa simu katika hoteli ya *Blue bay* kaja leo Juma anasema hili na hili vipi siku ya pili anafukuzwa kazi, jamani tunakwenda wapi ushahidi ninao umo ndani ya simu na iko siku nitaweka wazi, leo natoa *message send* ifike tu lakini iko siku nitatoa wala sifuti imo humu na sitoficha kabisa tena nitakua na tahadhari nitailindisha hii nitaweka askari, Mhe. Mohammed Aboud nisaidie nipate askari simu yangu ilindwe hii iko siku itatoa habari hizo. Watu wanafukuzwa kazi kwa kupewa taarifa tu kaja leo fulani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naanza kutoa uovu na siku zote mimi nikisema sisemi kwa kubahatisha natoa kwa *document*, *list* hizi ninazo mbili moja imenipotea sijui nimepigwa kipapai inipotee lakini siwezi kujua lakini labda imerogwa ndio ikapotea, *list* hii ni wakenya watupu hebu iangalie orodha hii. Wengi sana tu orodha hii hebu nambie hatujatawaliwa tu hii hapa orodha ninazo mbili, Hoteli ya Baraza, *Breez* huko ndio walipo tele tele kweli Mzanzibari atapata haki hapa fursa ya katiba imo humu, juzi tumesema sana kumbe bado tunaonekana wawakilishi tunaimba tu hatuimbi halafu mnatuchukia potelea mbali tuchukieni. Tutapambana na vita hivi hatukubali wengine humu nimetia *tick* wameshaanza kukimbia usiku wa jana kuamkia leo, walijua sijui na leo Mshimba atasema wameanza kukimbia nimetia *x* ndogo ndogo hawa naambiwa wameshakimbia hawa.

Lakini hebu angalia waliokimbia ni wachache kama kumi tu lakini waliobakia ni wengi tunazubaa, leo Mkenya ana *passport* ya Tanzania kama wenyewe wapo Uhamiaji wanisikilize huyu mtu amewadanganya amepeleka vyeti feki sasa akaona vile vyeti kwa hapa Zanzibari nimefanikiwa akaona akachukulie *passport* kwa Dar es

Salaam. *Passport* hiyo AB 499838. Mkenya leo ameichukua hiyo *passport* kesho mtampa ardhi hakuna sababu asichukue ardhi ni Mzanzibari halisi huyu. Mtu huyu anafanya kazi *Fisheman Resort* halafu unasema Mzanzibari ana haki ndani ya katiba Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema hapa tuko *serious* iwe leo *list Member* kama hii ya Wakenya wako kibao katika Zanziar hii kiasi waseme kuwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wwajumbe, tumpe nafasi Mheshimiwa Mjumbe kueleza yale ambayo anayataka.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nipeni nafasi au hamtaki ukweli *(Makofi)* Mhe. Mwenyekiti Wazanzibari wameshachoka kuchukuliwa haki yao, kama ni jambo la kufanya mfano hebu twenzetuni Kenya mimi na wewe na mwengine yoyote twende tukatake kazi kule, kwa nini jamani Zanzibar tumekuwa tuko huru kiasi hichi. Mimi siku moja nilimsikia mkubwa mmoja anasema hao Wazanzibari hawakusoma wewe unasema Mzanzibari wako hakusoma twende mitaani tukaoneshane wenye PhD hebu twendeni tukakuonesheni.

Mimi kwenye maskani yangu nina watoto Form six nina watoto PhD, nina watoto Form IV nina watoto Form III wako kibao wamekaa kule mitaani hawana kazi halafu kiongozi unakuja kusema hapa Watanzania hawataki kusoma, sikweli nakataa Mhe. Mwenyekiti hata siku moja. Mhe. Waziri ndio kwanza umeingia kazi hii tunakupa sio mchezo hii tunanyang'wanywa haki zetu Wazanzibari ilinde kwa nguvu zako zote na sisi tutakulinda.

Mhe. Mwenyekiti, leo anakwenda kupewa kitambulisho kimetoka Kamisheni ya Utalii na Sheria ya Kamisheni ya Utalii ili uweze kupata *certificate* au upate kibali cha kuweza kutembeza wageni lazima uoneshe ukaazi wa Mzanzibari, mtwana anayo huyo ID No. 5200288885 kapewa huyo Mtu wa Kitope hana hiyo ID huyo ni Mkenya huyo kosa kubwa sana hilo. Sheria inasema upate cheti cha Maruhubi sasa kakipata wapi, mwanasheria naomba sana hapa ndio pa kukaa ukatimiza sheria zako, Mwanasheria wangu hapa ndio kazi ya kutafuta sheria. *(Makofi)*

Mimi mwanasheria wako mdogo nitakusaidia mimi ni mwanao, ndugu yako na mwanafunzi wako nimeshajitolea sasa *ama fa ima* lakini nataka haki ya Mzanzibari kwenye hoteli ipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tu mheshimiwa wangu aliyepita hapa Waziri ambae sasa hivi kapelekwa sehemu ya uvuvi wenyewe, alituletea mswada mzuri sana na aliamini hivyo kwamba maana ya mswada ule uweze kuwasaidia Wazanzibari kwa ile haki ambayo imetolewa tuweze kunufaika, dhana hiyo ambayo siku zote na ndio maana nikasema jamani hii aya tusiitumie kwa sababu ni kitu ambacho kwa tafsiri ya Qurani kitu kilichokamilika mimi mnaniona mgonjwa tu mimi sio mgonjwa nakwambieni kwa mantiki yake. Kwa sababu tunatunga sheria lakini haikamiliki kwenye utendaji halafu ndio tunapoitia na aya pale *Alhamdulillah*, hiki sio kitu cha mchezo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeona asili ya kuing'ang'ania ile aya ni kwa sababu ya hiyo kwamba bado mpaka leo wanapata tabu na manyanyaso, leo utakuta Karafuu hoteli kuna mtu anawafukuza kiholela kwa kuwa nini wamekwenda kushitaki Idara ya Kazi, halafu mimi kitu kinachonishangaza mimi nilisema hebu tumpeni na ile Wizara ya kazi Mheshimiwa aweke sawa kabisa sheria zake, tukiweka mbali hatari yake ndio hii mzigo wote tunamtwisha waziri sio nafasi yake hapa, tumempa jina la utalii lakini sheria hana. Angekuwa na sheria basi mimi naamini angekamilisha mambo yote sio kitu cha mchezo, tusione tabu washauri tumshaurini vizuri rais jamani tulione hili.

Mhe. Waziri mpya usikubali ing'ang'anie uichukue wewe hii kwa sababu itakusaidia kwa sababu huna kitu wewe una utalii tu huna sheria, sheria yako ni ndogo sana uliyokuwa nayo *wallahi laadhim* nakwambia lakini vyenginevyo huna sheria. Sasa leo nikikwambia wananchi wanafukuzwa huko utanambia nini utaniambia niende *labour* tunakwenda wapi sasa mimi nitakushangaa wewe ndio mwenyewe Waziri wa Utalii halafu unanambia nipeleke *labour* kwa nini, tunakwenda wapi jamani tusione tabu tuilete huku tukupe wewe ile uone kama hutofanya kazi mimi naamini utafanya kazi vizuri. Lakini cha kushangaza yale maeneo ambayo yanasumbuka na utalii hawanufaiki twende leo Kiwengwa kaitafute asilimia ya watu wa Kiwengwa kama wamo hotelini wananyanyaswa hawapati ati.

Sasa tuna maana gani na kwa sababu gani waziri hamtembei katika *department* zenu kwa mujibu wa utaratibu hili mulikubali waziri wangu musikatae, moja katika kosa kubwa ni hilo tungekuwa tunatembelea *department* zetu na kusikiliza matatizo basi tusingekuwa tukipiga kelele siku zote waheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti, leo nakupa ukweli kuna watu ambao wamekuja nyumbani kwangu kwa bahati nzuri wengine nimewarejesha maana yake ni nusu ya maandamano wamekuja nyumbani.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Hoteli ya *Serena* kule kuna Wakenya wana miaka sita twende kwenye sheria inasemaje, huwezi ukaishi Zanzbar kwa miaka sita umfundishe Mzanzibari aweze kufanya kazi ile, leo watu wanakwenda pale kuchukua pencheni na kwenda kulala wakubwa tusiseme tutasema, watu mnakwenda kule kulala tunawajua msitake tuseme lakini kuna siku tutasema. Watu wanakwenda kuchukua pencheni halafu mna Mzanzibari pale PO hawatetei watu wake basi tu kwa kua na yeye anapata ramba ramba aa, jamani ramba ramba nyengine mbaya tusizikubali.

Mhe. Mwenyekiti, Serena inanyanyasa wafanyakazi kila leo ukifanya kosa dogo unafukuzwa, halafu siku hizi wana mchezo unajua mchezo wenyewe uko vipi Mhe. Mwenyekiti, unatafutiwa sababu ndogo tu Mkenya anafukuza watu hebu tufanyeni *research* siku moja, sijui niseme je. Nikija kwenye kifungu cha 117 na 88 mtanambia hamna uwezo wa fedha ningesema kamati teule iundwe tukahakikishe. Lakini itakua kila siku basi wawakilishi wanataka kamati teule tu msifikirie tunataka pesa, kamati teule itakayoundwa sarafi hii hatutaki hata pesa zenu lakini tuwachilieni tukafanye kazi, inauma sana Serena watu wana miaka sita sasa mimi najiuliza hawa watu wa *labour* wanafanya nini kazi yao nini sheria hawana, miaka sita nimepewa kesi zaidi ya tatu watu wanatimuliwa kila siku, tangu walinzi juzi tu kuna koo moja limefukuzwa bure bure inaumiza sana nataka kucheka lakini inabidi nikasirike.

Wazanzibari tunatafutiwa sababu ndogo tu kile kijiko kikikuponyoka tu kwako wewe ni kosa kesho unafukuzwa kazi kwa sababu gani analetwa mwengine Mkenya pale afanye kazi, Mhe. Mwenyekiti, sasa nawaambia wawakilishi wenzangu wa *back bencher* tukiona hawa wamelala sasa twendeni wenyewe si mchezo twendeni wenyewe *back bencher*. Maana yake tokea siku niliyosema hapa juzi hakuna *action* hata moja iliyochukuliwa watu wana vitambulisho kinyume na utaratibu, watu wameshajaa sasa hivi hotelini nimeonesha orodha hii hapa nimekwambieni mie watu kibao hotelini wamejaa hawa hapa na karatasi hizi mbili *full* wamejaa. Waziri husika wakifika hapa wanakaa kimya ndio maana nikataka tufanye kazi na mwanasheria wangu si mchezo tutakuja kudaiwa mbele ya haki.

Mwanasheria tutafute sheria tuitekeleze kwa kuwaokoa Wazanzibari lakini vyenginevyo vyovyote katiba yetu inatupiga fimbo hii hapa, nani Mzanzibari haki zake azipate. Mkenya ana ardhi Matemwe baada ya msuko suko juzi kakimbia Sheha kauza ardhi na Diwani nasikia naye kauza ardhi Mkenya kapewa ardhi na *passport* kapewa Zanzibar kachukulia hapa na kila kitu kapewa, kakimbia juzi sijui leo ya ngapi kakimbia. Mhe. Mwenyekiti, tuko maana yake mimi nashangaa ata sijui tuko vipi hii ni serikali kamili tena dola la kitaifa, serikali ya kitaifa sio kitu cha mchezo wenzetu nchi za nje wanachukua mfano kwetu serikali ya kitaifa ina mfumo gani na iko vipi tizama mfumo wake sasa hivi huu hapa mzuri tu ni wa kuwatetea haki za wanyonge ndio maana yake serikali ya kitaifa hakuna njia nyengine yoyote. Lakini kuna mambo mengine ambayo ya kushangaza hebu mimi naomba watueleweshe kuna maduka kule mjini nani mwenye haki ya kukusanya au kutoa leseni kati ya halmashauri na kamisheni ya utalii, hebu twambieni mvutano huo uko je nani mwenye haki zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naondoka huko sasa hivi nakuja kwenye uvuvi niachie leo Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uvuvi huu haramu tukitaka tusitake na sisi viongozi tunashiriki baadhi ya viongozi tunashiriki wewe humo huna bahari, uvuvi huu wa haramu hawishi tusidanganyane chombo kama sinacho Mshimba basi anacho Jussa, hana Jussa anacho Haji Omar Kheir hiyo ndio namna yenyewe. Mheshimiwa kama huyo ikikamatwa boti yake imevua uvuvi haramu yeye ndio mkali na yeye anajisahau kama ndiye anaetunga sheria hapa, anapiga simu iwacheni yangu mie hiyo. Haya niambie leo uvuvi huo utaondoka wa haramu tutawagombanisha wananchi wetu, hili ndio tatizo letu tuseme ukweli ulivyo, lakini wale wanyonge waliokua hawana bodi ya wakubwa wanafungwa kwa kua hana msimamizi yule mnyonge.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tuamueni kitu kwa sababu kuna mambo ambayo kama tutayawacha yanatuathiri na yatatutia njaa na sheria hebu tuiregeze kidogo sio kumwachia mtu kwenda kuvua aa, lakini kuna mambo mengine hebu tuyatizameni mimi juzi niliuliza hapa nipewe tafsiri ya chupa, kuna chupa ya gesi na kuna chupa ya kuvaa kwenda kule baharini sasa sijui ipi tafsiri yake kwa sababu mimi nashindwa. Kwa sababu mvuvi akivaa chupa ya gesi anaambiwa kosa, mzungu akivaa chupa ya gesi akienda chini kuzamia inaitwa chupa ile sasa hivi sheria ziko je mimi hapa inanikanganya hebu tuwekwe wazi katika tafsiri hii, ili ifafanuliwe tuweze kujua.

Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo kule Marumbi na Chwaka na hili nani asiyejua liko muda mrefu sana juzi tu kuna boti zimechomwa moto, wengine wamepigwa mawe jamani maisha haya yataisha je na wote ni ndugu mmoja, ukimuuliza huyu anakwambia kiongozi fulani anasimamia kwa upande huu, ukiuliza huyu anasema kiongozi fulani anasimamia upande huu. Jamani zile ni roho za binaadam hebu tufike pahali tukae chini tuwaite tuwaambie tena basi ni watu ambao hawana tatizo, unajua binaadamu unapokwenda pahali ikawa hujui na ukielimishwa basi ukijua unasema sasa mimi jamani basi, hawa watu hawana tabu watu wa Chwaka hawana

matatizo na watu wa Marumbi hawana matatizo. Wako tayari kabisa kukaa chini tulimalizeni tusende kule na itikadi zetu zilizokua za aina yoyote tuwache twende na ubinadamu tumuogope Mungu wale binaadamu wasije kuuwana.

Kwa hivyo ndio maana nikasema kua kuna mambo mengine viongozi tunachangia wenyewe, sasa viongozi katika masuala kama yale tusichangie tujaribu sana kuogopa kwa sababu pale wanapokufa wale jukumu na wewe kiongozi unachukua kabisa, tujisafishe viongozi. Mwalimu wangu anasema nikisema Makka basi ananambia Makka ni mji hebu twendeni tukahiji, tujiandae kwenda kuhiji yale mengine tuyawache jamani.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mie ata sita sasa hivi sina matatizo ninaelekea ukingo wa kumaliza Mhe. Mwenyekiti, nimeeleza Idara ya kazi katika bajeti inayokuja nawaombeni sana. Lakini hii hii idara ya Kazi kuna lile jengo la Mahakama hivyo Waziri sijui halioni lile jengo na sidhani kama Waziri anamjua huyu Jaji wake wa Mahakama sidhani kama anamjua kama angekuwepo leo ningemwambia ajibu kama anamjua, sidhani kama huyu ndio jaji wake anamjua sidhani.

Mhe. Mwenyekiti, hilo jengo bovu maana yake sijui huyo jaji atatoa haki vipi pale kumpa mnyonge ambaye amedhulumiwa kwenye kazi, matatizo yapo mengi sana ya watu ambao wamefukuzwa kazi kiholela wanaotiwa hatiani na mpaka leo pesa zao hawajalipwa. Tunapoamua mtu kumtia hatiani tujiandae adha ushinde au ushindwe na unaposhindwa yule mtu umlipe pesa zake za kumuweka muda mwingi nje, hili nalo tuna matatizo sasa hii Mahakama hii ikitoa hukumu.

Mhe. Mwenyekiti, samahani sana naomba nitoe utangulizi kidogo kuna mfanyakazi mmoja wa wizara ya afya anadai pesa chungu nzima mpaka leo hajalipwa na Mahakama imeshatoa hukumu, sijui sababu gani zinazokwenda na serikali hiyo hiyo ndio iliyomtia hatiyani yule ooh una matatizo fulani sijui nini nini akenda na Mahakama akakutikana arudishwe kazini lakini alipwe haki yake, lakini mpaka leo haki yake haijalipwa na hii kwenye bajeti nitasema sana haki yake alipwe, pengine nitaizuia bajeti hiyo lakini babu yangu simkeri atamtafutia haki yake namuaminia babu yangu .

Kwa sababu ana watoto wanamtegemea na huko nyuma amekopa sana hana kitu cha kulipa, sasa hayo ndio niliyokua nataka kusema. Lakumalizia tizama sasa hali halisi ilivyo jinsi gani ilivyo Mkenya alivyopewa nguvu Mzanzibari au Mtanzania hakupewa nguvu.

Kuna kesi imetokezea hoteli ya Baraza kuna mkuu ambae yeye ni *chief maintenance* ni mfuasi wake tu kamwambia nichukulie mzigo wangu huu wa taizi nenda kanipelekee nipate pesa, cha kushangaza yule mtu kafikisha ule mzigo umekwisha lakini kumetokezea matatizo. Kutokea matatizo sasa yule mwenzangu mie kwa kua ni Mtazania au Mzanzibari yeye kafukuzwa kazi na kiinua mgongo chake kapewa shilingi laki tatu lakini yeye hakupewa sijui zimepelekwa kituoni huko, ama zimekwenda kwa mkuu wa kituo au kwa nani hazijulikani pesa zile ziko wapi. Lakini Mkenya yeye karudi kazini kesi hiyo ipo RB 3273073 kituo cha Paje na mpaka leo kesi hiyo ipo. Namuomba Kamishna kama ananisikiliza aifatilie. Kwa nini kesi hii sheria isichukue mkondo wake wakati muhusika mmoja yupo anafanya kazi mpaka sasa hivi anaendelea yule kule kafukuzwa kazi kwa tuhuma za wizi.

Leo hii Mheshimiwa tunaonesha dhahiri kutokana na hili kwamba unyanyasaji upo dhahiri. Kumalizia kwangu Mheshimiwa nasema kua sasa Wazanzibari nataka nikwambieni na Mhe. Waziri, Wazanzibari wameshaamka wanadai haki yao kwa kupitia *back bancher* na hiyo haki itapatikana bila ya tatizo lolote.
Kwa hayo machache naomba nimalizie hapa. Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Kitope wamenambia nikae nimsikilize Waziri atakuja kutujibu nini. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kuweza na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika Kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Kwanza sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa Kamati hizi. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana na inastahiki kupewa pongezi.

Moja katika kazi muhimu ambayo Kamati hii imefanya ni kwamba wameweza kuangalia kwa kina miradi yote ya kitaifa jambo ambalo la kupewa pongezi. Hayo ndiyo mambo ambayo inatakiwa kamati iweze kuyaangalia kwa kina aina ya miradi inayoingia kila mahala na kuweza kupitiwa na kuchunguza. Tunashukuru kwa hayo.

Vile vile kamati hii sina budi kuishukuru tena kwa kazi kubwa ambayo imefanya ya kuweza kufatilia mapato na matumizi ya serikali na zaidi kuangalia matumizi ambayo wamezingatia katika suala zima la thamani halisi ya

fedha. Kwa sababu hapa tunapotakiwa katika kuchunguza mambo yetu tuangalie kwamba serikali inatoa fedha yake na tunataka tuone kwamba fedha hii inafanyiwa kazi kama inavyostahiki.

Kwa hivyo ujenzi wa nyumba zote zinazojengwa au kitu chochote ambacho wizara inafanya iangalie kwamba je, kweli thamani ya pesa inayotolewa inalingana na kitu kilichojengwa kama ni nyumba, hospitali au kitu chochote. Hii tunashukuru kwamba masuala haya wameweza kuyapitia na kuona hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la uchambuzi wa mapendekezo ya serikali. Katika uchambuzi tunaamini kwamba kuna kitu tunakiita makadirio. Tunaona kwamba makadirio yanakuwemo katika wizara zote. Kwa hivyo wamejitahidi kuangalia kwamba wamefanya uchambuzi mzuri katika mapendekezo yaliyoletwa na serikali na kuona kwamba wizara hii matumizi yake yanakua ni mazuri ambayo ni ya kupigiwa mfano. Kwa hiyo tunaipa pongezi kamati hii kwa kufanya vizuri. Hili ni suala la *estimation* kwamba serikali inaleta agizo wanapeleka na wao wanatoa *estimate* yao kwa hivyo ile *estimate* ni lazima ifatiliwe.

Mimi ninachokisema sasa hivi kwamba ningeomba hii kamati izidi kufikiria katika suala zima la *centralized system of government* yaani haya ni mambo kutoka juu kuja chini. Tukifanya hivi kwa muda mrefu itakua ile demokrasi yetu hatukuihalalisha sawa sawa. Lakini tunategemea kwamba si muda mrefu tutatoka katika *centralized system of government* na kuingia katika *decentralization* na *devolution*. Kwa hivyo hapa mimi nataka hii Kamati ili kuona dhamana yao kwamba ni nzuri wahakikishe kwamba suala la madaraka Wilayani yanakwenda sawa sawa. Hii ni wajibu wao kuona katika Wilaya zote tunapata serikali za mitaa.

Zaidi ya hayo kuipa pongezi tena Kamati hii juu ya mswada wa Sheria kupitiwa na kuweza kutoa maoni yao katika miswada yote ambayo inaingizwa katika kamati yao. Kwa hivyo wamejitahidi na kuona kwamba ahadi za serikali zinazotolewa katika Wizara wameweza kuzifatilia vizuri na kuweza kuzichambua na kuweza kutoa maoni yao na wao wameona kwamba utekelezaji wote umekua ni mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ni kuona kwamba Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti, wajibu wa Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti iwe inawajibika katika mambo yake yote ya sera zake nzuri *policy* yake ni nzuri na vile vile katika suala zima la mipango na sera na utafiti, utafiti uwe unatekelezwa. Suala la utafiti nafikiri tumelizungumza kwa kina, hapa Kamati hii inawajibika katika suala la Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti, ihakikishe kwamba utafiti unakwenda kama tulivyozungumza juzi, kwamba utafiti huo ni muhimu. Katika nchi zote zilizokua zinaendelea hakuna wizara ambayo ndani yake haifanyi utafiti katika mambo yake. Ikiwa kuna mipango mitupu utafiti hamna haijakua sawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, tuone kwamba watafiti hao waweze kuichunguza ardhi yetu kuiona ni ya aina gani ya ardhi, wadudu ambao wanaihujumu ardhi hii au udongo wake ni udongo wa aina gani ni *acidic* au si *acidic* kwa sababu kuna vipando vyengine unaweza kuvipanda katika ardhi visikubali kutona na hali ya ardhi kwa sababu ardhi ina *elements* nyingi ndani yake, unaweza kupanda kitu kisiwe. Kwa hivyo tunategemea kwamba utafiti utafanywa wa kina ili kuona kwamba ardhi yetu yote nzuri inatekelezwa kutokana na huu usimamizi huu mzuri wa kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, si ardhi peke yake inayohiji kuangaliwa pia hata maji kuona aina ya maji yenyewe, wanyama kama hawana maradhi, tuangalie mifugo yetu yote kwa jumla, matunda pamoja na mboga mboga. Hata utafiti ni lazima ufanywe kutokana na maradhi tuliyonayo mengi sana ya matunda pamoja na wanyama wetu ambao kuna *transportation* ya wanyama wa kutoka nje kuja ndani na *transportation* ya matunda ambayo yanatoka nje na kuingia ndani ya nchi. Kwa hivyo hii mipango, Sera na Utafiti niangalie vile vile na upande wake na kuweza kuzingatia kutokana hii Idara ya Kilimo tuliyonayo.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika Shirika la Utangazaji la ZBC *(Zanzibar Broadcasting Cooperation)*. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti tumefurahi kidogo kuona au na kusikia kua Zanzibar sasa hivi tayari inatoka katika mtindo wa *analog* na kwenda katika *digital* jambo la kufurahisha. Chamsingi katika suala hili Mhe. Mwenyekiti, hii kamati isisitize kwamba ni lazima wananchi wetu waeleweshwe kinachoendelea katika nchi. Tusijue sisi wawakilishi tu tuliokuwemo ndani kwamba kuna *system* mpya ambayo imejitokeza kutoka kwenye *analog* kuingia katika *digital* ni wajibu wetu na Kamati hii kuingilia kati kuona kwamba hali hii inakwenda na inakua nzuri na watu wanafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha zamani kilichopita suala zima la utangazaji wa habari au utoaji wa habari ulikua ni hafifu na ulikua ni mbaya sana. Tunategemea baada ya kua wao wamepata zana za kutosha wataweza kutuhakikishia kwamba watu wote Unguja na Pemba wanapata taarifa nzuri za matangazo. Kwa hivyo ningeona tu vile vile katika kamati hii iweze kulishughulikia hili suala kwamba utaratibu wa kuona hali halisi ya watu wa Pemba na watu wa Unguja wanafaidika katika mtindo mpya wa *digital*.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika Idara ya Habari na Maelezo, usambazaji wa habari ambao nausemea mimi hapa ni ule ambao utaleta faida ndani yake. Suala hili ambalo nalizungumza sasa hivi limeachwa kwa muda mrefu na wananchi hawafaidiki. Miaka ya nyuma iliyopita kulikua na utaratibu mzuri sehemu zote hususan mashamba ambapo watu wamekaa hawana la kufanya labda baada ya kucheza bao hawana shughuli nyengine. Kwa hivyo wizara hii ni lazima ikae isimamie kuona hali halisi kwamba wananchi wanafaidika kwa matumizi ya gari ambazo zinaweza kupita katika mashamba yote.

Suala ili limekatishwa muda mrefu, gari hazipiti tena za sinema kuonesha mambo kadhaa wakadhaa. Mimi ningeliiomba wizara hii pamoja na Kamati yake ambayo inaendelea, itilie mkazo na iweze kusimamia kwamba huu usambazaji wa habari uwe angalau unapita vijijini. Katika hayo iweze angalau kuona mambo muhimu kabisa. Kwa mfano mambo ya utapia mlo ni suala muhimu kwa watoto wetu. Ioneshwe hali halisi namna gani watoto wetu wanavyoingia katika mazingira ambayo yaliyokua sio mazuri ya utapia mlo. Vile vile sinema zetu hizi ziweze kuonesha hali halisi za Wazanzibari kutokana na maradhi ambayo waliyonayo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, hatari ya kua *pressure*. *Pressure* katika nchi hii imekua kubwa sana. Tumeona hivi karibuni wenyewe tumeshuhudia kwamba miongoni mwetu *pressure* imekua kubwa sana. Hatujulikani *pressure* hii ni *politically* au ni *pressure* ambayo mtu inampata kwa njia nyengine. Lakini baada ya kupima vielelezo vimetuonesha kwamba hali ya *pressure* Zanzibar ni sehemu kubwa ya watu wetu. Mambo kama haya yanataka yapelekwe shamba wakaelezwe athari ya kua na *pressure* kwa nini tuwe na *pressure*, mambo gani ambayo yanafanya tuwe na *pressure*.

Jambo jengine vile vile ni katika kuwaeleza wananchi ni maradhi ya kisukari. Haya ni maradhi mengi yaliyojaa katika nchi hii. Kwa hivyo wizara hii ya habari ijitahidi sana katika kutoa taarifa hizi kwa wananchi kwamba sehemu kubwa ya Wazanzibari hivi sasa hivi kuna maradhi ya kisukari. Tuwaeleze wananchi wetu nini sababu ya kuwa na maradhi haya na vipi kujikinga na maradhi ya kisukari. Sukari tunaitumia *hundred of bags* tunakula sukari, ma- *chemical* tuliyonayo ya ma - *juice* ambayo yamesambaa katika maduka yamejaa tele, yanachangia sukari nyingi sana, kwa hivyo mfumo wa damu unakua ni mbaya.

Masamli ambayo tunayatumia katika maduka yetu ni masamli *vegetable* "D" ambayo yanafanya mishipa yetu ya damu i-*clot* kwa sababu ya samli mbaya ambayo tunayoitumia. Haya ni mambo ya kuweza kuwaelimisha wananchi ili wajue hatari zilizotukabili.

Mhe. Mwenyekiti, tuone vile vile kwamba faida tuwambie wananchi faida ya kula matunda. Kwa nini tule matunda, tuwaelimishe wananchi wetu, sinema zifike, filamu zitolewe wananchi wetu waweze kuona faida ya kula matunda. Kwa sababu kuna *carbohydrates* unakula wali, unakula mihogo, haitoshi yote ni *carbohydrate* inakupa nguvu ya muda tu. lakini kuna vitu ambavyo ni muhimu unatakiwa kwa mujibu wa *balance diet* matunda upate, kama ndizi kidogo, mboga mboga, machungwa n.k. Watu wetu vitu hivi hawatumii ili kupunguza maradhi katika nchi hii, tunawajibu wa kuwapitia wananchi wetu kuwaelimisha kwamba haya ni mambo ya muhimu, matunda pamoja na mboga mboga liwe ni jambo la msisitizo kwa nchi nzima.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka niende katika hili shirika la magazeti. *Ahamdulillah* magazeti Zanzibar Leo yapo, lakini kwa mujibu wa takwimu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakisha dakika tatu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mheshimiwa kuna jambo moja ambalo nataka nilizungumze ni muhimu sana hayo mengine nitayakata.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la utalii, katika utalii hapa kuna mambo ambayo yanadumaza maendeleo ya wananchi. Mimi katika jimbo langu la Konde kuna barabara ambayo inapita katika msitu wa Ngezi. Msitu huu mpaka sasa hivi umeshindwa kuweza kuwanyima kazi barabara iliyomo. Barabara ya katika msitu ni barabara ya mawasiliano lakini mpaka leo kutokana na udhaifu wa barabara maji, tope na mashimo makubwa imeshindikana Wizara ya Mawasiliano kuitengeneza barabara hii.

Barabara hii huko mbele baada ya msitu huo kuna majengo ya watalii na tumekubaliana kwamba watalii mambo matatu ni lazima wapate, wapate maji, barabara na wapate na umeme. Lakini hali ya barabara kupitia msitu huu ni mbaya. Mimi nataka niseme leo hapa moja kwa moja na nitatoa ushauri wangu.

Kutokana na mazingira ya Wizara ya Kilimo imekataa kutengeneza barabara hii ya msituni kwa hali yoyote, hawataki kifusi kingie, hawataki lami itiwe hawataki lolote wamevinjari. Iliwahi kutokezea mara moja kutaka

kuziba angalau mashimo ikabidi wakawambia mkiendelea tutawapeleka mahakamani. Kwa hivyo Idara au Wizara na Wizara zimegongana na mwisho wameshindwa kuyaitimiza ahadi hiyo kwa wananchi. Wananchi wanapiga kelele, watalii wanapiga kelele, magari yao yanapata shida, lakini barabara imeshindwa kujengwa.

Ushauri wangu nautoa kwa hapa, mimi hili suala ikiwa wizara mbili zimeshindwa kutengeneza barabara hii, mimi suala hili nalipeleka moja kwa moja na ulipokee mwenyekiti ulipeleke kwa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar aweze kuliingilia kati, suala hili. Kwa sababu inaonesha Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mawasiliano imeshindwa hili ni suala la watalii, mbele kuna watalii, je, tunawafanya nini watalii. Kwa hivyo suala hili nalipeleka kwa Makamo wa Pili wa Rais aweze kulishughulikia na aweze kulitolea suluhisho zima la masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na wakati ambao unanitazama nina mengi ambayo nilikua nataka niyazungumze lakini naheshimu wakati wako. Ahsante sana nakushukuru na mimi naunga mkono yote haya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa ufupi juu ya hoja hii ya kamati ya Mifugo, Habari na Utalii, ambayo imewasilishwa mapema asubuhi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na wajumbe wake kwa kazi kubwa waliyoifainya na kuweza kutuletea ripoti hii ambayo mimi naiona ni makini na kwa kweli itaweza kutusaidia iwapo serikali watakusudia kuifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana waziri wawili waliobadilisha nafasi, mmoja kuacha uvuvi akenda habari na mmoja kuacha habari akenda uvuvi. Nadhani kila mmoja atakua amejifunza kutokana na alipotoka na sasa anaanza nyumba mpya. Nasema hivyo kwa sababu kipindi cha mwaka mmoja kuiongoza wizara ni kidogo na bila shaka wanahitaji kujifunza zaidi. Lakini kwa sababu ya umakini wao nadhani tuwaamini na kazi itafanyika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwenye suala zima la Shirika la Utangazaji na nianze kwenye urushaji wa matangazo. Nataka niseme tu kwamba mwaka jana Mhe. Waziri alijifunza kwamba wajumbe wote hawakuridhika na jinsi Wananchi wa Zanzibar na hasa Pemba wanavyokosa huduma ya matangazo na hasa televishen. Zikatoka ahadi nyingi, miezi mingi ikatajwa na sasa imepita bila ya mafanikio, kibusara, kistaarabu nadhani tumejifunza.

Mhe. Mwenyekiti, haki ya habari ni haki moja ya msingi kwenye katiba ya Zanzibar na kwenye maazimio na misimamo ya kimataifa. Katika zama hizi si busara kabisa kuwaachia wananchi wakaendelea kukosa habari kwa sababu eti ya ukosefu wa fedha. Mhe. Said mimi namuamini sana ameanza kwa ari mpya na kasi mpya kwenye uvuvi namuomba sana aanze kwa ari ile ile na kasi kubwa zaidi kwenye Wizara ya Habari, ili hatimaye pengine ndani ya bajeti hii inayokuja keshokutwa Wazanzibari wote popote walipo waanze kupata taarifa hizi kupitia redio na televishen zao.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibar wanahitaji sana kupata habari kupitia televishen. Shirika letu hili la utangazaji kwa kweli limekua ni tegemeo la Wazanzibar. Zanzibar hapa hatuna TV nyengine ila ni Televishen Zanzibar ambayo ndiyo mrithi wetu ni televisheni kongwe ya asili ambayo tumeambiwa ndiyo ya mwanzo kwenye ukanda huu ya Afrika Mashariki.

Kwa msingi huo Mhe. Mwenyekiti, kuna haja ya kujipinda kila hali na kuna changamoto ambayo ameipata naomba sana kabla ya kufika wakati wa bajeti basi ajitahidi na Mwenyezi Mungu amuwezesha ili tufanikiwe suala hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mbali na suala la TV kwa muda mrefu sasa tumekuwa na ukosefu wa matangazo ya redio katika masafa ya *shot wave* (SW) na *medium wave,* (MV) naomba Mhe. Waziri akija atusaidie kwamba tumesibiwa na nini. Wazanzibari kwa muda mrefu tumekuwa hatufaidiki sana na matangazo ya *shot wave* na *medium wave* na badala yake tunafaidika kidogo na matangazo ya (*FM*) sasa Mhe. Waziri atwambie labda tumesibiwa na nini ili sisi kama Wawakilishi tuweze kumsaidia ili Wazanzibari kupitia redio yetu tuweze kupata haki hii ya habari kupitia chombo hiki cha redio.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la uimarishaji wa vifaa kwenye ripoti hii, Mwenyekiti wa Kamati ametwambia kwamba vifaa aina ya UPS zimenunuliwa vine (4), vifaa hivi tumeambiwa kwamba vipo na vinafanya kazi, lakini baada ya kufanya utafiti mdogo tumeona kwamba kifaa hichi ya UPS vipo katika kituo

cha Mkanjuni Chake Chake, kipo katika kituo cha Mkoani na kipo katika kituo cha hapa Unguja eneo la Masingini, nimejaribu kutafuta cha nne kipo wapi. Mhe. Waziri labda unambie hii UPS ya nne imepotea wapi. Isijekua ni miongoni mwa vile vifaa vilivyopotea pale baharini Mkoani baada ya kuzama meli.

Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji wafanyakazi wetu wafanyiwe haki. Haki ya Wafanyakazi ni kupatiwa vifaa vya kutendea kazi na maslahi yake. Hivi leo mimi nna wasi wasi kabisa kwamba kama kutakuwa na *function* mbili sambamba, kama tutakua na Baraza la Wawakilishi, baadaye tukawa na Mhe. Rais au Makamo wa Rais anahutubia, anahitaji matangazo ya moja kwa moja ya TV lazima *function* moja itakwama kwa sababu ya tabia ya mfumo wetu wa umeme wa kukatika katika mara kwa mara. Kifaa hichi ya UPS ndicho ambacho kinaweza kusaidia pale ambapo umeme utakatika katika ili kuwawezesha watu wetu hawa kuweza kuweka matangazo ya TV *live*.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni kama changamoto Mhe. Mwenyekiti, nadhani sio suala la kufanya masihara, lazima kifaa hichi cha UPS wapewe wataalamu wetu hawa ambao wana mitambo ya kurushia matangazo live ya *television* ili kila wakati na popote pale waweze kufanya kazi hii kwa maslahi na ustawi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimwambie Mhe. Waziri mimi namwamini sana tumeanza naye mbali, alikua mjumbe wa PAC historia tunaijua amekua Waziri kwa mwaka mmoja sasa watu wanakula samaki wazuri tu wa kufuga na leo Waziri wa Habari, namuomba sana kifaa hiki cha matangazo UPS hasa kwa mitambo yetu ya *television* ambao tutaitumia kwa *program* ya *live* basi kiweze kupatikana ili mafundi wetu wawe nacho mkononi wakati wowote.

Tabia hii ya uzimakaji wa umeme kuna siku utatuathiri na tutakosa matangazo. Bahati mbaya matangazo tukiyakosa ikiwa kuna *function* ya Rais atakayeonewa ni yule mfanyakazi ambaye si kosa Lake. Tuwawezeshe wafanyakazi wetu, tuwawezeshe wataalamu wetu ili tuwalaumu kwa kosa, tusiwalaumu kwa uzembe wa serikali.
Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo katu na kamwe sitolivumilia ni maslahi ya wafanyakazi. Jambo hili tena iwe basi, watu wazima wakiambiwa iwe basi. Haiwezekani kuwatumia wafanyakazi wetu usiku na mchana bila ya kuwapa haki zao za maposho. Mwaka jana tumegombana na Mhe. Waziri aliyepita na mara hii hapa patakuja kuwa hapatoshi tukijaaliwa. Kila mfanyakazi ambaye haki yake hajapewa tuwapeni. Ni mwakilishi gani hapa anayefanya kazi bila ya kupewa haki yake. Sasa ikiwa mwakilishi hawezi kuvumilia seuze mtoto wa mwakilishi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri tuwapeni wafanyakazi wetu maposho yote ya kikao. Kuna tarifa kwamba kuna kikao tangu cha Oktoba hawajapewa haki yao. Huu si ustaarabu, huu si uwadilifu na hii sio nidhamu ya kazi. Wizara ya Utumishi wa Umma imejitahidi kujipanga, mishahara wanapata lakini kuna stahiki zao ambazo tumekubaliana kwamba wazipate kila baada ya kikao.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, posho la vikao, posho la nguo, posho la *over time* na maposho mengine ya safari tafadhali sana Mhe. Waziri nakuomba tuwapatie. Haki nyengine Mhe. Waziri nakuomba sana katika busara zako, ndugu zetu hawa walikwenda Uholanzi mwaka juzi, wakaikopesha serikali fedha. Maana yake fedha za Uholanzi walikua wapewe na serikali, wakaambiwa kwamba wajihudumie ili baadaye serikali itawasaidia. Kwa nini hatuwalipi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza kuna watu tayari wamestaafu, kuna watu tayari wamefariki dunia si utaratibu mzuri kwamba leo watu wanafariki dunia tena kwa muda mrefu hatujawapa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa *Alhaj* Said Ali Mbarouk, nakuomba sana haki hii ya mayatima wapelekee wenyewe. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli itakua si busara hatufanyi haki. Hapa tutasema kwamba kwa nini tufikirie jengine kuliko hizi haki, kwa nini tufikirie safari kuliko hizi haki, hebu tujibane. Mwezi mzima tusisafiri ndani ya wizara nzima lakini haki hii ya mayatima wapewe wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, haipendezi ndugu zetu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Leo hii si vizuri lakini ni lazima tuseme kwamba kuna wafanyakazi wamepelekwa Masingini na leo mnataka kuwapele Bungi hawana usafiri. Tuwafikirie, mfanyakazi mwanamke unampeleka Bungi, mwanamke unampeleka Masingini mpaka saa 6:00 arejee wapi na muda gani nyumbani kwake. Nani anayekubali mkewe akakae Masingini mpaka saa 7:00 bila ya usafiri, mimi binafsi sikubali katika hilo na ni lazima tuwapatie usafiri ili wakati wa kumaliza kazi zao warejee nyumbani kwa salama na amani tusiwasumbue. Hali hii Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tuseme kwamba wafanyakazi wetu wana nidhamu ya utiifu, wanafanya kazi kwa bidii lakini tunawavunja moyo na wakiacha kazi kwa kweli sisi tutakua tumechangia.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri ajitahidi atafute japo pahala akope maana uwezo wa serikali ni mdogo, lakini ukope gari ili tuwapatie watu wetu wanaokwenda kazini usiku hasa katika vituo vya Masingini na Bungi kwa ajili ya kurejea nyumbani. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba haipendezi kwani nchi imeharibika, nchi imekua na kila mtu ana nia yake, kuna siku Mwenyezi Mungu atunusuru hawa wakipata hasara itakua ni nani alaumiwe. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi naamini ni msikivu na akope hata humu Barazani wamo wafanyabiashara akope ili apate gari mbili ili tuwape wafanyakazi wetu utalipa baadae.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningelizungumzia ni suala zima la Shirika la Magazeti na nilipongeze kabisa shirika hili kwa kuendelea kutoa huduma nzuri na za kisasa kadri ya uwezo wao. Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo hasa Mhe. Waziri nimuombe sana kwamba undelee kujenga hoja Wizara ya Fedha ili wenzetu hawa wapatiwe fedha za kutosha kwa ajili ya kuendelea na kutoa habari kupitia gazeti lao za Zanzibar Leo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Wazanzibari wanatumia magazeti kinyume na siku za nyuma ambazo gazeti lilikua halina maana, lakini hivi leo gazeti limekua mali. Kwa hivyo, fedha ambazo wanatumia kuchapisha mitambo hii, basi Mhe. Mwenyekiti, tuongezewe ili shirika hili liweze kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo ningeizungumza ni suala zima la utalii, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani niwalani wale wote ambao wanachukua fursa zao, uwezo wao kuwadhalilisha Wazanzibari kwa sababu ya utalii. Mhe. Mwenyekiti, hii ndio nchi yetu mtu alipozaliwa mara nyingi hutarajia atakufa hapo hapo. Kwa hivyo, utalii usiwe sababu ya kuwanyanyasa na kuwadhalilisha watoto wetu, kama kuna mtu amefanya kosa basi aadhibiwe kwa kosa alilolifanya, lakini kama hakuna kosa basi lazima Wazanzibari walindwe kwa mujibu wa ustawi wao na utamaduni wao. Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo basi Mhe. Waziri nikuombe sana sheria imepita juzi, basi tuweke kanuni ambazo zitawalinda na kuwasaidia Wazanzibari kwanza, Mzanzibari kwanza ndio baadae utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni zikiwa nzuri Mhe. Waziri lazima kile kilio cha Wazanzibari ni kupatiwa kazi kwa wingi itaondoka na tatizo la kunyanyaswa Wazanzibari litaondoka. Kwa hivyo, nikuombe sana utumie busara yako chini ya serikali yetu uweke kanuni ambazo Wazanzibari zitawalinda kwanza kwa maana ya kuongeza nafasi za ajira na kulinda utamaduni na silka zetu za Wazanzibari. Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala zima la Chuo cha Maendeleo ya Utalii, niendelee kuwapongeza tu ingawa wanaendelea kukabiliana na changamoto ya fedha, lakini Mhe. Waziri asisahau kwamba tuko katika utandawazi na tuko katika ushindani wa soko la ajira katika sekta ya utalii. Kwa hivyo, tusifikirie tu kwamba vile walivyo ndio wataingia katika ushindani wa Soko la Afrika Mashariki kwenye utalii, au wataingia katika Soko la Dunia. Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwawezeshe kifedha ili waweze kutafuta walimu wazuri na waweze kuwaandaa vijana wetu katika masuala haya. Mhe. Mwenyekiti, niseme kabisa kua lazima tusiwe na woga, ni kwamba tuandae mazingira ambayo ajira pamoja na kwamba hatuwezi kuwazuia wageni kwa sababu utandawazi na makubaliano ya kimataifa, lakini Wazanzibari wapewe kipaumbele kwanza ndio baadae apewe mtu mwengine. Mhe. Mwenyekiti, ziko nchi soko la ndani la ajira hulindwa kwa kupewa kipaumbele wananchi wazalendo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningelizungumzia kuhusu hapa ni suala zima la takwimu. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 129 kifungu cha 18 kamati imezungumza kwamba Kamisheni ya Utalii haina takwimu za wageni, na kumbe vile mkitwambia laki moja au laki mbili kumbe sio sahihi. Kwa hivyo, pale ambapo tutakosa takwimu maana yake tutakosa mapato, Mhe. Waziri nikuombe kabisa kwamba tuandae utaratibu tuwawezeshe wenzetu hawa waweze kufanya takwimu sahihi za wageni wetu, takwimu hizi zitatusaidia kupata mapato. Kwa sababu kila mgeni ni mapato, hivyo hivyo tuwe na utaratibu mzuri wa kuweka takwimu ya wale *tourists* tuwajue ni wangapi, tuache ule mtindo wa kuwakaribisha wageni hapa kuja kuweka kinyesi tu, ni lazima tupate maslahi kwa ajili ya Wazanzibari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningezungumza, mwaka 1996 kule Shamiani Mwambe tulibahatika kujengewa hoteli ya mwanzo ya kitalii, ingawa baada ya miaka 4 ile hoteli haikumalizika kuna taarifa kwamba jamaa alifilisika. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri unambie eneo lile sasa liko kwa nani ili wale wajanja wapenzi wa ardhi wasije wakalichukua lile eneo bila ya maslahi ya nchi. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, pale kuna boti ya kisasa nzuri inakufa ndani ya macho na masikio ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anambie boti ile kwa nini inakufa, na kwa nini haina mwenyewe. Boti ambayo ingechukuliwa basi tungewawezesha vikosi vyetu vya KMKM kuifanyia kazi. Kwa hivyo, kama haina mwenyewe basi mutwambie ili watu wa Mwambe waiuze waweze kupata pesa, kwani hatuwezi kuacha mali ile inakufa pale chini ya mikono ya serikali, chini ya macho ya viongozi wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala zima la ushauri wa kamati kifungu hiki cha 23 kwamba kuna haja ya hoteli ya Wete, Mkoani na Chake Chake kurejeshwa kwenye mikono ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, hoteli hizi zimepewa kampuni muda mrefu na hakuna faida yoyote. Kwa hivyo, mimi nadhani kuna haja ya serikali sasa kutwambia kwa nini wanaendelea kung'aninia *National Marketing* na huyo ni nani na wazirejeshe hoteli hizi mikononi mwa serikali tukajenga uchumi wetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani kabisa kwamba tumeshindwa, juzi hapa tumeambiwa Bwawani kama hatuna uwezo, uwezo hauji tu kama radhi lazima tujipange, tuekeze na tuamue. Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba Bwawani, Mkoani, Chake Chake na Wete uwezo tunao wa kuziendeleza lakini kwa nini hatufanyi hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, niache eneo hilo la utalii niende kwenye ajira. Mhe. Mwenyekiti, asubuhi Mhe. Jussa hapa amezungumza kwamba kuna wafanyakazi mbali mbali hasa wa Kampuni ya Zantel, Zantel ambayo sisi ni m-bia kama sikosei tuna asilimia 18. Lakini wafanyakazi wetu wanateswa wanafanyakazi huu ni mwaka wa 9 hawana mkataba. Mhe. Mwenyekiti, huo sio utaratibu sheria ya kazi haikubaliani na hilo na lazima tuwasaidie.

Mhe. Mwenyekiti, tumefanya utafiti kwamba wale wenye mkataba wapo ambao wanapata mpaka laki saba, ambaye hana mkataba anapata shilingi laki moja na ishirini. Mhe. Mwenyekiti, huu sio utaratibu kabisa kwa hiyo Waziri sasa hivi hayupo pengine amesafiri, lakini akija aambiwe kwamba lazima tupatiwe utaratibu wa mikataba wafanyakazi wetu hapa Zanzibar, tuache tabia ya kuwanyanyasa wafanyakazi wetu hili ndio tegemeo letu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nimuombe Mhe. Waziri wa Uvuvi (Mhe. Abdilahi Jihadi Hassan) basi aanze pale Mhe. Said Ali Mbarouk alipofikia kwenye suala zima la uvuvi hasa ufugaji wa samaki kwa Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Ali Mbarouk bila ya kificho amefanya kazi ya ziada, amefanya kazi nzuri na leo wavuvi wote wa Zanzibar wamejenga mategemeo. Nina imani kwamba Mhe. Jihadi ataendelea na juhudi ile na bila shaka mafanikio yatapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nimuombe sana Mhe. Said Ali Mbarouk chonde chonde maposho ya wafanyakazi yapatikane, vyenginevyo Julai hapatatosha hapa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie ripoti hii kama ilivyoletwa asubuhi hii na Mwenyekiti wa Kamati hii. Kwanza nipongeze kwa kazi kubwa ambayo wamefanya kwa kweli ni kazi nzito na ngumu, lakini kwa sababu ni wajibu wao wamefanya kazi hii na leo wameiwasilisha hapa kwetu. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niende kama walivyoanza wenzangu asubuhi japo sitokwenda kwa wizara zote ambazo wamezifanyia kazi. Mhe. Mwenyekiti, kamati hii imefanyia kazi wizara tatu ambayo ni Wizara ya Habari na Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Wizara ya Uvuvi. Kwanza nianze na kuchambua angalau taasisi mbili tatu kwenye Wizara ya Habari, nikisema kwamba Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni muhimu kwani tunapata habari mbali mbali za ulimwengu huu nikianza na Shirika letu ambalo sasa hivi ni *ZBC* lina wafanyakazi ambao wanafanyakazi kwa juhudi kubwa. Mhe. Mwenyekiti, leo hapa tunaonekana kwenye maeneo mbali mbali ni kwa sababu ya jitihada zao ambazo wanazifanya kwa kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tuwatizame wafanyakazi hawa ni vipi tunawawezesha Mhe. Jussa asubuhi alisema kwamba ni lazima tuwe tunawatunza kwa sababu wao ni watu ambao ni kama wanaonekana kila mara kwenye vioo, ni vizuri tuwatunze na waende na ile kazi yao ambayo wanaifanya. Kwa kweli tunawaona vijana wetu kama hapa Barazani wapo wanashirikiana na sisi tunakua nao muda mrefu mpaka tunaondoka hapa.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba bado wanakumbana na changamoto nyingi, kwanza zikiwemo zile za usafiri hawana uhakika wa usafiri wanapoondoka hapa, basi hata zile kurugenzi ambazo zinazoendesha mambo haya kwa nini wasiwasaidie hawa vijana wetu ambao wanakuwepo hapa kwa muda mrefu. Nikisema kwamba habari inajumuisha magazeti pamoja na idara lakini kuna idara moja sikuiona hapa. Vile vile ni kwamba kamati hii imeeleza mafanikio mengi ambayo yameonekana katika taasisi hizi na vile vile waliziona changamoto nyingi ambazo ziko katika taasisi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba kuna gazeti letu la Zanzibar Leo ambalo unalisikia kila leo kwenye televisheni ya *TBC* huwa linachambuliwa kila siku. Kwa hivyo, hili ni jambo la kulishukuru kwamba gazeti letu sasa linasomeka na ni gazeti zuri kwa vile lilivyopambwa na sasa hivi wanatoa zile nakala ambazo zina rangi kwani huko mwanzo lilikua halina rangi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka Wizara ya Habari kwani ina mambo mengi ikiwemo utamaduni ndani yake kwani utamaduni ni lazima tuwe nao hakuna nchi iliyokua haina utamaduni wake, pia ni lazima kila mtu ajue

utamaduni wake. Kwa hivyo, ni lazima tutilie mkazo wa kuwafundisha watoto wetu utamaduni wetu ili waweze kuujua na kila tukiendelea kwa sababu maadili kutokana na utandawazi huu tulionao hua unapoteza sana silka zetu na mila zetu. Kwa hivyo, mimi naomba taasisi hii iwe inachukua jukumu kubwa la kuwaelimisha na kutoa taarifa mbali mbali kuhusu utamaduni wetu wa Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye idara ya utamaduni ilikua inabeba taasisi mbali mbali ikiwemo Makumbusho, lakini kadri tunavyokwenda tunaziona hizi idara nyengine zinakwenda kwenye wizara mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Idara ya Makumbusho kwa kweli tunahistoria nyingi ambazo zilikua zituingizie vipato vingi kwa hapa Zanzibar kwani Zanzibar yetu ni ndogo, niseme kwamba ule umasikini tusingekua nao. Lakini sijui kwa nini tunazo sehemu za historia kama pale Mangapwani ile ni sehemu nzuri mimi mwenyewe nilikwenda nikaona mambo yake pale. Lakini nafikiria tukenda kwa wenyeji zaidi tunaweza tukazipata sehemu zile, nimekwenda mpaka kwenye shimo ambalo wanasema ilikua ni makaazi ya watu. Mhe. Mwenyekiti, tukenda pale kwa sheha au wale wenyeji wa pale wanaweza kutuonesha maeneo mengi zaidi.

Lakini ukitizama ni kwamba yametupwa, unakwenda pale unakuta ni msitu tu ina maana hizi taasisi na hasa za utalii nafikiri ziwe zina-*negotiate* mambo baina ya sekta hii ya utalii pamoja na sekta ya habari na ya mambo ya kale, ziende ziangalie yale maeneo utasema yametupwa kabisa ni aibu hata kumpeleka mgeni kwenda pale kuona. Kwa kweli tungeweka maeneo kama yale tukayapa kipaumbele na tukawa na *strategic* ambayo tunasema sasa ni lazima kwa sababu utalii ni uti wa mgongo wa taifa letu hili.

Kwa hivyo, ni lazima maeneo yale tuwatafute wawekezaji au zaidi sisi wenyewe serikali ikawekeza pale hata kujenga vyuo vya utamaduni vikawekwa ili yale mazingira angalau yawe yanavutia, lakini unakwenda pale njia zenyewe hazitabiriki, hazionekani, unakwenda unampeleka mgeni anaona pori kabisa. Kwa hivyo, kama kweli tunataka kuukuza utalii au kama tunaona kwamba Sekta hii ya Utalii inatusaidia basi ni lazima serikali iandae *strategic* na hizi idara ambazo zinashughulikia aidha ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na sekta zote za habari ziende zione namna gani.

tuna mali nyingi, tuna utamaduni mwingi, tuna historia ya hapo kale ni nzuri, ni lazima vitu hivi tuvihifadhi na tuvione ubora wake na tuone kua ni uti wa mgongo wa taifa letu.

Nikienda kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Idara hii kwa kweli ni *pillar*, katika kila wizara unakuta idara hii ipo na hii ndio idara yenyewe ambayo hata yeye mwenyewe waziri maslahi yake yanakuweko kwenye idara hii. Kwa hivyo, ni lazima iwe kila mmoja anawajibika katika kutekeleza kazi yake vizuri na hii ndio inayosimamia idara nyengine zote. Najua mikakati wanayo na bila shaka kunakua na *briefing* mbali mbali lakini sasa ni lazima tubadilike. Kwa sababu Rais wetu keshatwambia tubadilike isiwe *business as usually*, kwa hivyo ni lazima sisi tuwe kila mmoja anawajibika kiupande wake ili tuone namna gani sasa tunataka tujikomboe na kwa uwezo wa *Allah* penye nia pana njia, ni lazima tushikamane kwa pamoja ili tuone nchi yetu tunatokana na umasikini wa kila kitu. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba niende na Wizara ya Uvuvi. Wizara hii vile vile ni sekta muhimu sana ambayo sisi kama wanadamu tunahitaji lishe bora na bila ya lishe bora basi tutapata utapiamlo. Kama hatukupata chakula kizuri tukapata *protein* kwa wingi, tukapata vile ku-*balance diet* tusile tu kwa kusema kwamba tuishi, lazima tu-*balance diet*.

Jana tulikua na madaktari hapa ambao wamekuja kutupima afya zetu. Kwa hivyo ni lazima tubadilike hata yale malaji kama tulivyoambiwa na madaktari wetu, tunakula nje ya ule utaratibu tuliowekewa tunajilia tu. Kwa hivyo, ni lazima kwenye Sekta hii ya Uvuvi na tunaambiwa siku zote hizi *red meat* ni mbaya ni lazima tule *white meat* ambazo ni samaki pamoja na kuku. Kwa hivyo, ni lazima serikali ichukue jukumu hili.

Zamani palikua na utaratibu sijui umeendea wapi, mimi husema kwamba tunaaza mambo mazuri lakini halafu yanatufia. Zamani kulikua kuna mabanda ambayo serikali yenyewe inauza madagaa lakini sijui utaratibu ule ulikwendea wapi. Hivyo serikali nayo isiwatafute tu wawekezaji halafu yenyewe ikajiweka kando, inatakiwa kama tunawekeza kwenye mambo ya usafiri basi na serikali nayo japo mkono wake uwepo. Kwa sababu kuna wananchi ambao hawana uwezo wanaitegemea serikali, mwekezaji atafanya yeye kama ni biashara lakini serikali iwe inawatizama wananchi wake wale ambao wana hali za chini. Sasa hili nalizungumza kwenye sekta hii ya uvuvi kwamba serikali isijitoe kabisa kwa sehemu mbali mbali lazima iwe inaweka mkono wake isiachilie kabisa kwa kusema kwamba ni kwa wawekezaji.

Mhe. Mwenyikiti, kwa hayo machache nashukuru na nasema ahsante sana na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani walionichagua nasema naunga mkono ripoti hii na nawapongeza sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi magharibi haya kunipatia fursa ya kusema machache kuhusiana na ripoti ya wenzetu waliojituma kwa muda wa kiasi cha miezi tisa. Nashukuru kwamba nimepata kujua mengi kutokana na ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kule ambako Mhe. Hija Hassan Hija ameanzia kwenye Televisheni. Ni muda mrefu sasa tuna kilio hiki cha televisheni na waziri tumeshapata mabadiliko, wa kwanza alikua anatwambia kwamba tunaingia katika mfumo mwengine wa *digital*, kwa hivyo, tutachelewa kwa sababu hiyo. Nashukuru kwamba mitambo ilifika na imefungwa Pemba lakini matangazo bado hatujayapata, ukiulizia unaambiwa kwamba kuna kifaa kilizama baharini, sasa sijui kifaa hicho kinafika shilingi milioni ngapi ya kua mpaka leo muda wa mwaka toka kuzama kwa kifaa hicho bado tunashindwa kupata matangazo. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akatupa uhakika hivyo ni lini hasa kwa sababu mimi naona choyo, nikienda Chake Chake nakuta matangazo nayaona lakini nikija Mkoani matangazo hakuna. Sasa mimi wasiwasi wangu labda sio kifaa kilichosababisha kwamba wengine wasipate matangazo labda ni uwezo wa mitambo uko mdogo ndio uliosababisha hayo. Sasa ili wananchi wapate kujiandaa kujua ukweli wa jambo hili wangepata kujua uhakika je, hivyo kweli hio Disemba tutapata au ni danadana tu, wengine labda wanaweza wakajiandaa kwa kutafuta *satelite dish* zao wenyewe wakaweza kukamata matangazo. Sasa ukweli utawasaidia kujua tufanye nini na kwa wakati gani. Sasa ningemuomba waziri hili akalishughulikia.

Lakini jengine ni kwamba hivi sasa tunasema tuna shirika tunaliita *ZBC* ambalo tumeshapata *digital* tayari. Lakini mimi wasiwasi wangu ni kwamba tumehama tu kubadilisha maneno kwamba tumetoka TVZ tunaingia *ZBC* lakini utendaji wake ni ule ule hakuna mabadiliko yoyote kwamba labda mfumo wa ulimwengu tu umetubadilisha kua tuondoke kwenye *analog* tuingie kwenye *digital*, lakini utendaji wake na mabadiliko yake ya *ZBC* hakuna.

Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia unaweza ukatoa kasoro nyingi katika Shirika letu hili, ukienda hata kwa hawa watangazaji kwa sababu tumeingia katika *digital* bila shaka wenzetu watakua wanatutizama Afrika Mashariki na pengine Afrika kwa jumla, lakini watangazaji wetu bado hawajawa na kiwango. Unaweza ukakuta wengi wanadodosa katika kutaja aidha viongozi wakuu katika nchi tofauti au hata majina ya nchi tofauti.

Lakini jengine ni kwamba televisheni hua zinatumika kwa matukio tofauti kuna matukio pengine kufungwa kwa barabara katika mtaa fulani au kutokea kwa tukio fulani, sitaki niliseme lakini hata tukio lililotokea la kuzama kwa meli labda tungelikua tuna televisheni iliyo ya kileo tungelipata kuona matangazo yale moja kwa moja. Lakini mimi kinachonishangaza ni kwamba hadi hii leo televisheni yetu inakwenda kwa wakati maalum unakuta pengine kuanzia saa sita mchana mpaka saa sita za usiku na kutoka hapo huioni tena. Sasa kama ni *digital* basi tubadilike tuwe *digital* twende na wakati.

Televisheni ya kwanza tulivyoambiwa na wanahistoria au ya pili kwa rangi kwa Afrika nzima lakini leo nashangaa kwamba sisi ni wale labda sijui wa karne ya ngapi nyuma. Kwa hivyo, kama kweli *digital* basi tuwe *digital*, matangazo ya televisheni ni muhimu wakati wote sio wakati fulani tu.

Mhe. Mwenyekiti, narukia kidogo katika Shirika la Magazeti, nalo hili ni moja katika njia ya kusambaza habari katika nchi na hivi sasa katika nchi yetu tuna gazeti moja. Mhe. Mwenyekiti, niliposoma historia nilikutia kwamba miaka labda hamsini au sabini iliyopita nyuma, nchi yetu ilikua ina magazeti yasiyopungua 10 katika miaka 1890. Karne hii tuliyonayo tunayoita sayansi na teknolojia bado sisi tuna kigazeti kimoja, na la kushangaza zaidi ni kwamba gazeti hili Mhe. Mwenyekiti, linachapishwa sio katika nchi yetu, linachapishwa nje ya nchi yetu. Kwa hivyo, miaka hiyo tulikua tuna mitambo sisi wenyewe hapa Zanzibar, tulikua tunachapisha magazeti wenyewe, lakini leo 2012 bado tunamtegemea mtu kutuchapishia magazeti yetu sijui tuna uhakika gani kwamba Zanzibar Leo kesho asubuhi tutaamka tukiwa nalo au tukiwa hatunalo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia hata hiyo *circulation* yake sijui kama wananchi walioko Pemba wanalipata asubuhi na mapema au wanalisoma kutokana na abiria aliyetoka Dar es Salaam akawapelekea kwa ile boti labda akamwambia hebu chukua na wewe ukasome. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa tunabadilika katika sekta ya habari basi tubadilike tumeshafika wakati sasa hiki kigazeti kimoja hakikidhi haja tena, tunatakiwa turejee ile miaka ya 1890 ambapo Zanzibar ilikua inajuulikana ni moja kati ya nchi iliyo na magazeti mengi kwa ukanda wa Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kidogo nakuja katika Kamisheni ya Kazi, Mhe. Hija Hassan Hija alizungumza hapa kwamba wafanyakazi wetu hawana mikataba, ni kweli kwamba wafanyakazi wetu hawana mikataba, hao wachache walioko katika hiyo Sekta ya Utalii basi wananyanyasika kwa sababu moja hii kwamba mikataba haipo wanaajiriwa kienyeji enyeji tu. Kwa hivyo, uhuru wa kumpa huyo muajiri amfukuze leo au kesho

unakuwa ni mpana zaidi. Hivyo, naiomba idara inayohusika hili iliangalie, lakini hii si kwa wageni tu, hii pia hata hawa wanaoajiri ambao ni wazalendo pia wanayo tabia kama hii.

Kuna waajiri ambao wanawachukua wafanyakazi lakini hawawapi mikataba na wakawa wakati wa kuwapa mikataba basi inakuwa mikataba ya kubabaisha, pengine miezi sita, mwezi wa saba basi umpe mkataba mwengine ili kuogopa kwamba akiingia katika labda uajiri wa aina fulani itabidi umlipe aina fulani ya mafao yake. Kwa hivyo, pia ujanja huu kwa waajiri upo. Kwa hiyonaiomba Idara ya Kazi suala hili iliangalie kwa kina zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, leo tuna Baraza la Taifa la Michezo, lakini Baraza hili limejikita zaidi katika mpira wa miguu na ninavyoona mimi tayari Baraza hili limeshashinda. Kwa sababu ni muda mrefu sasa kiwango cha mpira wetu wa miguu kimeshuka, lakini haya yote yanasaidiwa na migogoro iliyoenea au iliyojaa katika hivi vyama vinavyoshughulikia mpira wa miguu.

Ni miezi michache tu iliyopita nyuma tuliona kichekesho wakati unaandaliwa utaratibu wa kupatikana kwa Chama cha Mpira wa Miguu cha *ZFA*. Uchaguzi huo mimi niliona ni miujiza sijui walichagua vipi na la kushangaza zaidi hata huyo mwenyekiti ni juzi yeye mwenyewe ameachia ngazi sijui kwa sababu gani aling'ang'ania kule lakini leo anasema mimi sijui nimeshakuwa mtu mzima, sijui vipi kaondoka. Kwa hivyo haya yote yanachangia katika hili.

Lakini zaidi tusiangalie mpira wa miguu tu, kuna vijana ambao wamekwenda kushiriki katika mashindano ya *Olympic* ya walemavu hawakusaidiwa vijana hawa na wamerudi mmoja wao amefanikiwa kupata medali ya dhahabu hata taarifa hatuna. Nasikia kwamba ameitwa kijana huyu na anapewa ile posho yake kwa awamu, njoo leo nakupa hiki, subiri kidogo tutakupa hiki, huo ndio mtindo wetu. Kwa hivyo, mimi ningependa hili Baraza la Michezo likajipanga vizuri, kama ni kushughulikia michezo tukashughulikia.

Madaktari wetu juzi walitwambia kuwa moja katika kuondoa matatizo ya miili yetu basi tunatakiwa tufanye mazoezi. Kwa hivyo, Baraza nalo lingehamasisha watu wakaingia katika utamaduni huu.

Mhe. Mwenyekiti, narukia kidogo katika Baraza la Kiswahili. Huko nyuma wakati wa enzi za Dr. Salmin Amour na mimi nilibahatika kuwa ni mjumbe wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar, lakini toka siku niliyopata uteuzi sikuwahi tena kuitwa hata siku moja kuambiwa leo kutakuwa na *function* fulani, baada ya siku hiyo ya uzinduzi wa Baraza ikawa ndio mwisho. Hii hivi sasa inaleta athari kubwa kwa jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa sisi tunahesabika kwamba ndio tunaomiliki Kiswahili au sisi ndio tulio na Kiswahili Sanifu. Kwa wanaotaka kusoma Kiswahili Sanifu wanakuja kwetu sisi, lakini cha kushangaza ni kwamba Baraza limekaa *very idle* halifanyi shughuli yoyote lipo na tumebakia sisi kuwa ni *recipient* tuna *receive* tu mambo kutoka au maneno yanaingia katika lugha yetu. Mimi nasikitika na mengine hata siwezi kuyataja hapa kwamba tunayakaribisha maneno yanaingia katika lugha yetu mama na baba wakiwepo motto huwezi ukalitaja neno lile.

Kuna kile kichengeo tunachochongea penseli mimi siwezi hata kukitaja, lakini tumeruhusu majina kama hayo wakati sisi tukiwa ndio tunaohesabiwa Waswahili wa mwanzo na Waswahili tuliobobea katika fani hii na Kiswahili chetu ni Sanifu kuliko nchi nyengine zote.

Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako namalizia kwa Sekta ya Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba kuna migogoro mingi katika sekta hii na la kushangaza ni kwamba raia wa nchi hii tayari wameshaanza kuwekeana mipaka huko baharini. Unaweza kukuta kwamba raia wa kijiji fulani bila ya kwa kuna sheria yoyote inayokataza raia kutoka sehemu nyengine kuja kuvua katika maeneo yale basi anaweka mpaka wake anamwambia wewe hoo! Hapa usivue. Kwa hivyo, migogoro kama hii inaweza kusababisha madhara makubwa kwa jamii yetu. Ningemuomba Mhe. Waziri haya akayaangalia kwa kina, kuna maeneo ambayo tayari yametengwa hayo yanajulikana lakini kuna maeneo ambayo hayakutengwa wananchi wanayatenga wao wenyewe kwa kuepusha tu wananchi fulani wasiingie katika eneo lile. Huu ni usumbufu kwa sababu wengi kati ya wananchi wetu wanategemea sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwa Bodi ya Sensa. Hivi sasa tuna televisheni ambazo ni *independent* vituo vya matangazo ambavyo ni huru kabisa. Hapo nyuma ilikuwa kituo chetu ni kimoja tu, sasa mimi nashangaa hii Bodi ya Sensa inafanya kazi zake vipi, wakati sisi tunapata matangazo, tunapata film, tunapata michezo kutoka sehemu tofauti ambazo ni *independent*. Sasa wao sijui katika kufanya hiyo sensa ya michezo wanakuwa na

utaratibu gani, ningewaomba haya kama kweli tunakusudia kudumisha utamaduni wetu basi wakayazingatia kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisichukue muda wako mwingi nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa na mimi fursa nichangie ripoti hii ya Kamati iliyopo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati hii kwa ajili ya kufanya kazi zao kwa ufanisi kabisa na wametueleza mengi katika kutekeleza kazi zao na tumeona katika jitihada yao ambayo wanaifanya *Inshaallah.*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kwa hii Tume ya Utangazaji Zanzibar. Kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba niwapongeze sana Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kutekeleza kazi zake na kuona kilio chetu cha muda mkubwa na kukifanyia kazi kikamilifu. Kwa sababu tulikuwa wajumbe tunakuja hapa tunazungumza kuhusu mipango ya nchi yetu, maendeleo ya nchi yetu, matatizo lakini ilikuwa wale walengwa wananchi hawapati habari yoyote ile, lakini leo nawapongeza kwa sababu tunafanya kazi kuanzia asubuhi mpaka usiku bila ya kukosa, bila ya kuchelewa wanafanya kazi na wananchi wanapata faida na leo imezaa tija sana kazi yao.

Kwa sababu wananchi wanaangalia Televisheni Zanzibar na Redio Zanzibar kusikiliza, bila ya kukosa na wanakuwa wanakaa kwa zamu hasa wanafuatilia. Kwa hivyo, naomba jitihada yao waendelee kuifanya na kumuomba Mhe. Waziri aendeleze kazi hii nzuri iliyopo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo yote kizuri chochote kile hakikosi kasoro yake. Kwa hivyo mimi nawaomba tunaingia katika mabadiliko sasa hivi tunatoka kwenye *analogy* tunaingia kwenye *digital.* Tatizo letu sisi Wazanzibari huwa tunaaza tu mambo yetu lakini hatufiki mwisho na siku zote mimi huwa nasema kufanya kitu ukakianza lakini usikimalizie ni sawa kama hujafanya kitu chochote, kwa hivyo mtu akija ataona kama hujafanya kitu. Kwa hivyo, naomba sasa hivi tusianze tumalizie ili mzigo tukiubeba tuufikishe mwisho wake.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tulianza kwa Televisheni lakini kinyume chake kuna watu wamekuja wametupita, sasa ushauri wangu, natoa ushauri kwamba sasa hivi wakati umefika kwa *TVZ* au wanaita *ZBC* kwa Redio kuwa wakati umefika tukianza asubuhi mpaka asubuhi ya pili tusifunge saa sita. Kwa sababu wenzetu sasa hivi hakuna televisheni yoyote inayomalizia saa sita au redio, saa nyengine mnatuletea vipindi vishatufurahisha pale tunaangalia muda mchache unasikia paa, televisheni inafungwa. Kwa maana hiyo tunawaomba jamani sasa hivi ule muda wa kufunga saa sita umalizike, watu wanajitayarisha na vipindi vyao wanaweka rekodi zao anakuwepo mmopja tu au wawili fundi mitambo na muendeshaji vipindi mpaka asubuhi lakini wameshaweka rekodi zao. Mimi natoa ushauri kuwa sasa hivi tumefika wakati tusifunge tena saa sita jamani, kwa sababu mnatuumiza vipindi vishatufurahisha mnatukatia na siku nyengine kunakuwa na mambo muhimu sana ambayo yawepo mpaka asubuhi sasa tunakuwa tunajilazimisha.

Mhe. mwenyekiti, mfano siku za maulidi ikifika saa sita pengine maulidi yamenoga watu wanataka waone wao saa sita ni kufunga watu wanaondoka. Kwa hivyo, naomba ushauri wangu uzingatiwe kuwa sasa wakati umefika vipindi vyetu kuendelea mpaka asubuhi.

Suala jengine ninalotaka kulizungumza ni suala alilozungumza Mhe. Abdalla Mohamed Ali kuwa televisheni za Pemba mshatufungia mitambo lakini bado hatujafaidika na televisheni hizo. Wananchi wa Pemba bado hawajafaidika, TV inaonesha chenga tupu hupati chochote hasa kule kwetu Micheweni hatufaidiki kabisa. Kwa hivyo naomba kama kuna kifaa ambacho kimekosekana serikali ifanye jitihada ili na sisi kule Pemba tufaidike na matunda yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala la Redio Jamii iliyoko Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, serikali iliona kwa nia nzuri kama wanajamii wa Micheweni wanahitaji na wao wafaidike na nguvu za serikali yao, lakini sasa mimi ninachokiomba kuhusu redio hii ya Micheweni kwanza kabisa kuwa redio hii haina bajeti yoyote inayopitishwa kwa serikali kwa hivyo watu hao wanakuwa wanapata shida sana kwa sababu hawana msaada, wanakuwa watendaji wa redio hii wana wakati mgumu kweli kweli.

Kwa hivyo, naiomba serikali pamoja na kuwa ni redio jamii, lakini jamani tena kila siku tunakuja tukisema hapa tu mnaijua Micheweni ilivyo, hali ya Micheweni ilivyo mnaijua, kwa maana hiyo naomba mimi namuomba Mhe. Waziri anayehusika basi aone kuwa kuna haja ya kuwaombea hawa wanajamii wa Micheweni hii redio yao japo robo tu ya kumi kuwezeshwa ili waweze kumudu kufanya zile kazi zao, lakini wanafanya kazi katika wakati mgumu hata kulipia ule umeme inakuwa ni ngumu. Namuomba Mhe. Waziri alione hili.

Jengine kuhusu redio jamii kuna vijana ambao walianza kufanya kazi pale kuajiriwa, lakini mara moja wamefukuzwa kazi vijana wasiopungua sita wa Micheweni.

Sasa namuomba Mhe. Waziri ili kulitatua suala hili na kulijua kama kuna tatizo gani, basi namuomba yeye pamoja na mimi, naibu waziri na wakurugenzi twende Micheweni tukajue sakata hili lilianza vipi mpaka vijana hawa kufukuzwa kazi kuna tatizo gani? Kwa sabaub mara moja Mkuu wa Wilaya kawasimamisha kazi hawa na kuna mmoja ni fundi mitambo alianza na hii kazi lakini na yeye kasimamishwa na wamebaki watu watatu tu.

Kwa hivyo, naomba suala hili namuomba Mhe. Waziri kama analijua hili sakata basi anipe maelezo na mimi nilijue, maana mimi sijui limeanzaje naona watu wamefukuzwa tu, na kama halijui basi tufuatane twende pamoja ili tupate maelezo na kujua matatizo yao kuliwa na nini mpaka ikabidi kufukuzwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tatu za ziada.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, hata sijazungumza, lakini sibishani nawe Mheshimiwa nakubali. Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitakalozungumza kidogo naheshimu muda wako ni suala la utalii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuhusu suala hili la utalii limezungumzwa sana na wenzangu lakini na mimi nitie fupa kama kuna watu matajiri wa haya mahoteli kuwa watu wamewafukuza kazi kwa ajili ya kuongezwa hii mishahara. Kwa hivyo, kuna ndugu zetu ambao wamefukuzwa kwa uonevu hivyo namuomba waziri anayehusika aendelee kulifanyia kazi suala hili ili kulichunguza na kuona kama kuna matatizo gani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu kiti chako nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa *order paper* yetu tuliyonayo leo tulitakiwa tujadili ripoti za kamati mbili, lakini hadi dakika hii tumejadili kamati moja na bado wachangiaji wapo wengi, sasa basi tuwaombe hawa wachangiaji wawili ambao wamebakia wawe wastahamilivu ili tuweze kuwapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri waweze kujibu baadhi ya hoja tuweze kuendelea na ile kamati ya pili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika Ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Habari, Uwezeshaji na Utalii. Na mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nipongeze kamati hii kwa kazi nzuri waliofanya, lakini zaidi ya hapo niipongeze kamati kwa namna ambavyo wanashirikiana na wizara zetu katika kutusimamia katika utekelezaji wa shughuli zetu.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mara zote kamati hii imekuwa *very aggressive* kwa kweli katika kuhakikisha kwamba sisi mawaziri tunasimamia vizuri shughuli zetu kwa maslahi ya wananchi. Mwenyekiti wake dada yetu, mama yetu, Mhe. Asha Bakari Makame kwa kweli anaiongoza vizuri na kwa namna ambavyo ninamuona anapata mashirikiano mazuri kutoka kwa wajumbe na nawaomba waendelee kushikama ili kazi yao iendelee kupata matunda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwa ruhusa yako nichukue nafasi ya kujaribu kutoa ufafanuzi wa baadhi ya michango ambayo Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi wamejaribu kuichangia katika ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Habari imezungumzwa sana na kwa umuhimu wetu katika nchi yetu sekta hii na wajibu wao Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waweze kuizungumza na kufanya hivyo ili kutuzindua katika kusimamia na kuiongoza zaidi. Pameelezwa utaalamu mdogo katika kutusukuma kuelekea *digital*. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakiri hilo ni kweli, lakini hatukukaa tu kwamba tuna utaalamu mdogo ndio basi, tunashirikiana na Sauti ya Ujerumani *Deutschewelle* kutusaidia utaalamu kwa vijana wetu ili tutakapoanza basi tuwe tumeiva.

Kwa hivyo, ni kweli hivi sasa tuna utaalamu mdogo lakini wizara haikukaa tu kwamba ina utaalamu mdogo basi, inafanya kazi, inashirikiana na Shirika hili la Utangazaji lenye uzoefu wameanza siku nyingi na naamini kwa namna vijana walivyochangamkia basi tutafika pazuri tukianza tutakuwa tumeiva.

Eneo jengine ambalo limezungumzwa ni suala la maslahi ya wafanyakazi wa Shirika la *ZBC*. Mhe. Waziri aliyepita amejitahidi kwa kiasi kikubwa katika kuona kwamba maslahi ya wafanyakazi hasa *overtime* zao. Taarifa niliyonayo ni kwamba wanadai *overtime* za kikao kilichopita sio tokea bajeti hapana, taarifa nilizoarifiwa ni kwamba kuanzia kikao kilichopita na naahidi kwamba tutajitahidi kuona kuwa *overtime* zao zinalipwa kwa wakati muwafaka.

Suala la masomo ya Uholanzi na maposho yao ni kweli Mhe. Mwenyekiti, kwamba mwaka 2009 kuna wafanyakazi walipelekwa Uholanzi na hadi leo bado hawajalipwa marupurupu yao. Tutajitahidi kufanya hivyo Mheshimiwa kuwalipa na mimi nitoe wito kwa wafanyakazi wale ikiwa wanazo kumbukumbu sahihi basi waniletee ofisini kwangu nitajitahidi kutafuta namna yoyote lakini pesa zao waweze kulipwa, lakini wasinijie na maneno waje na kumbukumbu. Sasa ikiwa wanazo kumbukumbu sahihi waniletee Jumanne tukijaaliwa asubuhi nitajitahidi Inshaallah na uongozi na watendaji wangu tuangalie kukata pua tuunge wajihi lakini waweze kupewa pesa zao kwa kadiri ya *other chages* za wizara yetu zitakavyoruhusu.

Kuhusu tatizo la usafiri tunalo tutajitahidi kutafuta utaratibu katika bajeti inayokuja ama kutengeneza magari yaliopo ili wafanyakazi waweze kusaidiwa au kununua gari nyengine katika bajeti hiyo lakini wafanyakazi waweze kwenda kazini na kurudi kama ambavyo wafanyakazi wengine wanakwenda katika maeneo mengine ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi za Gazeti la Zanzibar Leo tumezipokea na nahakikisha kwamba Waheshimiwa Wajumbe pongezi hizi zitatusaidia kujiimarisha badala ya kubweteka.

Kuhusu hali ya Sekta ya Utalii. Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Utalii ndio sekta kiongozi katika nchi yetu, mapato mengi ambayo tunayapata ya kuendeshea serikali yetu yanatoka katika Sekta ya Utalii. Kuna mambo mengi ambayo yameanza kushughulikiwa na tutajitahidi kushughulikia.

Suala la ajira limekuwa likipigiwa sana kelele na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa muda wa miaka mingi. Na hili Mhe. Mwenyekiti, naomba tushirikiane katika hili, tuna tatizo kubwa ambalo Waheshimiwa Wajumbe katika majimbo yao lazima tushirikiane na viongozi wengine kuona kwamba haya hayatokei tena. Tatizo kubwa watu wanaonekana ni wajanja kupata Uzanzibari kiurahisi, na hili halihusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo lakini ni suala letu sote. Uzanzibari tunajua namna unavyopatikana na sisi tusipokuwa makini katika hili Mhe. Mwenyekiti basi walio Wazanzibari halisi watakosa haki wapate Wazanzibari ambao wamefanya ujanja katika kupata uzanzibari halisi.

Kwa hiyo hili linatuhusu sote katika Baraza hili Mhe. Mwenyekiti, linahusu viongozi wengine katika ngazi za wilaya na shehia ni jukumu letu kuhakikisha kwamba tunatafuta utaratibu wa kujisimamia ili kuona uzanzibari unapatikana kwa wale wanaohusika. Vyenginevyo tukilegeza kamba katika hili watu wanaupata uzanzibari na watautumia uzanzibari huo kujijaza katika mahoteli ya kitalii halafu sisi tutabaki huku huku kulalamika. Kwa hivyo, hili naomba tushirikiane.

Lakini pamoja hayo sisi wizara yetu tutashirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kuona kwamba tatizo hili limepata ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Makumbusho na Mambo ya Kale na Magofu yake kijumla ni eneo ambalo nitajaribu kulisimamia kwa kiwango kikubwa, na jitihada ambayo imefanywa kabla Mhe. Mwenyekiti, tutaiendeleza ili kuona kwamba magofu haya yaendelee kutoa taswira halisi ya utamaduni na historia ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia swahibu wangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk akizungumza kwa ukali suala la ajira katika mahoteli ya kitalii namuahidi kwamba tutalishughulikia na mashirikiano yake yanahitajika sana katika kulikamilisha hili. Haya ni mambo yetu sote lazima tushikamane kuona kwamba Wazanzibari ndio wanafaidika katika ajira za utalii.

Na katika suala hili naomba kuahidi kwamba sheria tuliyopitisha juzi ya Utalii,
kanuni zake tutakazotunga tutahakikisha kwamba Mzanzibari anapewa kipaumbele. Katika utungaji wa kanuni zenyewe basi naahidi kwamba tutashirikiana kwa karibu na kamati yako ya Baraza la Wawakilishi ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ili kuona kwamba yale ambayo Baraza la Wawakilishi inayapigia kelele basi yamezingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la urushaji wa matangazo ya *ZBC* hasa Pemba ninavyoelewa mimi matangazo ya *shortwave* ni kweli yalikua hayapatikani, lakini kuanzia mwezi huu wa tatu baada ya msaada mkubwa wa wenzetu wa China tayari mtambo ule wa *shortwave* unafanya kazi na nawaomba wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi wajaribu kui-*tune* na kwa kweli inapatikana bila ya matatizo.

Kuhusu kifaa cha *UPS* naomba nitofautiane kidogo na ripoti hii ya kamati pengine kuna matatizo ya uchapaji. Taarifa niliyonayo ni kwamba hizi zimenunuliwa nne badala ya tatu, moja imefungwa Masingini, ya pili iko Chake Chake – Mkanjuni na moja imefungwa Mizimiumbi. Kwa hivyo, rekodi ya kamati kidogo ina makosa

hapa naomba warekebishe huo ndio ukweli wenyewe. Kama nilivyosema kwamba *frequency* ya *shortwave* inapatikana ni nambari 25 na 49 katika redio zetu kwa hiyo tufungueni itapatikana bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nilifafanue ni suala la Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna wafanyakazi waliokua wakijitolea waliondolewa pale katika kituo cha Redio Jamii Micheweni. Sasa sio wafanyakazi ambao walikua tayari wameajiriwa, naona Mhe. Subeit Khamis Faki ametia kama wafanyakazi waliokuwepo pale walioajiriwa. Kwa hivyo, naomba anipe muda mimi na uongozi wangu wa wizara akitaka na yeye basi twende mpaka Micheweni katika Redio ya Jamii tukazungumze na Mkuu wa Kituo na Mkuu wa Wilaya basi tutajua sababu ambazo wameondolewa pale. Nina hakika kwamba taratibu zimefuatwa na kama anafuata viongozi sisi tutajaribu kutafuta ufumbuzi. Lakini nataka ieleweke kwamba si wafanyakazi wa kudumu kwa mujibu wa taarifa nilizonazo.

Mhe. Mwenyekiti, masuala naona yako mengi lakini mengi yalikua ni ushauri, sasa ule ushauri wote tuliopewa katika kuiendeleza wizara hii nawaahidi Waheshimiwa Wajumbe kwa maelekezo yao na kwa ushauri wao tunauchukua tutaufanyia kazi na kwa pamoja tutahakikisha kwamba ifikapo mwezi Disemba tukijaaliwa na sisi Zanzibar tutaingia katika *digital* kama ambavyo wenzetu wa Afrika Mashariki pengine wataingia. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa ufafanuzi kwa yale maeneo ambayo yamenigusa katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Lakini vile vile niwashukuru Kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa jinsi walivyotoa maelekezo hasa kwa zile kasoro ambazo wameziona na kwa nasaha na mapendekezo ambayo wameyatoa wenyewe chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Asha Bakari Makame. Sina budi kutoa pongezi na nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa ruhusa yako na mimi nijaribu kutoa ufafanuzi kwa yale maeneo ambayo kidogo yameguswa kwa sababu sikupata maeneo mengi sana labda kwa sababu ya udogo wa wizara yenyewe lakini nitajitahidi kadri ninavyoweza nitoe ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, masuala zaidi yaliyojitokeza katika sekta hii zaidi yamejikita kwenye migogoro. Niseme tu kwamba ni kweli mgogoro huu ni wa zamani sana tofauti na tunavyofikiria labda umeanza hii miaka ya karibuni, lakini migogoro iko toka miaka ya 50 na sio Marumbi na Chwaka tu. Sehemu nyingi kulikua na migogoro kama hiyo kama vile Makunduchi na Mtende, Makunduchi na Jambiani, Kojani na wapi, naweza kusema ni migogoro ya kizamani kwa kweli. Lakini sehemu nyengine *Alhamdulillah* tunashukuru kwamba imezimika na ulioonekana zaidi ni huu mgogoro wa Chwaka na Marumbi ambao kwa kweli kila kukicha unazidi kuja juu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba nimshukuru Mhe. Waziri kabla ya kuondoka kwake aliunda tume ya kufanya uchunguzi juu ya mgogoro huu ili kutafuta chanzo hasa cha mgogoro huu yaani wa Marumbi na Chwaka. Kwa kweli tume ile tayari imeshatoa ripoti yake ni hii hapa bado sijaisoma nimeipata leo lakini nitaifanyia kazi ili nihakikishe kujua nini chanzo cha mgogoro ule. Kwa sababu tume imefanya kazi vizuri na imewashirikisha wenyewe kwa hivyo nina imani kwamba chanzo cha mgogoro ule tayari kimeshapata ufumbuzi na tutajaribu kutumia hekima na busara kuhakikisha kua mgogoro huo unaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niseme juu ya mgogoro huu ni kwamba tuliomba humu kuna masharti ambayo labda yapunguzwe. Mimi naomba nipewe muda kidogo niangalie hii ripoti ili kuona nini hasa kilichojiri. Mhe. Mwenyekiti, mimi nina imani hakuna mgogoro usiokua na ufumbuzi isipokua kama walivyoeleza baadhi ya wajumbe naweza nikakiri kwamba kuna ubinafsi na nina imani vile vile kwamba kuna baadhi ya viongozi wanahusika na mgogoro ama kwa njia moja au kwa njia nyengine. Lakini ripoti ipo nitaisoma kwa kina na mimi mwenyewe nitafanya utafiti nikijumlisha nina imani kwamba nitapata ufumbuzi nini cha kufanya.

Lakini vile vile ukiangalia na masharti ya uvuvi nayo nafikiri si vibaya tukaangalia kama kulegeza kamba kidogo ili tuhakikishe wananchi wetu nao wanapata riziki zao kwa njia ambayo itakubalika. Halafu kisichozungumzika tutazungumza tutatazama athari kiasi gani zitapatikana lakini lazima na wavuvi nao wawajibike wabadilike kwa sababu dunia inabadilika na bahari halikadhalika inabadilika kwa hivyo tutakaa pamoja ili tukubaliane. Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na sheria ambazo zinawabana basi tutaziangalia upya kuona kiasi gani tunaweza tukazilegeza ili wananchi wapunguze kilio chao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Mshimba nae alizungumzia suala ambalo nimelizungumzia kwamba ni tatizo la muda mrefu, hiyo inakubalika lakini nina imani karibu tutapata ufumbuzi.

Mhe. Hija Hassan Hija nae alisema kwamba pale ambapo Mhe. Said Ali Mbarouk amefikia hatua nzuri tu kwa hivyo tuiendeleze na mimi naahidi kwamba nitaiendeleza sitopuuza na nitafuata nyayo zake pakuongeza na mimi nitaongeza.

Mhe. Fatma Mbarouk Said nae katoa nasaha vile vile kwamba lazima tuitumie bahari vizuri, tutumie mazao ya baharini kwa sababu ya kupata lishe bora. Nakubaliana nae kwa sababu *white meat* siku zote ndio inakubalika katika afya ya binadamu na sio *red meat* na hata madaktari wametushauri hivyo.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali nae vile vile kazungumzia suala hilo hilo la migogoro baina ya maeneo. Halikadhalika naahidi kwamba suala hili halitochukua muda litamalizika na kwa taarifa tu ni kwamba kesho kutwa Jumanne tutakuwa na kikao kule Dunga ambacho kitawashirikisha wadau wote. Vile vile yote ni miongoni mwa kutafuta nini chanzo cha mgogoro. Naamini kwamba tukiwa wakweli na tukiondoa ubinafsi basi mgogoro huu utaondoka. Mimi naamini kwamba ni ubinafsi na kuna baadhi ya viongozi ambao wanahusika ndio maana mgogoro ule unadumu, lakini vyenginevyo hakuna sababu yoyote ya kudumu mgogoro ule.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe kwa kweli maeneo makubwa yalikua ni mgogoro ndio suala ambalo limetawala katika sekta hii vyenginevyo hakukuwa na zaidi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia mimi niseme tu kwamba naliomba Baraza lako hili tukufu linipe muda ili niisome ripoti kesho kutwa tukijaaliwa kikao na mimi mwenyewe nitafanya utafiti basi ninahakika tutafungua ukurasa mpya. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala ambayo tuliyazungumza yanahusu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na pamoja na kwamba Waziri hayupo lakini serikali kwa mujibu wa katiba inawajibika katika Baraza la Wawakilishi kushirikiana kwa pamoja. Sijui masuala yale tunaweza kuyapatia ufafanuzi kutokana na hili.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Wakati Waziri wa Mifugo na Uvuvi anaendelea kujibu baadhi ya hoja nilikua najaribu kuwasiliana na safu ya mbele ya Mawaziri hapa ili niweze kufahamu namna gani itaweza kujibu yale masuala au hoja ambazo ulikuwa umezitoa Mhe. Mjumbe.

Lakini inaonekana ni hoja ambazo zilikua zinataka maelezo ya kina kabisa. Kwa hivyo basi, nichukue fursa hii kukuomba Mhe. Mjumbe kwamba taarifa kamili ya maelekezo ambayo ulikuwa umetoa utaipata kupitia kwa Waziri husika kwa njia ya maandishi. Ahsante sana Mhe. Mjumbe.

Mhe. Assaa Othman Hamad (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa mara nyengine tena ili nami niweze kukamilisha ngwe hii ya taarifa ya kamati yangu kama nilivyoiwasilisha asubuhi ya leo. Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya kamati imechangiwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu tisa (9), kati yao *backbenchers* walikua ni saba na Waheshimiwa Mawaziri walikua ni wawili. Kwa ruhusa yako naomba niwataje mmoja baada ya mwengine.

1. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Fatma Mbarouk Said
6. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
7. Mhe. Subeit Khamis Faki
8. Mhe. Said Ali Mbarouk
9. Mhe. Abdillah Jihad Hassan

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla nitoe shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kwanza kwa *backbenchers* hasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa pongezi zake za dhati alizotupa kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo yeye mwenyewe kaithibitisha iliyofanywa kwenye kitabu cha ripoti iliyokusanya kwa awamu tatu zilizopita. Tumepokea pongezi zake kwa niaba ya kamati yangu na kwa niaba ya Mwenyekiti wangu mahiri Mhe. Asha Bakari Makame ambaye leo ndio ninamuwakilisha.

Mhe. Mwenyekiti, wa pili ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tunampongeza kwa dhati kwamba nae amepita mle mle ambamo kamati yangu kwa muda wote ilikua inafanya kazi na Wizara husika juu ya mambo gani ambayo yataweza kuleta na kuharakisha maendeleo endelevu ya jamii ya Wazanzibari, hususan kwenye suala la ajira na jinsi gani taratibu zifanywe ili waweze kubainika wageni ni wepi, haki zao ni zipi na Wazanzibari bila ya kupotezewa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, napokea pongezi za Mhe. Hija Hassan Hija ameliona vile vile kakubaliana na kauli na msisitizo wa kamati yangu juu ya malipo ya wafanyakazi wetu kwenye Sekta ya Habari. Hili Mhe. Mwenyekiti, tunalikazia nguvu kwani haya ambayo tunaendelea nayo sasa hivi ni uwezo wa Mwenyezi Mungu na kazi nzuri wanayoifanya wao.

Mhe. Mwenyekiti, mwengine ni Mhe. Fatma Mbarouk Said tunapokea pongezi zake za dhati na yeye kama unavyomfahamu ni mtaalam kwa kiasi chake, ni mheshimiwa mahiri sana, jambo ambalo linamuweka kwenye nafasi na tasnia nzuri ya habari ambayo pia kabla ya kufika kwenye chombo hichi ilikua ni sehemu ambazo kazifanyia kazi. Tunakupongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, mwengine ni Mhe. Abdalla Mohammed Ali tunapokea pongezi kwa niaba ya kamati yangu na nakushukuru sana kwamba umeona haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutafuta na kuona ni kwa namna gani gazeti letu sasa la Zanzibar Leo liweze kuchapishwa hapa ndani na kurudisha heshima ya Zanzibar ambayo imetupotea kwa miaka zaidi ya 50 iliyopita.

Mhe. Mwenyekiti, mwengine ni Mhe. Subeit Khamis Faki tunapokea pongezi za kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wangu na yeye ameeleza kilio chake lakini Mhe. Waziri nashukuru amefafanua kwa makini sana.

Mhe. Mwenyekiti, mwengine ni Mhe. Said Ali Mbarouk ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo amejikita zaidi kutoa ufafanuzi kwenye sekta hiyo ya habari. Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba kazi ile iliyofanywa na kamati yangu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wameiona na mheshimiwa mwenyewe amekiri. Kamati kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti tuko pamoja na Wizara zote ambazo tumekabidhiwa kwa mujibu wa kanuni zetu na katiba ya nchi hii, tutashirikiana kuhakikisha kwamba tunawafikisha Wazanzibari pahala stahiki.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache natoa shukrani za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa uvumilivu, mashirikiano makubwa waliyonipa leo tokea asubuhi hadi jioni hii kuweza kuikamilisha kazi hii muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar. Mungu libariki Baraza la Wawakilishi, Mungu ibariki Zanzibar, Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaoipokea ripoti wanyooshe mikono juu, wanaoikataa, walioipokea wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba kutoa taarifa kwamba Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imepokelewa rasmi.

KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi hayupo kwa hivyo ndani ya ratiba yetu ya leo shughuli zote tumezimaliza.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile Mwenyekiti wa Kamati hayupo na taarifa tutashindwa kuipata, sasa basi napenda kuchukua fursa hii kutoa matangazo niliyonayo.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunatangaziwa kwamba kesho siku ya Jumamosi tutakua na semina kama ambavyo taarifa mmekwisha kuletewa huu ulikuwa ni ukumbusho. Semina hiyo itaanza saa 3:00 asubuhi katika viwanja vya Baraza la Wawakilishi hapa tulipo na usajili utaanza saa 2:30 za asubuhi ya kesho.

Baada ya hapo, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kwenda vizuri na salama hadi kufikia hapa ambapo tumefika siku ya leo. Nakushukuruni kwa mashirikiano ambayo mmenipatia na mpaka hapa naomba kuchukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi siku ya Jumatatu tarehe 16/04/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:22 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 16/04/2012 saa 3:00 asubuhi)